3 SEPTEMBA, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Saba – Tarehe 3 Septemba, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani *(Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute)*.

MHE. PATALI S. PATALI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji Maendeleo ya Kijani Duniani *(Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute)*.

MHE. ZUBERI Y. MFAUME K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu wa Bunge.

SPIKA: Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu.

Mheshimiwa Sichalwe.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 14 Novemba, 2025 Mheshimiwa Rais wetu alipokuwa akilihutubia Bunge hili kwa mara ya kwanza alitoa kauli ya faraja na ya matumaini kwa wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mkulima ni mwekezaji na kilimo ni biashara. Kwa kweli tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kauli hii. Kwa nyakati tofauti tofauti tumeona Serikali ikitoa hamasa kuwafanya wakulima walime kilimo bora na ambacho ni cha biashara. Kwa kufanya hivyo, Serikali imekuwa ikiweka mbolea ya ruzuku kwa wakulima wetu, lakini mbolea hii ya ruzuku pamoja na viuatilifu vingine ambavyo Serikali inatoa kwa wakulima kufikia azma na kauli ile ya Mheshimiwa Rais vimekuwa vikifika nje ya msimu. Kwa mfano, utakuta ni msimu wa kupanda, mbolea inakuwa haijafika; ni msimu wa kukuza, mbolea haijafika; ni msimu wa kunenepesha mazao, mbolea inakuwa haijafika.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina kauli ipi katika kuhakikisha kwamba mbolea zote za ruzuku na viuatilifu vyote ambavyo Serikali imedhamiria kumfanya mkulima awe ni mwekezaji na kilimo kuwa biashara, viweze kuleta tija? Serikali imejipangaje kuhakikisha mbolea inafika kwa wakati? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kujibu swali la Mheshimiwa Condester kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais wakati analihutubia Bunge alitoa kauli hiyo ya faraja kwa wakulima kuhusiana na suala la kutoa ruzuku. Nitumie Bunge lako Tukufu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hiyo, kwani tangu atoe kauli hiyo, Serikali yake anayoiongoza imetoa fedha nyingi sana kwenda kwenye ruzuku. Ninadhani takribani shilingi trilioni moja ambayo imekwenda kwenye ruzuku.

Mheshimiwa Spika, kufuatia fedha hizo nyingi za ruzuku, tumeona mabadiliko katika uzalishaji kwenye mikoa yetu. Juzi nilikuwa kule Katavi, nilielezewa kwamba uzalishaji umevuka malengo wakiwa wamezalisha zaidi ya tani milioni 1.5. Kwa hiyo, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais aliahidi na kweli ametekeleza kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge alichosema, kwamba kumekuwepo na changamoto kuhusu uianishaji wa ruzuku na msimu wa kilimo. Imekuwa bahati mbaya sana kwamba jambo hili limetokea, lakini linatokana na sababu ambazo zipo nje ya mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, dunia imeshuhudia mtiririko ama mfuatano wa *external shocks,* matatizo ambayo yapo nje ya mipaka ya nchi zetu hizi husika hasa zinazoagiza bidhaa hiyo. Tulishuhudia mwaka mmoja wakati Mheshimiwa Rais ndio ametoa ahadi hiyo, kulikuwepo na *lockdown* dunia nzima na mbolea inaagizwa kutoka nje. Kwa hiyo, kufuatana na *lockdown* hiyo

iliyotokana na UVIKO 19, *lockdown* hiyo iliathiri mnyororo wa ugavi, au mnyororo wa usafirishaji wa bidhaa hiyo. Fedha ilikuwepo, ahadi ilikuwepo, nia ilikuwepo lakini usafirishaji wa bidhaa hiyo kutoka inapozalishwa ilileta matatizo.

Mheshimiwa Spika, ukiathiri mnyororo kwa mwaka mmoja hadi urudi katika hali ya kawaida panakuwepo na athari zinazotokana na baada ya tatizo. Kwa maana hiyo, kukatokea mlundikano kutoka kule kwenye uzalishaji, pia kukatokea na mlundikano wa *order* zile ambapo zinatakiwa maeneo mengine. Kwa hiyo, mnyororo wa kupata bidhaa ile ukawa na shida.

Mheshimiwa Spika, tukiwa tu tumemaliza UVIKO 19 likatokea jambo la mzozo wa Ulaya ya Mashariki ambao nao uliathiri uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa hiyo. Kwa maana hiyo, pamoja na nia ya Mheshimiwa Rais, pamoja na nia ya Serikali, pamoja na uwepo wa bajeti na fedha, lakini uliathiriwa na mtiririko wa usafirishaji wa bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, tungali tunakaa sawa kama Mataifa yanayoagiza bidhaa hiyo, kukatokea tatizo la uhaba wa upatikanaji wa fedha za kigeni, kwa wale mtakao kumbuka. Bidhaa hii inayoagizwa yote inatumia fedha za kigeni. Kwa hiyo, kuna kipindi tena tukawa na shida hiyo ya uagiziaji kutokana na uhaba wa fedha hizo za kigeni.

Mheshimiwa Spika, tuna Mataifa yaliacha bidhaa zao hapa bandarini kwetu kwa zaidi ya miezi sita, wengine tisa kwa sababu ya uhaba wa fedha za kigeni. Hiyo nayo iliendelea kuathiri mnyororo wa usafirishaji wa bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, tungali tumeyamaliza haya, yametokea tena haya ya Mashariki ya Kati ambayo nayo eneo ambalo ndiyo njia ya kupitisha mizigo yote mara kadhaa likawa linafungwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kweli wakulima wetu wameathirika, lakini sababu zimekuwa ni mnyororo wa matatizo haya ambayo yapo nje ya mipaka yetu ambayo yamekuwa yakiathiri mnyororo wa ugavi. Sasa ni nini Serikali inafanya?

Mheshimiwa Spika, kwa hatua za muda wa kati, Serikali ilikaa na waagizaji ikawaelekeza waangalie uwezekano wa kuagiza bidhaa kutoka nchi mbadala. Hili tunalolisema kwenye bidhaa hii, tumefanya pia kwenye bidhaa nyingine ikiwemo sukari. Tukaagiza mbolea kutokea nchi za Afrika hapa ikiwemo Morocco, tukawaambia wenzetu waagize kutokea China. Hii yote ilikuwa ni namna ya kuweza kutafuta ufumbuzi wa tatizo la upitishaji wa bidhaa hiyo ambayo ni muhimu kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo kwa muda mrefu, tumeendelea kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya aina hii hapa hapa ndani ya nchi yetu ili kuweza kuepuka matatizo haya yanayojitokeza yanayohusiana na usafirishaji wa bidhaa hiyo kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha hapa Dodoma kimeshaanza kufanya kazi. Vilevile tumeendelea kuhamasisha wakulima waendelee kutumia mbolea ya Minjingu ya kutoka Arusha ambayo wenzetu wa nchi jirani wanaitumia sana kuliko sisi Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea kuhamasisha viwanda vingine hasa hasa vya zile mbolea muhimu ambazo tumekuwa tukiagiza ili tuweze kuepuka adha hiyo anayoisema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwalipa waagizaji wa mbolea ili kuweza kuhakikisha pia wanakuwa na ukwasi wa kuweza kuagiza mbolea pamoja na pembejeo nyingine kwa wakati huku tukihimiza taasisi zetu zinazosimamia usambazaji huo, zinazosimamia sekta hiyo kufanya kazi kwa wakati kwa kuwa misimu hii ya kilimo siyo ya dharura, inajulikana mkoa gani msimu unaanza lini? Mkoa gani msimu unaanza lini? *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo.

MHE. BAZILIO K. MBWILO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna anavyojibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwa uhakika, na kwa ufanisi mkubwa. Ahsante sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba, ni muda sasa umepita tangu Serikali ilipotoa kauli ya kulipa maveterani wetu wa vita ya Kagera. Sasa ningependa kuuliza, je, ni lini Serikali itaanza rasmi kuwalipa hawa maveterani wetu? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Nimpongeze Mheshimiwa Mbwilo, Mbunge wetu wa Nkasi Kasikazini kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ilitoa kauli kuhusu kuwalipa maveterani wetu, wazee wetu walioipigania nchi yetu kizalendo kabisa kabisa katika vita vya Idi Amin.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwenye hili, kwa sababu jambo hili ni la tangu mwaka 1978/1979, na miaka yote hii lilikuwa halijafika hatua hii ya kuweza kuwalipa wazee wetu hawa.

Mheshimiwa Spika, nia ya dhati ya Mheshimiwa Rais imeonekana kwanza kwa kubadilisha sheria ili kuweza kuwatambua wapiganaji wetu hao waliopigana katika vita hivyo vya Idi Amin. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ambayo imefanya malipo haya yakachelewa muda wote ule, ilikuwa ni kwa sababu aina ya wapiganaji wetu waliokwenda kule, wengine walikuwa bado hawatambuliwi na sheria hizi za wastaafu wa jeshini kutokana na mazingira ya wakati huo.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea, Mheshimiwa Rais alielekeza, na ninakumbuka nikiwa Waziri wa Fedha pamoja na wenzetu wa upande wa Jeshi letu la Wananchi tulikaa kutekeleza

maelekezo hayo na baadaye Mwanasheria Mkuu alileta marekebisho hayo, na sheria ilisharekebishwa kuwatambua wazee wetu hawa. Sasa kilichosalia ni nini?

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni masuala ya kuianisha taratibu tu za kimalipo. Kama anavyojua Mheshimiwa Mbunge, Serikali tunatekeleza mambo yaliyopo kwenye ahadi, mambo yaliyopo kwenye mipango, lakini kuna taratibu za malipo ambazo zinasimamiwa na Sheria ya Fedha, Sheria ya Bajeti na pia na maelekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambapo kwa taarifa niliyonayo ilishafikia hatua nzuri kiasi kwamba ninaweza kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, malipo hayo yataanza ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nilitumie Bunge lako Tukufu kuwaelekeza Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kukaa pamoja ili kuweza kuharakisha mchakato huo, kwa sababu kwenye bajeti tuliweka na sheria tulishabadilisha. Kwa hiyo, sasa hivi ni hatua za kuainisha taratibu za kimalipo na jambo hilo litaanza ndani ya mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza tunampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya kama Msimaizi Mkuu wa Serikali na kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akifanya ziara kwenye mikoa mbalimbali ambayo wananchi walijitokeza kwa wingi kwa imani ya kiongozi wao pamoja na imani ya Serikali yao katika kutatua migogoro mbalimbali. Katika ziara zake, mbali na changamoto mbalimbali, lakini changamoto kubwa ambayo imejitokeza ni migogoro ya ardhi. Kati ya kero ambazo watu wengi walijitokeza zaidi ya 50% kwenye kutoa changamoto ni migogoro ya ardhi, ambayo ni pamoja na ardhi

ya wakulima na wafugaji, watu kuzulumiwa viwanja, na ardhi kwa vijiji ambavyo vimepakana na hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Waziri Mkuu alikuja mkoani kwetu, Jimbo la Bunda Mjini, akaona ni namna gani ambavyo watu wana changamoto ya ardhi, migogoro ya ardhi iliyokaa muda mrefu hasa mgogoro wa Nyatwali ambao mpaka leo hawajapatiwa majibu. Vilevile ukienda kule Lindi kuna migogoro ya wakulima na wafugaji, Morogoro na maeneo mengine yote ambayo yamezunguka hifadhi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani katika kumaliza migogoro hiyo kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Ester Bulaya kwa swali lake zuri. Ni kweli nimepita maeneo kadhaa ikiwemo Bunda, na nimejionea migogoro kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameainisha; na ameainisha vyema. Hii ni aina ya migogoro ya mtu na mtu, wananchi na hifadhi, wananchi na uwekezaji, wakulima na wafugaji na maeneo mengine kuna migogoro inayofanana na hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mkakati wa kukabiliana na changamoto ya aina hii. Kwa upande mahsusi kama alivyosema, unaohusisha fidia, ninampongeza Mheshimiwa Rais, katika Awamu yake, ametumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kulipa fidia maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo yalitwaliwa siku nyingi sana na wananchi, walishalalamika kwa muda mrefu sana, lakini Mheshimiwa Rais katika awamu yake ametoa fedha nyingi kuweza kulipa fidia, ikiwemo eneo la kule Liganga na Mchuchuma, kule Manyara kwenye eneo linaitwa kwa kilugha cha Kiiraki gumugumu nitawauliza watani zangu kule waniambie. Pia eneo la Nyatwali, maeneo ya viwanja vya ndege ikiwemo Dar es Salaam, Kilimanjaro na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo mahsusi kama la Nyatwali tayari fidia ya awali ilishalipwa, zaidi ya shilingi bilioni 48, lakini ilikuja kuonekana kuna baadhi ya eneo lilikuwa bado halijalipwa fidia na ilielekezwa ifanyike tathmini upya, tathmini ambayo inaendelea hivi tunavyoongea. Niwaelekeze wale wanaofanya jukumu hilo kukamilisha haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nilikuwa kule Bunda, ninakumbuka eneo moja linaitwa Kwamjapani, kitu kama hicho, na *blocks* nyingine ambazo zipo mle ndani ya eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tathmini ikishakamilika, ulipaji utaendelea kama ambavyo imefanyika katika maeneo mengine ikiwemo hilo la Nyatwali kwa maeneo ambayo yalishalipwa. Kwa kuwa sijamaliza majumuisho Mkoa wa Mara, nimwambie Mheshimiwa Mbunge nitakaporudi kumalizia Bunda *DC,* basi tutajadiliana wakiwemo na wataalamu wa eneo hilo husika ili tuweze kuchukua hatua inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia kupitia Bunge lako Tukufu hapa tulileta mapendekezo, na Bunge lako likapitisha. Sasa tutakuwa na fedha ambayo kutoka kwenye makusanyo inaenda moja kwa moja kwenye mfuko wa uwekezaji na maeneo mahususi ya uwekezaji ili pale Serikali inapotoa maeneo kwa ajili ya uwekezaji ama kwa sababu yoyote ile, pawe na fedha mahususi kwa ajili ya kulipa fidia ili tusilimbikize madeni kwenye maeneo ambayo Serikali imeyatwaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa migogoro mingine, tumeendelea kusisitiza matumizi bora ya ardhi, na jambo hili la migogoro ya ardhi ni jambo *sensitive* sana kwa sababu idadi ya watu inaongezeka, lakini ardhi ni ile ile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumesema tuheshimu matumizi bora ya ardhi ili kuheshimu ardhi ambayo ni mahususi kwa ajili ya kilimo, na tuheshimu ardhi ambayo ni mahususi kwa ajili ya ufugaji ili kuepusha mizozo inayoweza kujitokeza kutokana na mahitaji haya ya wakulima na mahitaji ya ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye haya mengine ambayo yanahusisha dhuluma za hapa na pale za mtu na mtu, Serikali tunaangalia upya taratibu tunazotumia kushughulikia migogoro hii. Tumekuwa tukitumia Mabaraza ya Ardhi na katika ngazi fulani migogoro hiyo inaenda Mahakamani. Serikali inaendelea kufanya mapitio kuona kama tuendelee na Mabaraza ya Ardhi au migogoro hii yote ipelekwe Mahakamani, kwa kuwa sasa Mahakama zipo maeneo mengi katika wilaya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni swali la msingi na katika hatua zote hizo za aina ya migogoro aliyoainisha, Serikali inaendelea kushughulikia, na jana Mheshimiwa Rais wakati anawaapisha Wakuu wa Mikoa, aliwaelekeza Wakuu wa Mikoa wote kwenda kushughulikia matatizo haya ya migogoro ili wananchi waweze kujiletea maendeleo wakiwa na utulivu bila kuhangaika kila siku na masuala haya ya migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemwelekeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI awaandikie Wakuu wa Mikoa maelekezo yale mahususi ambayo Mheshimiwa Rais aliyatoa jana wakati akiwaapisha Wakuu wa Mikoa. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Edibily Kinyoma.

MHE. EDIBILY K. KINYOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza nianze kuishukuru Serikali kwa jitihada kubwa ambayo imezifanya hasa kwenye uwekezaji upande wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanyika kwenye Sekta ya Viwanda, bado kuna shida kubwa hasa kwenye upande wa saruji. Bei ya saruji hivi karibuni imekuwa ikipanda kwa kasi sana. Nikinukuu baadhi ya maeneo, kwa mfano mwaka 2015 wakati Dangote imeanzishwa, bei ilishuka mpaka kufikia *around* shilingi 10,000 lakini 2020 ilikuwa *around* shilingi 13,000, na shilingi 14,000. Sasa hivi, tunavyozungumza iko zaidi ya shilingi 20,000, baadhi ya maeneo nchini inafika mpaka shilingi 25,000 mpaka 26,000.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kauli ya Serikali kuhusiana na kuanzisha tathmini ya gharama halisi ya uzalishaji wa *cement* nchini ili ije na bei elekezi kwa wananchi wetu ambayo itatoa unafuu kwenye sekta ya ujenzi Tanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nijibu swali zuri la Mheshimiwa Edibily, Mbunge wa Kasulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa kulileta swali hili zuri linalohusiana na bei ya *cement*. Jambo hili ni jambo linalogusa maisha ya kila Mtanzania na nimelifurahia sana kwa sababu ndani ya Serikali pia kwa nyakati tofauti tumekaa kushauriana, kujadiliana kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nikiwa Waziri wa Fedha wakati ule, tulikaa na kaka yangu Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, tukawa tunajadiliana kikao cha chai, tukisema hivi vifaa vya ujenzi ikiwemo *cement,* hivi hatuwezi tukatengeneza bei zake zikawa kama za *Coca-Cola* hivi ambayo bei yake ya Dar es Salaam na Kigoma ni hiyo hiyo?

Mheshimiwa Spika, tukaangalia hivi ni nini na nini kinachofanya bei za *cement* zitofautiane? Tuligundua kuna vitu vingi na vingine kwa wakati huu vinaweza visitekelezwe kwa kiwango hicho. Moja ya jambo ambalo tulikubaliana ndani ya Serikali na Mheshimiwa Rais akiwa ameelekeza katika dira yake na *vision* yake ya masuala ya uwekezaji, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, ni kuwa na viwanda kanda mbalimbali ili kuepukana na utaratibu huu ambao punde panapotokea moja ya *factor* ya gharama za usafirishaji kupanda, basi na bidhaa hiyo inapanda.

Mheshimiwa Spika, hiki alichokisema Mheshimiwa Mbunge cha hivi karibuni ni kutokana na kupanda kwa bei za mafuta za hivi karibuni. Tulikaa ndani ya Serikali, tukakaa na wadau wa usafirishaji kama nilivyojibu katika moja ya swali, tukatafuta

namna ya kuepusha kupanda kwa gharama za usafirishaji. Nilizisema juzi sababu hizo na bado pia ninapanga kukutana na wale wasafirishaji wa mizigo.

Mheshimiwa Spika, nilishakutana na wasafirishaji wa abiria, na ninapanga kukutana na wasafirishaji wa mizigo kuangalia namna ya kushughulikia baadhi ya maeneo tunayoweza kurekebishwa ili kupunguza gharama za usafirishaji. Kwa hiyo, hicho ndicho ambacho kilisababisha katika siku za karibuni kupanda kwa mafuta, kukasababisha kupanda kwa gharama za usafirishaji ikiwemo suala la *cement*.

Mheshimiwa Spika, habari njema ni kwamba Mheshimiwa Rais tayari alishaelekeza watu wanaotaka kuwekeza kwenye bidhaa hizi wapewe kipaumbele. Kwa taarifa nilizonazo, hivi tunavyoongea, kule Kigoma kuna kiwanda kimojawapo ambacho kiko katika hatua za utekelezaji ili kuweza kuwa na viwanda vingine vinavyozalisha bidhaa hii upande wa magharibi mwa nchi yetu ikiwemo Kigoma, Kagera na Katavi. Hii itaepusha kutoa bidhaa hiyo kuanzia Mtwara ama kuanzia Tanga ambako ni upande mwingine wa nchi yetu kupeleka upande mwingine wa nchi yetu jambo ambalo linasababisha bidhaa hiyo kupanda gharama kutokana na hizo gharama za usafirishaji na gharama za usambazaji.

Mheshimiwa Spika, tutakaa na wasambazaji ili tuweze kujua namna ambavyo tunaweza tukazuia bei kupanda kiwango cha kuwafanya wananchi washindwe kumudu kuhimili gharama hizo na kupunguza kasi ya kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali.

(Hapa Mhe. Nassriya Nassir Ali alizungumza kupitia Mtaalamu wa Lugha ya Alama)

MHE. NASSRIYA NASSIR ALI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa Serikali inayo Sera ya Bima ya Afya kwa Wote; wanawake, vijana, watoto na watu wenye ulemavu, je, Serikali

ina mkakati gani wa kuhakikisha upatikanaji wa haraka wa bima hiyo? Mungu Ibariki Tanzania. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Nassriya Nassir kwa kuwakilisha vyema. Mheshimiwa Mbunge anafuatilia mambo ya nchi, anafuatilia mambo ya kisera na anaishauri Serikali mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili jambo la Bima ya Afya kwa Wote ni kweli Serikali imeanza utekelezaji wake mwezi Januari mwaka 2026 kama ilivyokuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaweka *seed money,* (fedha ya awali) kwa zaidi ya shilingi bilioni 48 kwenda shilingi bilioni 50 ambayo inalenga kuhakikisha kwamba makundi yale ya awali yanapata huduma hiyo, yanapata Bima hizo ili kuweza kuokoa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, hatua inayoendelea ambayo tayari katika Bunge lako Tukufu tumeshuhudia ni Serikali kuendelea kutafuta vyanzo vya mapato ili kuwezesha kuongeza wigo wa wale wanufaika ambao wanatakiwa kunufaika na Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Spika, jambo moja tu ambalo ninaomba niliweke wazi mbele ya Bunge lako Tukufu ni kwamba Bima ya Afya ni tofauti na *TASAF,* na wala tusichanganye Bima ya Afya na *TASAF,* kwamba ni Mfuko wa Kusaidia Watu Wasiojiweza, la hasha. Bima ya Afya, hii ni programu ambayo inatakiwa ihusishe wananchi wote ili kuweza kusaidiana katika namna ya kupata matibabu kwa kutumia Bima ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kadri Watanzania wote watakapohamasika kujiunga na Bima ya Afya, ndivyo tutakavyofanya hii programu iweze kutekelezeka. Tukiibadilisha

Bima ya Afya ikawa ni *TASAF* kwamba tunasubiri tu Serikali ipeleke fedha ili itibu Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kwa namna hii tutakuwa tunajiandaa kufanya programu hii isitekelezeke vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe Watanzania na Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kuhamasisha Watanzania wote kushiriki kwenye zoezi la Bima ya Afya kwa sababu pale watakaposhiriki Watanzania wote kwenye Bima ya Afya, wakajiunga na Bima ya Afya huku Serikali ikitafuta vyanzo kwa ajili ya kusaidia zile familia ambazo haziwezi kukata Bima ya Afya, ndipo tutakapofanya jambo hili la Bima ya Afya liweze kutekelezeka kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika nchi zilizowahi kujaribisha kutaka kufanya jambo hilo litekelezwe na Serikali peke yake, programu hizo hazikufanikiwa. Kwa hiyo, jambo hili linahitaji litofautishwe na *TASAF* ambayo ni programu ya kusaidia zile jamii tu zisizojiweza. Bima ya Afya, ni kwa Wote. Maana yake kila Mtanzania ashiriki kukata Bima ya Afya na kupitia programu hiyo ndipo tutakapoweza kuwa na Bima ambayo ni jumuishi ambayo haitaacha mtu nyuma wakiwemo wale makundi ambao hawajiwezi. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, juzi Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo, kulalamika, na kukemea uchafu kwenye Jiji la Dar es Salaam. Wakati mwingine Halmashauri za Dar es Salaam na Miji mingine mikubwa nchini wanapokuwa na miradi ya *PPP,* wanapoleta miradi hii kushughulikiwa na watu wa TAMISEMI, majibu aidha yanachelewa au hayaji majibu ya kuwatia moyo kuendelea na hizi *PPP*. Matokeo yake mji unaendelea kuwa mchafu.

Hata hivyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, nikushukuru na wewe na ninamshukuru Waziri wa TAMISEMI kwa namna mlivyolivalia njuga suala la uchafu Dar es Salaam na kulitolea uvumbuzi kuwa *PPP* sasa zitumike na halmashauri mradi

zifuate sheria, taratibu, kanuni za nchi ili mji uwe salama na miradi ya Kiserikali na *Private Sector* iwe salama.

Niwaombe wataalamu wa TAMISEMI, tabia ya kutokuwa na mwamko wa kubadilisha mawazo ya *PPP* waache. Katika ushauri uliotolewa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, katoa mtu ushauri kwamba tuwe na chombo cha umma. Halmashauri peke yake ni chombo cha umma. Tuanzishe chombo cha umma kwa mkopo kizoe taka wakati kuna mtu anakuja na hela zake na uwekezaji wake anaambiwa asubiri! Kwa hiyo, nikushukuru kwa hatua ulizochukua wewe na Makamu wa Rais na Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pia watu wetu wa TAMISEMI wabadilishe fikra zao, tunakwenda kwenye vision 2050. *Vision* 2050 Bunge hili ndiyo limeridhia uwekezaji wa vision hii, 70% zitatoka *Private Sector.* Niwaombe sana watendaji wa Serikali, badilikeni. Kama hambadiliki, mtabadilishwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakushukuru. *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, Maswali ya Kawaida.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali ya kawaida. Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe.

Na. 94

Kubadilisha Jina la Jimbo la Tarime Vijijini Kuwa Jimbo la Nyamwaga

MHE. MWITA M. WAITARA aliuliza: -

Je, lini Jimbo la Tarime Vijijini litabadilishwa na kuitwa Jimbo la Nyamwaga?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Masharti ya Kanuni ya 18 ya Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2024 yameainisha kuwa, Tume itatoa tangazo kwa umma kuwataarifu kuhusu kuwasilisha maombi ya kugawa au kubadili jina la Jimbo la Uchaguzi. Tangazo hilo hutolewa inapofika mwaka wa uchaguzi, hususan kipindi baada ya Uboreshaiji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge, mara Tume itakapotoa tangazo hilo na kuanza mchakato wa kugawanya au kubadili majina ya Majimbo, ndipo awasilishe ombi hilo kupitia Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara ili maombi hayo yaweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

SPIKA: Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini katika hiyo Wilaya ya Tarime, lakini Makao Makuu ya Jimbo ni Nyamwaga. Kwa hiyo, wananchi wa Tarime Vijijini wangetamani Jimbo lao liitwe Jimbo la Nyamwaga; Makao Makuu ya Nyamwaga; na hili suala haliongezi gharama yoyote ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Ningependa kujua, kama Serikali na Tume wanaweza wakaridhia maombi hayo pindi tutakapopeleka maombi kufuata hatua mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mwaka 2024 wananchi wa Sirari waliomba kupewa Mamlaka ya Mji Mdogo na wananchi wa Nyamongo waliomba Mamlaka ya Mji Mdogo, kugawa kata na vitongoji vikubwa, kwani kata moja inakuwa na vitongoji mpaka 20.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa, tuliambiwa kwamba Serikali wakati huo uchumi ulikuwa ni mdogo, na sasa uchumi unakua mwaka hadi mwaka, ni lini majibu ya matumaini kwa mwananchi wa Sirari, Nyamongo na baadhi ya vitongoji ambavyo wangetamani viwe vijiji ili waendelee kupata huduma za kijamii?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA): Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Mheshimiwa Mwita Waitara kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya. Kwenye swali lake la kwanza anataka kupata uhakika wa kwamba jina litabadilishwa. Nimwambie kwamba, wananchi wa Tarime Vijijini wakifuata utaratibu huo ambao nimeueleza ambao ndiyo unaozingatiwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, basi watapata jina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tume inao uzoefu na imefanya hivyo kwenye maeneo tofauti, kwa mfano kwenye Jimbo la Mheshimiwa Florent lilikuwa linaitwa Jimbo la Mkenge likabadilishwa kuitwa Jimbo la Missenyi; Mpanda Vijijini ilibadilishwa na kuitwa Tanganyika; Singida Kaskazini imeitwa Ilongero; Handeni Vijijini ikaitwa Handeni, na maeneo mengine, kwa hiyo, ninamhakikishia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili anataka wagawanye maeneo. Ninaomba nimrudishe Mheshimiwa Mbunge kwenye sura za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na 288.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Mwongozo ambao umetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Profesa Shemdoe wa mwaka 2025 ambao unawapa utaratibu mzuri wa jinsi ya kuanzisha hizi Mamlaka za Serikali za Mitaa, basi wafuate utaratibu. Wafanye vile vikao, wakimaliza kupitia kwa Katibu Tawala Mkoa wa Mara, wawasilishe maombi hayo kwa Katibu Mkuu, TAMISEMI ili maombi hayo ya wananchi yaweze kufanyiwa kazi. Ninakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, kiukweli haya majina ya Majimbo, mfano Jimbo la Bunda linaitwa hivyo lakini ukienda pale kwa wananchi, wanaliita Jimbo la Bunda Vijijini; lina utata. Kuna majimbo mengine yanayoitwa vijijini, ni mjini. Ninakushukuru sana kwa utaratibu ulioutoa kwamba na sisi tunataka Jimbo la Bunda liitwe Jimbo la Chamuriho, siyo Jimbo la Bunda ili kuondoa utata uliopo kati ya Bunda na Bunda Mjini.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA): Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, ninaomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge asubiri mwaka wa uchaguzi utakapofika, Tume itakapotangaza, wafuate huo utaratibu, basi jina litaweza kubadilika kama ambavyo wananchi wanatamani kwa kupitia yeye Mwakilishi wao. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ngonyani.

Na. 95

Ujenzi wa Barabara ya Namanditi - Mwanamonga

MHE. JACQUELINE K. N. MSONGOZI aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Namanditi hadi Mwanamonga katika Manispaa ya Songea utaanza?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Namanditi - Mwanamonga - Parangu katika Halmashuri ya Manispaa ya Songea ina urefu wa kilometa tisa. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 barabara hii imetengewa bajeti ya shilingi milioni 120 kwa ajili matengenezo ya kuweka changarawe, ujenzi wa mifereji ya maji pamoja na vivuko. Aidha, kwa sasa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* Mkoa wa Ruvuma ipo katika hatua za manunuzi ili kumpata mkandarasi ili utekelezaji wa matengenezo ya barabara hii uweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo, ili kuhakikisha inapitika kipindi chote cha mwaka kikamilifu. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Ngonyani.

MHE. JACQUELINE K. N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ambayo inatoka Namanditi kwenda Mwanamonga na hatimaye Parangu, ni muhimu sana kwa kuchagiza maendeleo ya maeneo haya. Kimsingi Eneo la *EPZ* ambalo limetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda, tayari viwanda vimeshaanza kujengwa, lakini malighafi zote na bidhaa

zote ambazo zinasaidia ujenzi huu zinapita katika barabara hii ambayo ni mbovu. Je, lini Serikali itaanza kwa dharura ujenzi wa barabara hii ili kuwezesha ujenzi huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Barabara hii ni muhimu sana kwa wanawake ambao wanajishughulisha na shughuli za ujasiriamali hususan wauza mboga mboga ambao wanafanya shughuli hizi katika maeneo haya, lakini wamekuwa wakipata changamoto ya kutokufika kwenye maeneo ya masoko kwa wakati. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwezesha barabara hii, ili wadau hawa waweze kufika kwenye maeneo haya kwa wakati? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kwa namna ambavyo anafuatilia utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii ya Namanditi – Mwanamonga – Parangu katika Manispaa ya Songea.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa sababu inakwenda kwenye eneo maalum la uwekezaji, *EPZA*, lakini tunafahamu pia ni barabara muhimu sana kwa shughuli za kiuchumi. Ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha tayari tumeitengea shilingi milioni 120, na hivi sasa *TARURA* Mkoa wa Ruvuma wako hatua za mwisho za kutangaza zabuni hii ili kumpata mkandarasi, ili mapema iwezekanavyo ndani ya mwaka huu wa fedha, barabara hii iweze kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kumsisitiza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Ruvuma kuharakisha taratibu za manunuzi ya barabara hii ili mkandarasi aende *site* kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la pili, tunafahamu pamoja na shughuli nyingine, barabara hii ni muhimu kwa wajasiriamali akina mama na wananchi wote kwa ujumla kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, ndiyo maana tutahakikisha inajengwa mapema iwezekanavyo ili iweze kupitika vizuri.

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Songea katika kipindi hiki imejengewa barabara za lami zaidi ya kilometa 10 kupitia Mradi wa *TACTIC* awamu ya kwanza, na hivi sasa tunaendelea kujenga barabara ya lami kilometa 2.6. Yote hii ni jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba, Manispaa inakuwa na barabara bora na wananchi wanakuwa na huduma bora zaidi za kiuchumi.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi, niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika Wilaya yetu ya Kilolo, kuna maeneo ambayo hayapitiki kabisa wakati wa mvua, na sasa hivi mvua zimekaribia; na Serikali ilikuwa imetuahidi kwamba itatuletea fedha ili matengenezo yaweze kufanyika kabla mvua hazijaanza, na *El-Nino* ndio imeshatangazwa, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuja kwanza Kilolo kujionea na kutupatia hizo fedha ili matengenezo yaanze kufanyika? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Jimbo la Kilolo kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara kuhusiana na uboreshaji wa barabara katika Jimbo la Kilolo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote, kama ambavyo Serikali tumesema mara kwa mara katika Bunge hili, kwamba tunatambua ziko barabara nyingi zilizoathirika na mvua katika kipindi cha msimu wa mvua uliopita.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai mpaka tarehe 30 Agosti, mwaka huu wa fedha tayari Serikali imeshapeleka katika halmashauri zetu fedha jumla ya shilingi 69,870,000,000 katika halmashauri 162.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili ni endelevu. Hivi sasa kazi za utengenezaji, marekebisho na ujenzi wa barabara zinaendelea katika halmashauri zetu kote nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Serikali itaendelea kupeleka fedha. Pia niko tayari kuambatana naye, tutapanga tuone ratiba na namna nzuri ya kufika kukagua barabara hizo, lakini muhimu kuhakikisha fedha zinaendelea kwenda na ujenzi wa barabara hizo unaendelea kufanyika.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Tabasam Mwagao. Mheshimiwa Tabasam umo ndani?

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, nimo ndani.

Na. 96

Ujenzi wa Nyumba za Watumishi Hospitali ya Wilaya – Mwabaruhi

MHE. TABASAM H. MWAGAO aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Nyumba za Watumishi katika Hospitali ya Wilaya ya Mwabaruhi ambayo hadi sasa haina hata nyumba moja ya Watumishi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa

Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Jimbo la Sengerema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na nyumba za watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Kutokana na ongezeko la ujenzi wa hospitali mpya za halmashauri umepelekea mahitaji makubwa ya nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya mahitaji ya nyumba za watumishi ambapo jumla ya nyumba 25,690 zinahitajika kote nchini, wakati nyumba za watumishi zilizopo ni takribani 7,696 sawa na 30%. Aidha, katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, takwimu zinaonyesha mahitaji ya nyumba 125 na zilizopo ni nyumba 70 sawa na 56%.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, imewasilisha andiko Wizara ya Fedha kuomba jumla ya shilingi bilioni 13.8 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi 2,000 kwenye maeneo yenye uhitaji zaidi nchini, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema. Ninaomba kuwasilisha.

(Hapa kipaza sauti cha kilikuwa na changamoto)

SPIKA: Mheshimiwa Tabasam. Waheshimiwa, ninaomba mngezima *mic* zenu, mwacheni mwenye swali aulize.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Sengerema tayari tumeshajenga zahanati ambazo ni mpya pamoja na vituo vya afya, lini Serikali italeta madawa pamoja na vifaa tiba na watumishi katika hospitali na zahanati hizo pamoja na vituo vya afya vipya vilivyojengwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, katika Jimbo la Sengerema tumejenga zaidi ya zahanati 17 kwa nguvu za wananchi pamoja na Mfuko wa Jimbo. Lini zahanati hizo zitapata fedha ili wananchi sasa waondokane na matatizo ya kufuata tiba

mbali, hasa vikiwemo visiwa vya Nyakanyanse ambavyo vipo umbali mrefu kuja katika maeneo ya tiba? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Tabasam kwa kuendelea kufuatilia changamoto katika Jimbo lake la Sengerema.

Mheshimiwa Spika, katika Kanda ya Ziwa, Mheshimiwa Tabasam ni miongoni mwa Wabunge wakongwe ambao wana tija katika nchi yetu na wana mchango mkubwa sana katika maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Tabasam, katika zile zahanati ambazo zimekamilika, nimwelekeze *DMO* wetu pia na Mkurugenzi kuanza kutenga rasilimali tulizonazo ndani ya halmashauri kuona kwamba tunaanza kutoa matibabu yale ya muhimu katika zahanati hizi.

Mheshimiwa Spika, ni maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba zile zahanati ambazo tayari zimekamilika, zianze kutoa huduma kwa mama zetu kupima ujauzito, kupima watoto wetu na kupunguza umbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwenye swali la pili, mimi na yeye tutaongozana kwenda kwenye Jimbo lake la Sengerema ili na watumishi wote wa halmashauri, tukatoe majibu kwa wananchi na kuanza kutoa huduma hizi muhimu kwa wananchi wetu. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Alan.

MHE. ALAN T. MVANO: Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kakonko, bado yapo maeneo mengi ya vituo vyetu vya huduma za afya ambayo yana changamoto ya nyumba za watumishi

ikiwa ni pamoja na Kituo cha Afya cha Gunzu pamoja na maeneo mengine. Je, ni lini Serikali itaweka fedha kwa ajili ya kuongeza nyumba za watumishi katika Wilaya ya Kakonko? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Spika ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Alan, Mbunge wa Jimbo la Kakonko kwa namna anavyofuatilia na kusisitiza maendeleo katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tumeshaandika andiko maalum la kuhakikisha kwamba ujenzi wa zile nyumba 2,000 ambazo zinahitaji zaidi ya shilingi bilioni 13.8. Tutafanya namna ya ku-*mobilize resources,* tuko hatua ya kutafuta fedha kuhakikisha kwamba tunaanza kujenga nyumba hizi. Tumeelekeza hasa katika zile halmashauri za pembezoni ambazo zina upungufu na zina uhitaji mkubwa wa nyumba. Hii ni *retention mechanism* ya kufanya watumishi wetu waendelee kutoa huduma bila kuwa na *pressure* katika maeneo yale ya pembezoni mwa nchi. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa.

Na. 97

Kujenga na Kumilikisha Maeneo kwa Ajili ya Wafugaji

MHE. FAGASON A. NKINGWA aliuliza:-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kutenga na kumilikisha maeneo kwa ajili ya wafugaji nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kutenga, kupima na kumilikisha maeneo ya wafugaji yenye ukubwa wa hekta milioni sita kwa wafugaji ifikapo mwaka 2030. Katika kufanikisha hili, hadi kufikia mwaka 2025/2026, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliandaa mipango ya matumizi ya ardhi iliyowezesha kutenga zaidi ya hekta milioni 3.6 kwa ajili ya shughuli za ufugaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2025/2026, zaidi ya hekta milioni 1.3 zilizopo katika vijiji 365, zimepimwa na kutangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali, *GN* Na. 597 na *GN* Na. 718. Sambamba na hatua hiyo, mipango ya matumizi ya ardhi imejumuisha maeneo 53 yenye jumla ya hekta 790,865.54 ambapo wananchi wamekabidhiwa Hati za Hakimiliki za Kimila, ili kujumuisha umiliki na kusimamia rasilimali hizo kwa ufanisi na kuongeza upatikanaji wa maeneo ya malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga, kupima na kumilikisha maeneo ya malisho kwa ajili ya matumizi ya mifugo kwa kuzingatia mahitaji ya kila eneo nchini. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Fagason.

MHE. FAGASON A. NKINGWA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya upimaji wa ardhi pamoja na maeneo, je, ni lini Serikali sasa itakuja kupima kwenye Jimbo la Mbogwe? Swali langu la kwanza hilo.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, liko pori ambalo lina changamoto kubwa sana kwenye jimbo langu la Mbogwe. Hili ni pori la Kigosi. Pori hili limekuwa na changamoto kubwa kati ya wafugaji, wakulima, pamoja na wachimbaji. Je, Serikali ina mpango gani kuja kuhakikisha inalipima pori hili, ili wananchi wa Jimbo la Mbogwe waweze kufaidika? Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ninaendelea kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa kwa umahiri wake wa kufuatilia taarifa za maendelezo ya ardhi na kuungana na Serikali katika kuzuia migogoro ambayo inaweza kujitokeza katika maeneo ambayo hayajapimwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bunge hili imeweza kuidhinisha fedha ambazo Wizara ya Ardhi tumepokea zaidi ya shilingi bilioni 38 kwa ajili ya kupima vijiji vyote vilivyobakia visivyopungua 1,500 katika mwaka huu wa 2026.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutashirikiana naye kwa ajili ya kubainisha vijiji vyote ambavyo havijapimwa katika halmashauri yake na jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, nikimjibu swali lake la pili, pori ambalo amelizungumza ninakiri kuwa pori hilo lina mwingiliano wa matumizi kati ya wahifadhi pamoja na wanaofuga kama alivyoeleza vizuri sana hapa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipokuwa anajibu swali alipoulizwa na Wabunge kuhusu utatuzi wa migogoro. Alitoa rai ya watu tunaotumia au makundi yanayotumia ardhi kuepuka mwingiliano wa matumizi ya ardhi katika maeneo ambayo yamepimwa.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu katika pori hili, kwa sababu kuna shughuli za uchimbaji mle ndani, sidhani kama kuna changamoto kati ya wanaotunza pori hili pamoja na wachimbaji. Hofu yangu ni wafugaji ambao shughuli za kifugaji haziruhusiwi

katika pori hili. Ninaomba tu nitoe rai kuwa kusiwe na mwingiliano katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama kuna mkanganyiko wa kufufua mipaka, sisi Wizara ya Ardhi tuko tayari kuambatana na Mbunge tuone jinsi ya kufufua mipaka hiyo ili tuweze kujua mipaka hii ni ya pori, na mipaka hii ni ya maeneo mengine ya matumizi ya mifugo na shughuli nyingine. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa changamoto ya migogoro ya ardhi imekuwa ni nyingi sana na wananchi wanaongezeka na mipaka iko vile vile, je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kupunguza maeneo ya hifadhi kuwagawia wakulima na wafugaji ili kupunguza migogoro hii? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa swali zuri na nia njema ya kutaka kupunguza migogoro hii, na kimsingi kuzuia.

Mheshimiwa Spika, huku tukifahamu, idadi ya watu inazidi kuongezeka na ardhi yetu bado ipo vilevile, haiongezeki, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametueleza, ni sisi kuwa na mipango mizuri ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Bunge hili limepitisha fedha kwa ajili ya kupanga matumizi bora ya ardhi. Tunachotakiwa sisi wafugaji na wakulima, tuwe na mipango mizuri ya kujua na kufuga kisasa na kulima kisasa. Hakutakuwa na migogoro.

Mheshimiwa Spika, pia hakutakuwa na ardhi ya kutosha kwa sababu ardhi imebaki vilevile na idadi ya watu inaongezeka. Hivi niwasihi wafugaji, tufuge kisasa kwa kuwa na malisho ya kimkakati

ya kulima wenyewe na tusiende kuvuruga mipango ya matumizi mengine ya hifadhi ya ardhi yetu. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la Katibu wa Bunge, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa Maafisa Uhamiaji wamewasilisha hati za kusafiria za Wabunge, ziko tayari.

Hivyo, Waheshimiwa Wabunge ambao hawajachukua hati zao za kusafiria wanaombwa kufika jengo la utawala, ghorofa ya nne, chumba namba tisa, muda huu.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi.

Na. 98

Ukarabati wa Vituo vya Polisi Malindi na Makadara

MHE. MUHSIN HAJI USSI aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati au kujenga upya Vituo vya Polisi vya Malindi na Makadara?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi, Mbunge wa Malindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi cha Malindi kinabeba historia kubwa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jeshi la Polisi linatarajia kutekeleza ukarabati wa Vituo vya Polisi vya Malindi na Makadara, vyote vilivyopo katika Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi kupitia fedha za matumizi mengineyo, katika mwaka wa fedha 2026/2027. Aidha, Serikali kupitia Jeshi la Polisi linafanya

mawasiliano na Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Polisi Malindi. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Ussi.

MHE. MUHSIN HAJI USSI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kituo cha Polisi cha Malindi kinapatikana katikati ya Mji wa Zanzibar, ambao ni mji wa kihistoria na kitalii, kinahudumia wananchi pamoja na watalii wanaotembelea Zanzibar, je, Serikali ipo tayari kukifanya kituo hicho cha Malindi kuwa cha kisasa, na vilevile kuongeza watumishi pamoja na vitendea kazi ili kiweze kutoa huduma za kiusalama kwa ufanisi, zenye kuendana na hadhi ya Zanzibar katika sekta ya utalii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili dogo la nyongeza. Kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi hutumia barabara iliyopo mbele ya kituo cha Malindi kwenda jimboni kwake, je, ni lini atakuwa tayari kuambatana na mimi kukagua miundombinu ya Kituo hicho cha Polisi cha Malindi Zanzibar? Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Ussi kwa maswali yake mawili ya nyongeza ambayo ni muhimu sana kwa mustakabali wa uhuishaji wa huduma ya usalama katika eneo la Mji Mkongwe.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, Kituo cha Polisi cha Malindi kwanza kina vitendea kazi vya kisasa zikiwemo redio, pia kuna *CCTV* na vinginevyo. Vilevile, kwa hadhi na ukubwa wa kituo kile, kina watendaji au watumishi ambao wanakidhi mahitaji ya eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuimarisha usasa pamoja na kuimarisha ulinzi katika eneo hilo, na kwa mazingatio mawili aliyoyaeleza ya kihistoria ya mji wenyewe, pia na lile la utalii katika eneo hilo, ninataka nimwambie tu Mheshimiwa

Mbunge kwamba, bahati nzuri eneo la Mji Mkongwe ni moja kati ya maeneo ambayo Serikali kwa kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejenga na kuweka mfumo madhubuti wa uangalizi wa kamera za kisasa, kwa maana ya *CCTV*.

Mheshimiwa Spika, mji ule umewekwa kamera katika kila eneo na kumewekwa kituo maalumu kwa maana *ya Command and Control Center*, ambayo inaweza kupokea taarifa za matukio yote katika eneo hilo. Hivyo, kwa upande wa usasa, Serikali imejitahidi kuhakikisha kwamba eneo hilo linalindwa kisasa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, eneo la Mji Mkongwe ni moja kati ya eneo ambalo lina ulinzi shirikishi unaofanya kazi vizuri kwa ushirikiano wa karibu sana na Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, ninamwahidi tu kuwa, tutaendelea kushirikiana na vijana wa ulinzi shirikishi wa Malindi ili kuhakikisha kwamba tunazidi kuimarisha eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inao utaratibu wa kuimarisha ulinzi hasa maeneo ya kitalii, ikiwemo Mji Mkongwe, katika maeneo mbalimbali ya fukwe. Kwa hiyo, hata Mji Mkongwe wapo Askari maalumu ambao wanaitwa Polisi Utalii, ambao wanashughulikia usalama wa utalii muda wote. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, kwa swali la kwanza la eneo la Mji Mkongwe, liko vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa swali la pili, ninamwahidi tu kuwa tuko tayari kuendelea kuambatana, ingawa kwa Kituo cha Polisi cha Makadara yapo mazungumzo na majirani zao pale ofisi za CCM za wilaya, ili kuona namna gani kitawekwa vizuri ikiwezekana kujengwa upya ili na ofisi ya wilaya ijengwe upya, hatimaye kuweza kuwa na kituo cha kisasa zaidi. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Kata ya Nyandoto, Kenyamanyori na Nkende ni kata

ambazo zina uhitaji mkubwa wa vituo vya Polisi na nilishauliza hapa Serikali ikaahidi kwamba itafuatilia kuona kama zina hati, sasa tayari hizi kata zina hati na zinasubiria tu kupelekewa fedha ili ziweze kujengwa vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua sasa, ni lini fedha zitaenda ili kata hizi za Nyandoto, Kenyamanyori na Nkende waweze kujengewa vituo vya Polisi? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Esther Matiko kwa swali lake la msingi na la muhimu. Kweli kama alivyoeleza aliwahi kuniuliza na tulimwahidi kuwa tutafanya hivyo, yaani tutajenga vituo hivyo. Lini fedha zitafika? Ninamwomba tu kwamba ndiyo tumeanza mwaka wa fedha wa 2026/2027, tuko mwezi wa Pili au wa Tatu tunaanza *quarter* ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, tunapoanza mwaka wa fedha au *quarter* ya kwanza ya mwaka wa fedha, utoaji wa fedha hasa zile za maendeleo unachukua muda kidogo. Kwa hiyo, mara tutakapopata fedha hizo za maendeleo, basi na eneo hilo tutafikisha fedha ili kusudi ujenzi wa vituo uweze kuendelea. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Said Ibrahim Mzimba.

Na. 99

Ujenzi wa Makazi ya Askari Polisi Jimbo la Mtambile

MHE. SAID IBRAHIM MZIMBA aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Makazi ya Askari Polisi katika Jimbo la Mtambile Wilaya ya Mkoani?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Ibrahim Mzimba, Mbunge wa Mtambile kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa makazi bora ya Askari Polisi, ikiwa ni chachu ya kuboresha utendaji kazi wa kila siku wa ulinzi wa raia na mali zao. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ulifanyika ukarabati mkubwa wa kituo cha Polisi na makazi ya Askari ambayo yapo ghorofa ya juu ya kituo cha Polisi katika Jimbo la Mtambile lililoko Wilaya ya Mkoani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutokuwepo kwa eneo la ujenzi wa jengo jipya la makazi katika eneo hilo, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeingiza kwenye mpango wa ukarabati jengo la ghorofa ya makazi lililopo kituoni hapo kwa mwaka wa fedha 2027/2028. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Mzimba.

MHE. SAID IBRAHIM MZIMBA: Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa makazi duni yanazorotesha utendaji kazi wa ndugu zetu Polisi, je, katika Kituo cha Polisi cha Kengeja, ni lini yatapatikana makazi ya Polisi? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Said Ibrahim Mzimba kwa kazi kubwa anayoifanya. Mwaka wa fedha uliopita wa 2025/2026 alituuliza kuhusu kituo ambacho tumekikarabati sasa cha Mtambile na kimeshafanyiwa kazi pamoja na makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu ninaona amekuja na hii ya Kengeja. Serikali inaendelea na utekelezaji wa mpango wa miaka mitano wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya makazi pamoja na vituo vya Polisi nchi nzima. Aidha, Serikali imepanga katika kila

mkoa walau kuwa na majengo makubwa mawili ya ghorofa ikiwa ni sehemu ya kuimarisha makazi ya Askari.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ninataka Mheshimiwa Mbunge na Askari wa eneo lake wote na Watanzania kwa ujumla wajue, Serikali inafanya kila liwezekanalo kuimarisha makazi na maeneo yao ya kazi ili kusudi waweze kufanya kazi kama wanavyofanya wengine katika ofisi zao katika mazingira mazuri zaidi. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Regina.

MHE. DKT. REGINA C. MALIMA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kisiwa cha Ukerewe kina visiwa 38 na Serikali mwaka 1922 iliahidi kujenga kituo au kukarabati Kituo cha Nansio, lakini hadi leo hakijakarabatiwa. Niseme tu ya kwamba, kuna umuhimu wa kufanya hivyo kwa sababu kituo cha Nansio ndicho kinachotegemewa katika visiwa vyote 38. Je, Serikali haioni kwamba ni muda mwafaka wa kufanya hivyo? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Regina kwa kuja kwanza na historia na kumbukumbu za kituo cha Polisi kinachotegemewa katika eneo la Ukerewe kwamba tokea mwaka 1922 ndiyo kimejengwa na kinahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Spika, ninachukua hoja ya Mheshimiwa Dkt. Regina kwa sababu tulivyokuwa tunawasilisha bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 tuliweka randama ambayo inaonyesha kila mkoa ujenzi na ukarabati utakaofanyika kwa makazi na vituo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitakwenda kuhakiki kujiridhisha; ikiwa na kituo hiki kipo kwenye randama hiyo, basi tunamhakishia ndani ya mwaka wa fedha huu tutakikarabati. Endapo hakipo hapo, ninamhakikishia tu kwamba, tutazungumza na wenzetu wa Jeshi la Polisi tuone namna gani ya kuweza

kushughulika na jambo hili ambalo ni la muda mrefu sana. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Abubakar Omari.

Na. 100

Ujenzi wa Kituo cha Kupoozea Umeme cha Ziba

MHE. ABUBAKAR A. OMARI aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ziba kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu 2025?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakar Alli Omari, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* imeendelea na uboreshaji wa miundombinu ya umeme katika Wilaya ya Igunga, kwa kutekeleza mradi wa kimkakati uliohusisha ujenzi wa njia ya kusambaza umeme wa Kilovoti 33, yenye urefu wa kilometa 41, kutoka Kituo cha Kupoza Umeme cha Lusu, pamoja na ujenzi wa Kituo cha Kudhibiti Mifumo ya Umeme *(Switching Stations)* katika eneo la Ziba, ambacho kimekamilika na kimesaidia kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa umeme katika maeneo mbalimbali katika Wilaya ya Igunga.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha zaidi hali ya upatikanaji wa umeme katika Wilaya ya Igunga, Serikali kupitia *TANESCO* inatarajia kuanza kufanya upembuzi yakinifu wa awali *(Pre-Feasibility Study)* kwa ajili ya maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Igunga. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Abubakar.

MHE. ABUBAKAR A. OMARI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Awali ya yote, kwa idhini yako, ninaomba tu niwapongeze *TANESCO* kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wilaya ya Igunga, hasa Meneja wao, Ndg. Raphael Ambokisye. Hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa hivi wananchi katika visima vya maji vya Mwamloli, Mwamakingi, Isenegeja, Mwamala, Simbo, Tambalale, Nsheli, Igondela, Igumo, Mwansuho pamoja na Chibiso wana shida sana ya umeme ukizingatia sasa hivi ni kiangazi, je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye visima vya maji vya ambavyo tumeshaomba toka mwaka Septemba, 2025; na barua ya *RUWASA* ilikwenda tarehe 1 Septemba 2025?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kuna kata ambazo zimepata umeme, lakini pembezoni mwa hizo kata umeme haujafika, kwani kuna maeneo waliacha. Maeneo ya kata zenyewe ni Ndembezi (pembezoni mwa Ndembezi) Nkinga (Njia Panda maarufu kwa Mzee Masaba), Mwisi, Itobo na Busomeke B. Je, lini Kata hizi zitafikishiwa umeme? Ninaomba majibu.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninampongeza Mheshimiwa Abubakar kwa kufuatilia na kuhakikisha kwamba jimbo lake linapata umeme na wananchi wake wananufaika na uwepo wa nishati ambayo tunaizalisha kwa wingi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza, Serikali imeshaeleza kupitia Wizara ya Nishati kwamba, taasisi zote za Umma na miradi yote ya Serikali inatakiwa kupewa kipaumbele na kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, kwenye visima vyake tisa tumeshafanya utafiti na taasisi hizo tumeshazipeleka kwa *REA* ambao ndiyo wanahusika katika kupeleka umeme.

Mheshimiwa Spika, ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge, sasa hivi tunafanya gharama za ununuzi wa vifaa ili tuweze kupeleka umeme katika visima hivyo kwa kadri ambavyo tutapata fedha. Nikumhakikishie kwamba, miradi yote, siyo tu visima, lakini shule, ukijumlisha ofisi za Serikali, lazima zipatiwe umeme kwa sababu lazima tufungamanishe miradi ya Serikali ili kupata tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba Serikali yetu kupitia ilani zetu mbalimbali tumekuwa na vipaumbele. Kwanza kuhakikisha kata zote zinapata umeme; pili, kuhakikisha vijiji vyote vinapata umeme na sasa tumekamilisha; na tatu, kuhakikisha vitongoji vyote vinapata umeme. Sasa tuko karibia 64%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kumaliza kupeleka umeme katika vitongoji vyote, tutaendelea na miradi ya ujazilizi. Lengo la Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kila kaya inapata umeme, kwa sababu umeme siyo changamoto katika nchi yetu. Kwa hiyo na maeneo yake tutapeleka miradi ya ujazilizi na yote yatapata umeme. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Sara Ally.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kwanza ninapenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Umeme la *Stieglers* ambalo alilikuta kwa mtangulizi wake likiwa na 30%, lakini Mheshimiwa Rais amekamilisha ujenzi wa bwawa hili. Tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Mvomero eneo la kimkakati la viwanda ni Tarafa ya Turiani na Dakawa, na tuna viwanda vingi, lakini tuna changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya umeme, na kwa kuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba tutajenga kituo cha kupooza umeme cha kilovoti 220 eneo la Dumila na eneo tayari lipo, je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kituo hicho cha kupoza umeme ili viwanda vya

eneo la Jimbo la Mvomero na maeneo ya karibu waweze kunufaika na mpango huu? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Sara Msafiri kwa kufuatilia kwa karibu kuhusiana na suala la upatikanaji wa umeme wa uhakika usiokatikakatika kwa ajili ya kuhudumia viwanda vilivyoko katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninamshukuru Mheshimiwa Sara kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hakika Mheshimiwa Rais alikuta Bwawa letu la Mwalimu Nyerere liko katika asilimia ndogo sana, 30%, lakini amejitahidi, tumeweza kujenga na kumaliza, tumejaza maji na sasa tumeongeza zaidi ya nusu ya upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tuna Megawati 2,000 na kitu, sasa hivi tunaongelea Megawati 4,000 na kitu. Ni kwa sababu ya tija ya kuanzishwa kwa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Ninamshukuru sana na Mheshimiwa Rais, na ninaamini anafarijika kuona kwamba Wabunge tunamuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge, lengo la Serikali ukisoma Dira ya 2050, tunatamani kujenga vituo vya kupoza umeme kila wilaya. Tija yake itasaidia kupunguza kupotea kwa umeme, itasaidia kupunguza kukatikakatika kwa umeme, kwa sababu umeme utakuwa hausafirishwi mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo yenye viwanda, tumeweka vipaumbele ili kuweza kuchochea uchumi kwa kuhakikisha nishati inakuwa ni ya uhakika. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, katika eneo lake la Kilombero tunaendelea kutafuta fedha. Mipango ipo, fedha zikipatikana, tutajenga kituo hicho cha kupoza umeme ili viwanda vipate umeme wa uhakika. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante, tunaendelea. Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana.

Na. 101

Matumizi ya Nishati Mbadala ya Jua – Njombe

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Nishati Mbadala ya Jua ili kuwapunguzia changamoto Wanawake wa Mkoa wa Njombe?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme kutoka vyanzo vya nishati jadidifu ikiwemo jua, ili kuongeza uwezo wa uzalishaji na kutekeleza mkakati wa kuchanganya vyanzo vya uzalishaji umeme nchini *(generation mix)*.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, umeme unaozalishwa kutokana na nishati ya jua unachangia jumla ya Megawati 65 katika gridi ya Taifa. Kati ya hizo, wazalishaji wadogo *(SPPs)* wanachangia Megawati 15 kutoka vyanzo vya jua.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inatarajia kuongeza Megawati 100 baada ya kukamilika kwa Mradi wa Umeme Jua wa Shinyanga Awamu ya Pili pamoja na Megawati 22 kutoka katika miradi mitatu ya wazalishaji wadogo iliyoko katika hatua za mwisho za ujenzi wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha matumizi ya nishati ya jua katika kuzalisha umeme yanafanikiwa, ikiwa ni pamoja na kuweka ruzuku katika vifaa vya *solar* vinavyoingia nchini ili kuchochea

matumizi ya umeme jua miongoni mwa wananchi, ikiwemo wanawake wa Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia *TANESCO* na *REA* imeendelea kuchukua hatua kuhakikisha maeneo yote nchi nzima ambayo hayajafikiwa na gridi ya Taifa ikiwemo maeneo ya visiwani, yanapata huduma ya umeme kutumia nishati ya jua. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi.

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali ambayo kimsingi nimeridhika, ninapenda kujua tu mkakati sasa wa Wizara. Tunazo shule nyingi ambazo wanapenda kusoma usiku lakini hawana umeme; Ofisi za Watendaji wa Kata, na wa Vijiji wanataka ku-*print*, kutumia kompyuta; sasa hivi Watendaji, Makatibu Tarafa ni wasomi wazuri, je, Wizara ina mpango gani wa kutumia umeme wa jua ambao una bei rahisi? Wanaweka tu zile *panel* za *solar* juu ya bati na kupata umeme katika taasisi hizi za Serikali vijijini. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza dada yangu Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana kwa swali lake zuri, lakini kwa kufuatilia kwa karibu na kuona umuhimu wa kuwa na *generation mix* katika uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo ni ngumu kupeleka nyaya za umeme kwa mfano maeneo ya visiwani, lakini kuna baadhi ya taasisi ambazo zinaweza kutumia umeme mbadala badala ya kutumia umeme wa gridi kwa maana ya kutegemea nyaya kama alivyoeleza vizuri sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana kwamba Serikali yetu sikivu ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan iliamua kuweka ruzuku kwenye vifaa vyote

vinavyoingia nchini ambavyo vinahusika na uzalishaji wa umeme kupitia umeme jua. Kwa kufanya hivyo, imewapa unafuu wananchi kuweza kununua *solar systems* ambazo mtu anaweza akatumia kutokana na uhitaji wake. Kwenye maeneo ya vijijini na taasisi mbalimbali, tumepeleka hizi *solar* kwa nafuu ya ruzuku zaidi ya 50%, zile ambazo ziko chini ya megawati 50 tumepeleka ruzuku kwa zaidi ya 85% tumeingiza mle.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi Serikali tunafahamu umuhimu wa jambo hilo na tunashukuru kwa ushauri mzuri ambao Mheshimiwa Mbunge anatupatia na tunaendelea kuzipelekea taasisi ambazo ni ngumu kutumia umeme wa gridi waweze kutumia umeme wa *solar* kama shule na taasisi nyingine ndogo ndogo ambazo ziko mbali na umeme wa gridi. Ninashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, ni takribani miaka minne sasa tangu tumeanza kuzungumzia Bwawa la Lumakalya katika Kata ya Bulongwa, Kata ya Kipagalo, na Kata ya Iniho. Wananchi wale wamesimama kwa takribani miaka minne hawafanyi shughuli za kiuchumi wakisubiri fidia ili kujengwe chanzo hiki cha umeme. Ni lini Serikali itatoa fedha kwa wananchi hawa ili wapishe mradi, na pia mradi uweze kujengwa kwa masilahi ya wananchi wa Tanzania na Wanamakete zaidi? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na leo ni mara ya pili ameniuliza swali hili na nimekuwa nikifuatilia kwa karibu. Ninajua naye anafahamu kwamba umeme wa maji ndiyo umeme ambao tunautegemea sana katika *generation mix*, kwa sababu hilo Bwawa la Lumakalya na umeme wa *hydro* ambao utazalishwa pale ni moja kati ya mradi mkubwa ambao tunautegemea kutusaidia kuongeza zile Megawati 8,000 ambazo tunatarajia kuzifikia ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kutafuta fedha ili tuweze kuwalipa fidia wananchi wake na mwisho wa siku tuweze kuanzisha mradi huo. Kwa hiyo, nimwombe awe na Subira, sisi wenyewe tuna uhitaji mradi huo sana kwa sababu uko kwenye ilani, uko kwenye Dira na sisi Wabunge tumeshawaeleza wananchi kwamba tutafikia Megawati 8,000. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi kutafuta fedha tulipe fidia ili tuweze kuanzisha mradi huo muhimu wa kimkakati. Ninakushukuru.

SPIKA: Waheshimiwa maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha. Sasa ni kipindi cha wageni. Nitaanza na wageni waliokaa katika jukwaa Mheshimiwa Spika.

Wapo wageni 33 wa Mheshimiwa Spika ambao ni Umoja wa Wanamichezo wa Simba na Yanga kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine waliokaa Jukwaa la Spika, ni wageni watatu wa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Dkt. Maduhu Kazi, Naibu Katibu Mkuu (Mazingira); Dkt. Deogratius Paul, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Hifadhi ya Bioanuai; Dkt. Fredrick Manyika, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Mabadiliko ya Tabianchi na Tathmini ya Mazingira; Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera Charles, kutoka Wilaya ya Butiama Mkoa wa Mara ambaye ni Ndugu Madaraka Nyerere, Mtoto wa Mwalimu Julius Nyerere, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Bunge kutoka Ubalozi wa Marekani ambao ni Ndugu Garvey Pierre, Mkuu wa Kitengo cha Siasa, *welcome to the Parliament*; na Ndugu Deogratius Kithama, Afisa Ubalozi. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Sumbawanga na Mkoani Rukwa. *(Makofi)*

Wapo wageni 32 wa Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Karatu Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ambaye ni Meneja Biashara Wakubwa wa *Yas* Kanda za Juu Kusini; na Mfugaji wa Mbwa wa Kisasa wa Kibiashara Ndugu Rornald Richard Makawa. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Ndugu Trace Mwakyembe, mtoto wake kutoka Zanzibar.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo, Ndugu Fulgence Matipa, mpigakura wake kutoka Nkasi Kaskazini mkoani Rukwa. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Tamima Haji Abass, familia yake kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas, ndugu zake kutoka Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watano wa Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Musoma Mjini Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Abubakar Ali Omari, wapigakura wake kutoka Jimbo la Igunga mkoani Tabora. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, marafiki zake kutoka Jijini Dodoma na nchini Zimbabwe. *(Makofi)*

Wapo wageni saba wa Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala, viongozi wa CCM kutoka Kata ya Rwamgasa Jimbo la Busanda mkoani Geita. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 42 wa Mheshimiwa Erick James Shigongo, Madiwani na Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka Wilaya ya Buchosa mkoani Mwanza. *(Makofi)*

Vilevile, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Kwanza ni Viongozi watatu wa Taasisi ya Kiislam *Masjid Salahudin* kutoka mkoani Kilimanjaro, karibuni. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 56 na walimu nane wa Shule ya Dunda kutoka Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 120 na walimu saba wa Shule ya Sekondari ya Wasichana D'alzon ya Jijini Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa, mnakumbushwa leo siku ya Alhamisi tarehe 3 Septemba, 2026 Waziri wa Mifugo Uvuvi, Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa anaomba kukutana na Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Kagera, Simiyu, Kigoma, Rukwa, Katavi, Ruvuma, Njombe na Mbeya.

Kikao hiki kitafanyika katika Ukumbi wa Frank Mfundo jengo la utawala ghorofa ya tatu kuanzia saa saba mchana mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge.

Ajenda ya kikao hiki ni uelewa wa mikopo inayotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa vijana hususan ufugaji samaki kwa njia ya vizimba. Waheshimiwa Wabunge wa mikoa hiyo iliyotajwa mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Mwenyekiti wa *TYPC*, Mheshimiwa Zainab Katimba anaomba kuwatanganzia Wabunge wote vijana wenye umri wa chini ya miaka 40 kuwa leo tarehe 3 Septemba, 2026 kutakuwa na mafunzo ya kuwajengea uwezo Wabunge vijana yatakayofanyika baada ya Bunge kuahirishwa kuanzia saa nane mchana hadi saa kumi jioni kwenye Ukumbi wa Msekwa.

Mafunzo haya yatafunguliwa na Waziri wa Madini, Mheshimiwa Anthony Mavunde. Wabunge wote vijana mnaombwa kufika bila kukosa.

Katibu.

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Azimio la Bunge kuhusu kuridhia Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani *(Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute)*

SPIKA: Ahsante. Sasa ninamwita Waziri. Jiandae Mwenyekiti.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ninaomba kuwasilisha Azimio la Kuridhia Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani *(Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute)*.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la azimio la kuridhia mkataba wa uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani duniani, Ibara ya 21 ya mkataba wa uanzishwaji wa taasisi hiyo inatoa nafasi kwa nchi kujiunga na Taasisi ya *GGGI* baada ya kusainiwa kwa mikataba na kuwasilishwa hati ya kuridhia masharti ya mkataba huo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya *GGGI*.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *GGGI* ni taasisi ya Kimataifa inayowezesha nchi wanachama kutekeleza mipango ya maendeleo inayozingatia ukuaji wa uchumi wa kijani ili kufikia malengo endelevu na makubaliano ya Paris kuhusu upunguzaji wa gesi joto.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *GGGI* iliundwa rasmi tarehe 20 Juni, 2012 ikiwa na nchi wanachama watano baada ya kusainiwa kwa mkataba wa uanzishwaji wa taasisi hiyo kwa mujibu wa Ibara

ya 22. Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi hiyo ulianza kutekelezwa tarehe 18 Oktoba, 2012 baada ya nchi tatu kuwasilisha hati ya kuridhia kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya *GGGI.* Hadi Mei, 2026 taasisi ilikuwa na wanachama 55 ambapo kati ya hao, 54 ni nchi wanachama, na moja ni jumuiya ya kikanda ambayo ni *Organization of Eastern Caribbean States (OECS)*. Aidha, nchi wanachama 13 zinatoka Bara la Afrika ambazo ni Nigeria, Angola, Benin, Burkina Faso, *Cote d'Ivoire,* Ethiopia, Morocco, Rwanda, Senegal, Togo, Uganda, Kenya na Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi za Afrika Mashariki ambazo zimejiunga na kufaidika na taasisi ni Rwanda, Kenya na Uganda. Aidha, hadi kufikia Mei, 2026 nchi 28 zilikuwa zimeonesha nia ya kuridhia mkataba wa kuanzishwaji wa *GGGI* ambapo kati ya nchi hizo 16 zinatoka Bara la Afrika. Nchi hizo ni Cameroon, Comoros, Djibouti, Gambia, Ghana, Misri, Madagascar, Malawi, Msumbiji, Tunisia, *São Tomé and Príncipe,* Sierra Leone, Somalia, Sudan, Zimbabwe na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Jumuiya Umoja wa Ulaya pia ipo katika mchakato wa kuwa mwanachama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *GGGI* ilianzishwa kwa lengo la kushirikiana na nchi wanachama katika uandaaji wa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; kusaidia taasisi za ndani za nchi mwanachama kupata ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya Kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi; kuwezesha uwekezaji kwenye hati fungani za kijani; kuwezesha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye masharti nafuu ya riba kwa nchi wanachama; kuimarisha mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti na kuwajengea uwezo watalaamu wa nchi mwanachama katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya uanzishwaji wa Taasisi ya *GGGI* ni kushirikiana na nchi wanachama katika uandaaji wa miradi ya hifadhi ya mazingira ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; kusaidia taasisi za ndani kupata ithibati katika usimamizi

wa fedha za mifuko ya Kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi; kuwezesha uwekezaji kwenye hati fungani za kijani; kuwezesha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi; kuimarisha mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti; na kuwajengea uwezo wa kitaalamu wataalamu wetu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani. Kigezo kimojawapo cha kunufaika na faida zitokanazo na Taasisi ya *GGGI* ni kuwa mwanachama wa taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu una ibara 28. Ninaomba nieleze maudhui ya baadhi ya ibara kwa ufupi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 2, inayohusu malengo ya kuanzishwa kwa Taasisi ya *GGGI*. Ibara hii inaeleza malengo ya kuanzishwa kwa Taasisi ya *GGGI* ambayo ni kusaidia maendeleo endelevu kwa nchi mwanachama hususan nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi kwa kusaidia na kuwezesha dhana ya ukuaji wa uchumi wa kijani; na kuwezesha upatikanaji wa nafasi za ajira zenye staha.

Mheshimiwa Spika, malengo mengine ni kupunguza umaskini; kukuza ushirikishwaji wa jamii; kukuza hifadhi endelevu ya mazingira ikiwemo upunguaji wa uzalishaji wa gesijoto na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; na kukuza uhifadhi wa bionuai na upatikanaji wa nishati safi na maji safi na salama kwa gharama nafuu kupitia ushirikiano kati ya nchi zinazoendelea, sekta ya umma pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3, inatoa tafsiri ya mwanachama mchangiaji na mwanachama mshiriki. mwanachama mchangiaji ni mwanachama ambaye anachangia kiasi kisichopungua Dola cha Marekani milioni 15 kwa kipindi cha miaka mitatu au Dola za Marekani milioni 10 kwa kipindi cha miaka miwili ya kwanza ya uanachama wake. Mwanachama mshiriki, ni mwanachama wa *GGGI* ambaye sio mwanachama mchangiaji.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 ni shughuli za Taasisi ya *GGGI*. Ibara hii inaeleza shughuli za Taasisi ya *GGGI* ambazo ni kusaidia nchi zinazoendelea na kuzijengea uwezo wa kubuni na kusaidia kutekeleza mipango na maendeleo kwa kuzingitia dhana ya uchumi wa kijani; kupunguza umaskini; kuzalisha fursa za ajira na ushirikishwaji wa jamii; kufanya tafiti; na kuhamasisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na ubunifu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5 inahusu uanachama. Ibara hii inaeleza sifa ya kuwa mwanachama wa Taasisi ya *GGGI* ambazo ni nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa au kuwa jumuiya ya kikanda ambayo imekubali kutekeleza malengo ya taasisi kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 2 ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, Ibara 12(1) inahusu vyanzo vya mapato. Ibara hii inaeleza vyanzo vya mapato ya Taasisi ya *GGGI* ambavyo ni michango ya hiari kutoka kwa wanachama wa taasisi hiyo, michango ya hiari kutoka mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, mauzo ya machapisho na mapato mengine, riba kutokana na uwekezaji kwenye mifuko mbalimbali na mapato mengine kulingana na kanuni ya fedha zilizoidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Taasisi ya *GGGI*.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 ni kuhusu kinga na upendeleo. Ibara hii inaeleza kuwa nchi mwanachama inaweza kutoa kinga na upendeleo wa Taasisi ya *GGGI* ikiwemo mali na wafanyakazi kwake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21 kuridhia mkataba Ibara hii inaeleza utaratibu wa nchi kujiunga na Taasisi ya *GGGI* baada ya kusainiwa kwa mkataba na kuwasilishwa hati ya kuridhia masharti ya mkataba huo *instrument per session* kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya *GGGI*.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 22(2) inaeleza utaratibu wa kuanza kuwa mwanachama kamili wa Taasisi ya *GGGI* ambapo nchi itakuwa mwanachama kamili siku 30 baada ya kuwasilisha

hati ya kuridhia kujiunga na mkataba wa uanzishwaji wa Taasisi ya *GGGI*.

Mheshimiwa Spika, Ibara 24 marekebisho, Ibara hii inaeleza kuwa nchi mwanachama ina haki ya kupendekeza marekebisho ya mkataba wa uanzishwaji wa Taasisi ya *GGGI* kwa masuala ambayo yatakuwa na manufaa kwa nchi mwanachama.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 25 inahusu kujitoa uanachama. Ibara hii inaelezea utaratibu wa kujitoa uanachama kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya *GGGI* ambapo utekelezaji wake unaanza rasmi miezi sita baada ya Mkurugenzi kupokea taarifa ya kujitoa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 28 inahusu kuvunjwa kwa mkataba. Ibara hii inaeleza utaratibu wa kuvunjwa kwa mkataba ambapo hatua hiyo itatekelezwa kwa kuzingatia maamuzi ya mkutano mkuu wa wanachama wote na utekelezaji wake utaanza mwaka mmoja baada ya uamuzi kutolewa. Aidha, baada ya kuvunjwa kwa mkataba wa *GGGI,* Taasisi ya *GGGI* itakoma.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya faida ya kuridhia Mkataba wa *GGGI*. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia mkataba wa kuanzishwaji wa Taasisi ya *GGGI* itaweza kunufaika katika masuala mbalimbali ikiwemo kuongezeka kuimarika kwa uwezo wa kuibua na kuandaa miradi ya hifadhi ya mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na kuongezeka kwa taasisi za ndani zenye ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya Kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, manufaa mengine ni kuongezeka kwa wawekezaji kwenye hati fungani za kijani; kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi; na kuongezeka kwa wigo wa kidemokrasia wa ushawishi wa nchi katika medani za kisiasa kiuchumi na uhifadhi wa mazingira; kuongezeka kwa upatikanaji wa fursa za ajira kwa Watanzania; na kuimarika kwa mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko tabianchi kupitia tafiti

na kuongezeka kwa tija na uzoefu wa wataalamu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuridhiwa kwa Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani, Serikali haitaweza kuweka maangalizo kwa kuwa Ibara ya 23 ya mkataba imezuia uwekwaji wa maangalizo wakati wa kusaini au kuridhia mkataba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kuwasilisha Azimio la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani *(Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute)* kama ifuatavyo:-

Kwa Kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa;

Na Kwa Kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa mikataba mbalimbali ya Kimataifa na kikanda ya hifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi; Mikataba hiyo inajumuisha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (*United Nations Framework Convention on Climate Change - UNFCCC);* Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea Hali ya Jangwa na Ukame (*United Nations Convention to Combat Desertification – UNCCD);* na Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuwai *(Convention of Biological Diversity - CBD);*

Na Kwa Kuwa, Taasisi ya Ukuaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani ilianzishwa kwa lengo la kushirikiana na nchi wanachama katika uandaaji wa miradi na uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kusaidia taasisi za ndani kupata ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya Kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kuwezesha uwekezaji kwenye hati fungani za kijani, kuwezesha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi, kuimarisha mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya

tabianchi kupitia tafiti na kuwajengea uwezo wataalamu wetu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani;

Na Kwa Kuwa, Taasisi ya Ukuaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani ni taasisi ya Kimataifa inayowezesha nchi wanachama kutekeleza mipango ya maendeleo inayozingatia ukuaji wa uchumi wa kijani ili kufikia malengo endelevu ya Makubaliano ya Paris kuhusu upunguzaji wa gesi joto;

Na Kwa Kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inadhamiria kujiunga kama mwanachama mshiriki itakuwa na wajibu wa kutoa kinga na haki ya kidiplomasia kwa taasisi za ukuzaji wa maendeleo ya kijani duniani iwapo zitajenga ofisi nchini;

Na Kwa Kuwa, madhumuni ya Mkataba huu wa Uanzishaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani yanajumuisha:-

(a) Kusaidia kuwezesha dhana ya ukuaji wa uchumi wa kijani;

(b) Kuwezesha upatikanaji wa fursa za nafasi za ajira zenye staha;

(c) Kupunguza umaskini;

(d) Kuongeza ushirikishwaji wa jamii katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko dhidi ya athari ya mabadiliko ya tabianchi;

(e) Kuhifadhi uendelevu wa mazingira ikiwemo upunguzaji wa uzalishaji wa gesi joto na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi;

(f) Kuwezesha uhifadhi wa Bioanuai; na

(g) Upatikanaji wa nishati safi na maji safi kwa gharama nafuu kupitia ushirikiano kati ya nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea, sekta ya umma na sekta binafsi.

Na Kwa Kuwa, kuridhiwa kwa mkataba huu kutakuwa na manufaa yafuatayo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:-

(a) Kuimarika kwa uwezo wa kuibua na kuandaa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(b) Kuongezeka kwa taasisi za ndani zenye ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya Kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi;

(c) Kuongezeka kwa uwekezaji kwenye hati fungani za kijani.

(d) Kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu;

(e) Kuongezeka kwa wigo wa kidiplomasia na ushawishi wa nchi katika medani za kisiasa, kiuchumi na uhifadhi wa mazingira;

(f) Kuongezeka kwa upatikanaji wa fursa za ajira kwa Watanzania;

(g) Kuimarika kwa mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti; na

(h) Kuongezeka kwa tija na uzoefu wa wataalamu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani.

Kwa Hiyo Basi, kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutokana na kuridhia mkataba huo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Tatu na kwa mujibu wa mashati ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 linaazimia kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji

wa Maendeleo ya Kijani Duniani *(Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute)*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili Azimio hili na kuliridhia kwa mujibu wa Ibara 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA), MHESHIMIWA MHANDISI. HAMAD YUSSUF MASAUNI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAELEZO KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA UANZISHWAJI WA TAASISI YA UKUZAJI WA MAENDELEO YA KIJANI DUNIANI (AGREEMENT ON THE ESTABLISHMENT OF THE GLOBAL GREEN GROWTH INSTITUTE) – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ninaomba kuwasilisha Azimio la Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani (Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute).

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Azimio la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani ni Ibara ya 21 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani inayotoa nafasi kwa nchi kujiunga na Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani (Global Green Growth Institute (Taasisi ya GGGI)) baada ya kusainiwa kwa mkataba na kuwasilisha Hati ya kuridhia masharti ya mkataba huo (Instrument of Accession) kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya GGGI.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya GGGI ni taasisi ya kimataifa inayowezesha nchi wanachama kutekeleza mipango ya maendeleo inayozingatia ukuaji wa uchumi wa kijani ili kufikia

malengo endelevu na Makubaliano ya Paris kuhusu upunguzaji wa gesijoto.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya GGGI iliundwa rasmi tarehe 20 Juni 2012 ikiwa na nchi wanachama 5 baada ya kusainiwa kwa Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI. Kwa mujibu wa Ibara ya 22, Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI ulianza kutekelezwa tarehe 18 Oktoba, 2012 baada ya nchi tatu (3) kuwasilisha Hati za Kuridhia kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya GGGI. Hadi Mei 2026, Taasisi ya GGGI ilikuwa na wanachama 55 ambapo kati ya hao, 54 ni nchi wanachama na 1 ni Jumuiya ya Kikanda ambayo ni Organisation of Eastern Caribbean States (OECS). Aidha, nchi wanachama kumi na tatu (13) zinatoka Bara la Afrika ambazo ni Nigeria, Angola, Benin, Burkina Faso, Cote D'Ivoire, Ethiopia, Morocco, Rwanda, Senegal, Togo, Uganda, Kenya na Zambia. Nchi za Afrika Mashariki ambazo zimejiunga na kufaidika na Taasisi hii ni Rwanda, Kenya na Uganda. Aidha, hadi kufikia Mei, 2026 nchi 28 zilikuwa zimeonesha nia ya kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa GGGI ambapo kati ya hizo nchi 16 zinatoka Bara la Afrika. Nchi hizo ni Cameroon, Comoros, Djibouti, Gambia, Ghana, Misri, Madagascar, Malawi, Msumbiji, Tunisia, São Tomé and Príncipe, Sierra Leone, Somalia, Sudan, Tanzania na Zimbabwe. Aidha, Jumuiya ya Umoja wa Ulaya pia uko katika mchakato wa kuwa mwanachama.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya GGGI ilianzishwa kwa lengo la kushirikiana na nchi wanachama katika uandaaji wa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; kusaidia taasisi za ndani za nchi wanachama kupata ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi; kuwezesha uwekezaji kwenye hati fungani za kijani; kuwezesha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi wanachama; kuimarisha mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti na kuwajengea uwezo wataalamu wa nchi wanachama katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani.

2.0 MADHUMUNI YA MKATABA WA UANZISHWAJI WA TAASISI YA GGGI

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI ni kushirikiana na nchi wanachama katika uandaaji wa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kusaidia taasisi za ndani kupata ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kuwezesha uwekezaji kwenye hati fungani za kijani, kuwezesha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi, kuimarisha mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti na kuwajengea uwezo wa wataalamu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani. Kigezo kimojawapo cha kunufaika na faida zitokanazo na Taasisi ya GGGI ni kuwa Mwanachama wa Taasisi hiyo.

3.0 IBARA ZA MKATABA NA MAUDHUI YAKE

Mheshimiwa Spika, mkataba huu una Ibara 28 naomba nielezee maudhui ya baadhi ya Ibara kwa ufupi kama ifuatavyo: -

Ibara ya 2: Malengo Kuanzishwa kwa Taasisi ya GGGI

Ibara hii inaeleza malengo ya kuanzishwa kwa Taasisi ya GGGI ambayo ni kusaidia maendeleo endelevu kwa nchi wanachama hususan nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi (emerging economies) kwa: kusaidia na kuwezesha dhana ya ukuaji wa uchumi wa kijani; kuwezesha upatikanaji wa nafasi za ajira zenye staha; Kupunguza umasikini; kukuza ushirikishwaji wa jamii; kukuza hifadhi endelevu ya mazingira ikiwemo upunguzaji wa uzalishaji wa gesijoto na uhimilivu mabadiliko ya tabianchi; kukuza uhifadhi wa bionuai; na upatikanaji wa nishati safi na maji safi na salama kwa gharama nafuu kupitia ushirikiano kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea sekta ya umma na binafsi;

Ibara ya 3: Tafsiri

Ibara hii inatoa tafsiri ya mwanachama mchangiaji na mwanachama mshiriki. Mwanachama mchangiaji ni mwanachama ambaye anachangia kiasi kisichopungua dola za

Marekani milioni 15 kwa kipindi cha miaka mitatu (3) au dola za Marekani milioni 10 kwa kipindi cha miaka miwili (2) ya kwanza ya uanachama wake na Mwanachama Mshiriki ni mwanachama wa GGGI ambaye siyo mwanachama mchangiaji;

Ibara ya 4: Shughuli ya Taasisi ya GGGI
Ibara hii inaelezea shughuli za Taasisi ya GGGI ambazo ni: Kusaidia nchi zinazoendelea kwa kuzijengea uwezo wa kubuni na kutekeleza mipango ya maendeleo ya kwa kuzingatia dhana ya uchumi wa kijani; Kupunguza umasikini; Kuzalisha fursa za ajira na ushirikishwaji wa jamii; kufanya utafiti; Kuhamasisha ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ili kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na ubunifu;

Ibara ya 5: Uanachama
Ibara hii inaeleza sifa za kuwa mwanachama wa Taasisi ya GGGI ambazo ni; nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa au kuwa Jumuiya ya Kikanda ambayo imekubali kutekeleza malengo ya taasisi kama yalivyoanishwa katika Ibara ya 2 ya Mkataba;

Ibara ya 12(1): Vyanzo vya Mapato
Ibara hii inaeleza vyanzo vya mapato vya Taasisi ya GGGI ambavyo ni: - Michango ya hiari kutoka kwa wanachama wa Taasisi ya GGGI; Michango ya hiari kutoka kwa Mashirika yasiyokuwa ya Serikali; Mauzo ya machapisho na mapato mengine; Riba kutokana na uwekezaji kwenye mifuko mbalimbali; na Mapato mengine kulingana na kanuni za fedha zilizoidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Taasisi ya GGGI;

Ibara ya 15: Kinga na Upendeleo
Ibara hii inaeleza kuwa nchi mwanachama inaweza kutoa kinga na upendeleo kwa Taasisi ya GGGI ikiwemo mali na wafanyakazi wake kwa mujibu wa sheria;

Ibara ya 21: Kuridhia Mkataba (Accession)
Ibara hii inaeleza utaratibu wa nchi kujiunga na Taasisi ya GGGI baada ya kusainiwa kwa mkataba na kuwasilisha Hati ya kuridhia masharti ya mkataba huo (Instrument of Accession) kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya GGGI;

Ibara ya 22(2) inaeleza utaratibu wa kuanza kuwa mwanachama kamili wa Taasisi ya GGGI ambapo nchi itakuwa mwanachama kamili siku ya 30 baada ya kuwasilisha Hati ya kuridhia kujiunga na Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI;

Ibara ya 24: Marekebisho
Ibara hii inaeleza kuwa nchi mwanachama ina haki ya kupendekeza marekebisho ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI kwa masuala ambayo yatakuwa na manufaa kwa nchi mwanachama;

Ibara ya 25: Kujitoa Uanachama
Ibara hii inaeleza kuhusu utaratibu wa kujitoa uanachama kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya GGGI ambapo utekelezaji wake utaanza rasmi (take effect) miezi sita (6) baada ya Mkurugenzi kupokea taarifa ya kujitoa; na

Ibara ya 28: Kuvunjwa kwa Mkataba
Ibara hii inaeleza utaratibu wa kuvunjwa kwa Mkataba ambapo hatua hiyo itatekelezwa kwa kuzingatia maamuzi ya Mkutano Mkuu wa wanachama wote na utekelezaji wake utaanza mwaka mmoja (1) baada ya uamuzi kutolewa. Aidha, baada ya kuvunjwa kwa Mkataba wa GGGI, Taasisi ya GGGI itakoma.

4.0 MATOKEO NA FAIDA ZA KURIDHIA MKATABA WA GGGI

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI itaweza kunufaika katika masuala mbalimbali ikiwemo:

a) Kuongezeka kuimarika kwa uwezo wa kuibua na kuandaa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

b) Kuongezeka kwa taasisi za ndani zenye ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi;

c) Kuongezeka kwa uwekezaji kwenye hati fungani za kijani;

d) Kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi;

e) Kuongezeka kwa wigo wa kidiplomasia na ushawishi wa nchi katika medani za kisiasa, kiuchumi na uhifadhi wa mazingira;

f) Kuongezeka kwa upatikanaji wa fursa za ajira kwa Watanzania;

g) Kuimarika kwa mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti; na

h) Kuongezeka kwa tija na uzoefu wa wataalamu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani.

5.0 MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KURIDHIA MKATABA

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuridhiwa kwa Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani, Serikali haitaweza kuweka maangalizo (reservations) kwa kuwa katika Ibara ya 23 ya Mkataba umezuia uwekwaji wa maangalizo (reservations) wakati wa kusaini au kuridhia Mkataba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha Azimio la kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani (Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute) kama ifuatavyo;

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Umoja wa Mataifa;

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa mikataba mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda ya hifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Mikataba hiyo inajumuisha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (United Nations Framework Convention

on Climate Change - UNFCCC), Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (United Nations Convention to Combat Desertification - UNCCD) na Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai (Convention on Biological diversity - CBD);

KWA KUWA, Taasisi ya Ukuzaji Maendeleo ya Kijani Duniani ilianzishwa kwa lengo la kushirikiana na nchi wanachama katika uandaaji wa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kusaidia taasisi za ndani kupata ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kuwezesha uwekezaji kwenye hati fungani za kijani, kuwezesha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi, kuimarisha mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti na kuwajengea uwezo wa wataalamu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani;

KWA KUWA, Taasisi ya Ukuzaji Maendeleo ya Kijani Duniani ni taasisi ya kimataifa inayowezesha nchi wanachama kutekeleza mipango ya maendeleo inayozingatia ukuaji wa uchumi wa kijani ili kufikia malengo endelevu na Makubaliano ya Paris kuhusu upunguzaji wa gesijoto;

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inadhamiria kujiunga kama Mwanachama mshiriki, itakuwa na wajibu wa kutoa kinga na haki za kidiplomasia kwa Taasisi ya Ukuzaji wa Kijani Duniani iwapo itajenga ofisi nchini;

KWA KUWA, madhumuni ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji Maendeleo ya Kijani Duniani yanajumuisha:-

(a) kusaidia na kuwezesha dhana ya ukuaji wa uchumi wa kijani;

(b) kuwezesha upatikanaji wa fursa za nafasi za ajira zenye staha;

(c) kupunguza umasikini;

(d) kuongeza ushirikishwaji wa jamii katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira na makabiliano dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi;

(e) hifadhi endelevu ya mazingira ikiwemo upunguzaji wa uzalishaji wa gesijoto na uhimilivu mabadiliko ya tabianchi;

(f) kuwezesha uhifadhi wa bioanuai; na

(g) upatikanaji wa nishati safi na maji safi kwa gharama nafuu kupitia ushirikiano kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea sekta ya umma na binafsi.

NA KWA KUWA, kuridhiwa kwa Mkataba huu kutakuwa na manufaa yafuatayo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:

(a) kuimarika kwa uwezo wa kuibua na kuandaa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(b) kuongezeka kwa taasisi za ndani zenye ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi;

(c) kuongezeka kwa uwekezaji kwenye hati fungani za kijani;

(d) kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi;

(e) kuongezeka kwa wigo wa kidiplomasia na ushawishi wa nchi katika medani za kisiasa, kiuchumi na uhifadhi wa mazingira;

(f) kuongezeka kwa upatikanaji wa fursa ya ajira kwa Watanzania;

(g) kuimarika kwa mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti; na

(h) kuongezeka kwa tija na uzoefu wa wataalamu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani.

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutokana na kuridhia Mkataba huo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Tatu, na kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani (Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba Bunge lako tukufu lijadili Azimio hili, na kuliridhia kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mhandisi Hamad M.Y. Masauni (Mb.)
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. JACKSON G. KISWAGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, ninaomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 113(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge (2025) naomba kuwasilisha Maoni ya

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu kuridhia Mkataba wa Uanzishaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani, 2012 *(The Agreement on the Establishment of Global Green Institute of 2012)*. Maoni yanayowasilishwa ni utekelezaji wa jukumu la Kamati kushughulikia mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, kwa mujibu wa fasili ya saba, Kifungu cha 1(b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Sambamba na jukumu hilo la kikanuni, jukumu hilo ni sehemu ya utekelezaji wa Madaraka ya Bunge ya kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyofanyia kazi. Kwa mamlaka uliyopewa na Kanuni ya 111(a) ulileta hoja ya kuridhiwa kwa mkataba husika kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge Maji na Mazingira, na Kamati ilikutana tarehe 15 Agosti, 2026 ili kupata maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano wa Mazingira, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yusuff Masauni.

Mheshimiwa Spika, aidha, tarehe 22 Agosti, 2026, Wajumbe wa Kamati walipata tena fursa nyingine ya kujadili maudhui ya mkataba huo kwa kupata maelezo ya ziada ya Serikali yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mhandisi Dkt. Yusuff Masauni.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilialika wadau mbalimbali kufika mbele ya Kamati ili kutoa maoni yao kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wa mkataba huo kwa mujibu wa kanuni ya 111(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Wadau 11 walifanikiwa kuwasilisha maoni yao mbele ya Kamati na wadau wengine watatu waliwasilisha maoni yao kwa njia ya barua pepe.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati. Taasisi ya *GGGI* ni taasisi ya Kimataifa inayowezesha nchi wanachama kutekeleza mipango ya maendeleo inayozingatia ukuaji wa uchumi wa kijani

ili kufikia malengo endelevu na Makubaliano ya Paris kuhusu upunguzaji wa gesijoto.

Mheshimiwa Spika, taasisi hii ilianzishwa nchini Korea Kusini mwaka 2010 kama taasisi isiyo ya Kiserikali isiyokusudia kutengeneza faida *(Non-Profit Foundation)*. Tarehe 20 Juni, 2022 mkataba wa kuibadili taasisi hiyo kuwa taasisi ya Kimataifa uliwekwa wazi kwa ajili ya kusainiwa Jijini Rio de Janeiro nchini Brazil. Mkataba wa uanzishwaji wa taasisi ya Kimataifa ya *GGGI* ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 18 Oktoba, 2012 kufuatia nchi tano kukamilisha taratibu za kusaini na kuridhia mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, hadi Mei, 2026 taasisi ya *GGGI* ilikuwa na nchi wanachama 55 ambapo kati ya hizo, wanachama 13 wanatoka Bara la Afrika ambao ni Angola, Algeria, Benin, Burkina Faso, Cote d'Ivoire, Ethiopia, Morocco, Rwanda, Senegal, Togo, Uganda, Kenya na Zambia.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mei, 2026 nchi 28 zilikuwa zimeonesha nia ya kuridhia mkataba wa kuanzishwa kwa taasisi ya *GGGI* ambapo kati ya hizo, nchi 16 zinatoka Bara la Afrika. Nchi hizo ni Tanzania, Cameroon, Comoros, Djibouti, Gambia, Ghana, Misri, Madagascar, Malawi, Msumbiji, Sao Tome and Principe, Sierra Leone, Somalia, Sudan, Tunisia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3 ikisomwa pamoja na Ibara ya 12 ya Mkataba, zimeeleza kuwa kuna aina mbili za wanachama ambao ni wanachama wa kuchangia *(contributing member)* na wanachama wa kushiriki au kutochangia *(participating member)*.

Mheshimiwa Spika, taasisi ya *GGGI* inaipa mamlaka nchi inayotaka kujiunga kuamua aina ya wanachama kama ni uanachama wa kuchangia au uanachama mshiriki wa kutokuchangia. Kwa mujibu wa mkataba huo wanachama wote wana haki sawa katika kufanya maamuzi ya taasisi hiyo kupitia Mkutano Mkuu wa Wanachama yaani *Assembly*.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Kamati ilielezwa kuwa Tanzania inakusudia kuwa mwanachama mshiriki

(participating member). Uanachama huo utaipa nchi haki ya kuwa na kura moja katika Mkutano Mkuu *(Assembly)* kama zilivyo nchi zote wanachama. Aidha, nchi inaweza kupata nafasi ya ushiriki kwenye Baraza *(council)* ambapo kuna nafasi tano kwa wanachama wachangiaji na nafasi tano kwa wanachama washiriki.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya mkataba. Mambo ya mazingira kushughulikiwa kwa mujibu wa Ibara ya 9 na Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ibara hizo zinaweka mujibu wa kulinda maliasili katika kuainisha matumizi na uhifadhi wa rasilimali nchini.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa mikataba mbalimbali ya Kimataifa na ya kikanda inayohusu uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Mikataba hiyo inajumuisha mikataba ya Umoja wa Mataifa ya mabadiliko ya tabianchi na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati ilihitaji kufahamu kama malengo ya kuanzishwa kwa taasisi ya *GGGI* hayatakuwa kikwazo kwa miradi ya kimkakati na kipaumbele ya Kitaifa inayohusisha nishati isiyo safi kama makaa ya mawe na viwanda vya kuchakata mafuta yaani *refineries* pamoja na miradi mingine ya gesi. Kamati ilifahamishwa na Serikali kuwa kujiunga na mkataba huo hakutaathiri mipango ya Serikali katika kutekeleza miradi ya kimkakati hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa na Serikali kwamba Ibara ya 2 haiondoi mamlaka ya Serikali kuamua vipaumbele vyake vya maendeleo. Aidha, miradi ya kimkakati itaendelea kutekelezwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050, sera, sheria, mipango na mikakati ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa shughuli zitakazotekelezwa na taasisi ya *GGGI*. Kamati ilijulishwa na Serikali kuwa shughuli kuu ya taasisi hiyo ni kujenga na

kuwajengea uwezo wataalamu wetu kuandaa maandiko na kuibua miradi, kuomba ufadhili kutoka mifuko ya fedha za mazingira kama *GCF* na *GTF* kwa kutoa urahisi wa kuzifikia fedha za miradi ya mazingira na kufanya utafiti wa kina kuhusu masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejiridhisha kwamba ikiwa mwanachama anahitaji kujitoa uanachama, utaratibu wa kujitoa uko wazi. Katika Ibara ya 25 mwanachama atatoa taarifa ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa *GGGI* ambapo utekelezaji wake utaanza rasmi miezi sita baada ya Mkurugenzi huyo kupokea taarifa ya kujitoa.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kamati ilitaka kufahamu vyanzo vya mapato vya *GGGI* katika kujiendesha iwapo wanachama wengi wataamua kutokuchangia. Serikali imeeleza Kamati kuwa vyanzo vya mapato vya *GGGI* ni pamoja na michango ya hiari na vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, pia, endapo wanachama hawataamua kuchangia michango, *GGGI* itabaki na vyanzo vingine vya mapato kwa mujibu wa Ibara ya 12 (1) ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa za kifedha za *GGGI* zinaonesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2021 – 2024 takribani Dola za Kimarekani milioni 241, sawa na 77.2% zilitokana na vyanzo vingine vya mapato wakati Dola za Kimarekani milioni 71.1, sawa na 22.8% ilikuwa ni michango kutoka nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha kuwa *GGGI* imekuwa ikitegemea kwa kiasi kikubwa mapato yatokanayo na vyanzo vingine vya mapato na siyo michango ya wanachama pekee.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu na faida ya kuridhia mkataba huu. Baada ya kufanya mahojiano na wadau mbalimbali ndani na nje ya Serikali katika kuridhia kwa mkataba wa Taasisi ya *GGGI* Kamati imebaini kwamba kuna manufaa mbalimbali kwa Tanzania kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, manufaa hayo ni pamoja na kuongezeka na kuimarika kwa uwezo wa kuibua na kuandaa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kusaidia kuongezeka kwa taasisi za ndani zenye ithibati pamoja na usimamizi wa fedha za mifuko ya Kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kuongezeka kwa uwekezaji kwenye hatifungani za kijani kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi na kuongezeka kwa wigo wa kidiplomasia na ushawishi wa nchi katika medani za kisiasa, kiuchumi na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, pia, kuongezeka kwa upatikanaji wa fursa kwa ajira kwa Watanzania, kuimarika kwa mbinu za kukabiliana na changamoto za kimazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti na kuongezeka kwa tija na uzoefu wa wataalam wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya Kamati kujadili kwa kina hoja ya Serikali kuhusu Azimio la kuridhia mkataba wa GGGI, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ipewe jukumu la kuratibu shughuli zote zitakazohusiana na taasisi ya *GGGI*. Kwa kuwa mkataba huo unahusisha utekelezaji kupitia sekta mbalimbali hususan uchumi, mazingira, mabadiliko ya tabianchi, uwekezaji, nishati, kilimo, maji, viwanda na maendeleo ya kijani; Serikali baada ya kujiunga na taasisi ya *GGGI* ifanye tathmini ya mara kwa mara juu ya mabadiliko ya sheria *(amendments)* yanayoweza kufanyika baada ya kujiunga ili yasiathiri utekelezaji wa miradi ya kimkakati na vipaumbele vya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujiunga na taasisi ya *GGGI,* Serikali ifanye tathmini ya jumla ili kuona kama matarajio na malengo yamefikiwa kama yalivyokusudiwa na Serikali isimamie Taasisi ya *GGGI* ili iweze kushirikiana na wataalam wa ndani ya

nchi kwa ajili ya kutoa misaada au msaada wa kitaalam kufikia kuandaa maandiko ya miradi ya kijani nchini. Kamati tulijadili na tukaona kwamba Tanzania siyo kisiwa, na kwa kweli tunaishi katika dunia ya pamoja, kwa hiyo, tunahitaji taasisi mbalimbali za Kimataifa ili kuendelea kupanua wigo na kuendelea kujenga uwezo wetu wa kiuchumi hasa katika kusimamia pia masuala ya mazingira. Kwa hiyo, tulijiridhisha kwamba tunaweza kuridhia mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Ninaomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vyema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni vyanzo na nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ambao katika kutekeleza majukumu yao ya kikatiba walichambua, walijadili na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Azimio la Kuridhia Mkataba huu. Kwa kutambua mchango wao, ninaomba majina yao yote yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyoorodheshwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Mheshimiwa *Eng.r* Hamad Yussuf Masauni, akisaidiwa na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo. Aidha, ninawashukuru Watendaji Wakuu wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Dkt. Richard Stanslaus Muyungi akisaidiwa na Manaibu Katibu Makuu wawili, Dkt. Maduhu Isaac Kazi na Dkt. Latifa Mohammed Khamis.

Mheshimiwa Spika, kipekee, ninawashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo kuhusu hoja, baada ya maelezo haya, ninaomba Bunge lako sasa lipokee, lijadili na kuridhia mapendekezo kuhusu kuridhia mkataba wa uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani 2012 *(GGGI)* kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA UANZISHWAJI WA TAASISI YA UKUZAJI WA MAENDELEO YA KIJANI DUNIANI, 2012 (GGGI) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Awali

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 113 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, naomba kuwasilisha **Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Kuhusu Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani, 2012 (GGGI)** ***((The Agreement on Establishment of the Global Green Growth Institute of 2012)***.

Mheshimiwa Spika, maoni yanayowasilishwa ni utekelezaji wa jukumu la Kamati la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa mujibu wa **Fasili ya 7 (1) (b)** ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, sambamba na jukumu hilo la Kikanuni, jukumu hilo ni sehemu ya utekelezaji wa Madaraka ya Bunge ya kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

1.2 Namna Kamati Ilivyofanya Kazi

Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka uliyopewa na Kanuni ya **111 (1)** ulileta Hoja ya Kuridhia Mkataba husika kwa Kamati ya Maji na Mazingira, na Kamati ilikutana tarehe 15 Agosti, 2026 ili kupata maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mhe. Dkt. Hamad Yussuf Masauni (Mb.). Aidha, tarehe 22 Agosti, 2026 Wajumbe wa Kamati walipata tena fursa nyingine ya kujadili maudhui ya Mkataba huo kwa kupata maelezo ya ziada ya Serikali yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mhe. Dkt. Hamad Yussuf Masauni (Mb.).

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilialika wadau mbalimbali kufika mbele ya Kamati ili kutoa maoni yao kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wa Mkataba huo kwa mujibu wa Kanuni ya **111 (2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Wadau 11 walifanikiwa kuwasilisha maoni yao mbele ya Kamati na wadau wengine 3 waliwasilisha maoni yao kwa njia ya barua pepe.

2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI

2.1 Chimbuko la Mkataba

Mheshimiwa Spika, GGGI ni Taasisi ya Kimataifa inayowezesha nchi wanachama kutekeleza mipango ya maendeleo, inayozingatia ukuaji wa uchumi wa kijani, ili kufikia malengo endelevu na Makubaliano ya Paris kuhusu upunguzaji wa gesijoto.

Mheshimiwa Spika, Taasisi hii ilianzishwa nchini Korea Kusini mwaka 2010 kama Taasisi isiyo ya kiserikali isiyokusudia kutengeneza faida (*Non-Profit Foundation*). Tarehe 20 Juni 2012 Mkataba wa kuibadili Taasisi hiyo kuwa Taasisi ya Kimataifa uliwekwa wazi kwa ajili ya kusainiwa Jijini Rio de Janeiro nchini Brazil. Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Kimataifa ya GGGI ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 18 Oktoba, 2012 kufuatia nchi 5 kukamilisha taratibu za kusaini na kuridhia Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, Hadi Mei 2026, Taasisi ya GGGI ilikuwa na nchi wanachama 55 ambapo kati yao, wanachama 11 wanatoka Bara la Afrika ambao ni Angola, Benin, Burkina Faso, Cote D'Ivoire, Ethiopia, Rwanda, Senegal, Togo, Uganda, Kenya na Zambia.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mei, 2026 nchi 27 zilikuwa zimeonesha nia ya kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya GGGI ambapo kati ya hizo nchi 15 zinatoka Bara la Afrika. Nchi hizo ni Tanzania, Cameroon, Comoro, Djibouti, Gambia, Ghana, Madagascar, Malawi, Msumbiji, São Tomé na Príncipe, Sierra Leone, Somalia, Sudan, Tunisia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3 ikisomwa pamoja na Ibara ya 12 ya Mkataba zimeeleza kuna aina mbili za uanachama ambazo ni uanachama wa kuchangia (*Contributing member*) na uanachama wa kushiriki / kutochangia *(participating member.*

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya GGGI inaipa mamlaka nchi inayotaka kujiunga kuamua aina ya uanachama, kama ni uanachama wa kuchangia au mwanachama mshiriki/ kutochangia. Kwa mujibu wa Mkataba huo wanachama wote wana haki sawa katika kufanya maamuzi ya Taasisi hiyo kupitia Mkutano Mkuu wa Wanachama.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Kamati imeelezwa kuwa, Tanzania inakusudia kuwa Mwanachama Mshiriki *(participating member)*. Uanachama huo utaipa nchi haki ya kura moja katika mkutano Mkuu *(Assembly)* kama zilivyo nchi zote wanachama. Aidha, nchi inaweza kupata nafasi ya uwakilishi kwenye Baraza *(Council)* ambako kuna nafasi tano kwa wanachama wachangiaji na tano kwa wanachama washiriki.

2.2 Maudhui ya Mkataba

Mheshimiwa Spika, Mambo ya Mazingira kushugulikiwa kwa mujibu wa Ibara ya 9 na Ibara 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Ibara hizo zinaweka wajibu wa kulinda maliasili katika kuainisha matumizi na uhifadhi wa rasilimali Nchini.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa , Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama wa Mikataba mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Mikataba hiyo inajumuisha:-

(a) Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi *(United Nations Framework Convention on Climate Change – UNFCCC*),

(b) Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame *(United Nations Convention to Combat Desertification – UNCCD)*, na

(c) Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai *(Convention on Biological diversity* – CBD

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati ilihitaji kufahamu kama malengo ya kuanzishwa kwa Taasisi ya GGGI hayatakuwa kikwazo kwa miradi ya kimkakati na kipaumbele ya Kitaifa inayohusisha nishati isiyo safi kama makaa ya mawe na viwanda vya kuchakata mafuta (refineries).

Mheshimiwa Spika, Kamati imehakikishiwa na Serikali kuwa, kujiunga na Mkataba huu hakutaathiri mipango ya Serikali katika kutekeleza miradi ya kimkakati, ambayo inatarajiwa kuanzishwa hapa nchini**.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa na Serikali kwamba, Ibara ya 2 haiondoi mamlaka ya Serikali kuamua vipaumbele vyake vya maendeleo. Aidha, miradi ya kimkakati itaendelea kutekelezwa kwa kuzingatia Dira ya 2050, Sera, Sheria Mipango na Mikakati ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa shughuli (*activites*) zitakazo tekelezwa na Taasisi ya GGGI. Kamati ilijulisha na Serikali kuwa, Shughuli kuu ya Taasisi ni:-

(i) Kujengea wataalamu uwezo wa kuandaa maandiko ya kuibua miradi;

(ii) Kuomba ufadhili kutoka Mifuko ya fedha za mazingira kama GCF na GTF. kwa kutoa urahisi wa kuzifikia fedha za miradi ya mazingira.

(iii) Kufanya utafiti wa kina kuhusu masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejiridhisha kwamba, ikiwa Mwanachama anahitaji kujitoa uanachama, utaratibu wa kujitoa uko wazi, katika Ibara ya 25. Mwanachama atatoa taarifa ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa GGGI ambapo, utekelezaji wake utaanza rasmi (*take effect)* miezi sita (6) baada ya Mkurugenzi huyo kupokea taarifa ya kujitoa. Masharti hayo ya Itifaki yanasomeka kama ifuatavyo: -
"Any party may withdraw from this Agreement by written notification, of its intention to withdraw from this Agreement. Such withdrawal shall take effect six months after the date of receipt by the Director General of the Secretariat of the notification."

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kamati ilitaka kufahamu vyanzo vya mapato vya GGGI katika kujiendesha. Serikali imetoa taarifa kwa Kamati kuwa, Vyanzo vya mapato vya GGGI ni pamoja na michango ya hiari na vyanzo vingine, pia endapo wanachama wachangiaji watasitisha michango, GGGI itabaki na vyanzo vingine vya mapato kwa mujibu wa Ibara ya 12(1) ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Taarifa za Kifedha za GGGI zinaonesha kuwa katika kipindi cha 2021–2024, takribani **US$ 241.2 Mil.** sawa na asilimia **77.2** yalitokana na vyanzo vingine vya mapato, wakati **US$ 71.1 Mil.** sawa na asilimia **22.8** ilikuwa ni michango kutoka nchi Wanachama. Hii inaonesha kuwa GGGI imekuwa ikitegemea kwa kiasi kikubwa mapato yatokanayo na vyanzo vingine vya mapato na si michango ya wanachama pekee.

2.3 Umuhimu na Faida za Kuridhia Mkataba

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya mahojiano na wadau mbalimbali ndani na nje ya Serikali, katika kuridhia kwa Mkataba, wa Taasisi ya GGGI, Kamati imebaini kwamba kuna manufaa mbalimbali kwa Tanzania kuridhia Mkataba huo kama ifuatavyo:

(a) Kuongezeka na kuimarika kwa uwezo wa kuibua na kuandaa miradi ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(b) Kusaidia kuongezeka kwa taasisi za ndani zenye ithibati katika usimamizi wa fedha za mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi;

(c) Kuongezeka kwa uwekezaji kwenye hati fungani za kijani;

(d) Kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo yenye riba nafuu kwa nchi;

(e) Kuongezeka kwa wigo wa kidiplomasia na ushawishi wa nchi katika medani za kisiasa, kiuchumi na uhifadhi wa mazingira;

(f) Kuongezeka kwa upatikanaji wa fursa ya ajira kwa watanzania;

(g) Kuimarika kwa mbinu za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia tafiti; na

(h) Kuongezeka kwa tija na uzoefu wa wataalamu wa ndani katika masuala ya ukuaji wa uchumi wa kijani.

3.0 MAONI NA USHAURI

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kujadili kwa kina Hoja ya Serikali kuhusu **Azimio La Kuridhia Mkataba Wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani, 2012 (GGGI),** Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

(a) Ofisi ya Makamu wa Raisi – Mazingira ipewe jukumu la kuratibu shughuli zote zinazohusiana na GGGI, kwa kuwa Mkataba huo unahusisha utekelezaji kupitia sekta

mbalimbali hususani uchumi, mazingira, mabadiliko ya tabianchi, uwekezaji, nishati, kilimo, maji, viwanda na maendeleo ya jamii;

(b) Serikali baada ya kujiunga na Taasisi ya GGGI, ifanye tathimini ya mara kwa mara juu ya mabadiliko ya Sheria (ammendments) yanayoweza kufanyika baada ya kujiunga ili yasiathiri utekelezaji wa miradi ya kimkakati na vipaumbele vya Kitaifa;

(c) Baada ya kujiunga na GGGI, Serikali ifanye tathimini ya jumla ili kuona kama matarajio ya malengo yamefikiwa kama ilivyokusudiwa; na

(d) Serikali iisimamie Taasisi ya GGGI ili iweze kushirikiana na Wataalam wa ndani ya Nchi, kwa ajili ya kutoa msaada wa kitaalaam katika kuandaa maandiko ya miradi ya kijani nchini.

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, ambao katika kutekeleza majukumu yao ya kikatiba, walichambua, kujadili, na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Azimio la kuridhia Mkataba huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb, - Mwenyekiti
2. Mhe. Prof. Pius Zebhe Yanda, Mb, - M/Mwenyekiti

3. Mhe. Asya Sharif Omar, Mb, - Mjumbe
4. Mhe Anna Richard Lupembe, Mb, - Mjumbe
5. Mhe. Azza Hilal Hamad, Mb, - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. George Venance Lugomela, Mb, - Mjumbe
7. Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb, - Mjumbe
8. Mhe. Haiderali Hussein Gulamali, Mb, - Mjumbe
9. Mhe. Jamal Ramadhan Mwinyi, Mb, - Mjumbe
10. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb, - Mjumbe
11. Mhe. Martha Festo Mariki, Mb, - Mjumbe
12. Mhe. Maryam Azan Mwinyi , Mb, - Mjumbe
13. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb, - Mjumbe
14. Mhe. Mecktridis Fratern Mdaku, Mb, - Mjumbe
15. Mhe. Patali Shida Patali, Mb, - Mjumbe
16. Mhe. Patrick Adkin Mwalunenge , Mb, - Mjumbe
17. Mhe. Eng. Ramadhani Hamza Singano, Mb, - Mjumbe
18. Mhe. Sanya Jussa Jafari, Mb, - Mjumbe
19. Mhe. Thomas Maganga Kampala, Mb, - Mjumbe
20. Mhe. Zuwena Athuman Bushiri, Mb, - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni (Mb.), akisaidiwa na Naibu Waziri wake Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo (Mb), Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Dkt Richard Stanslaus Muyungi, akisaidiwa na Manaibu Katibu Mkuu , Dkt Maduhu Isaac Kazi na Dkt Latifa Mohammed Khamis.

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Leonard, kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 Mapendekezo Kuhusu Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba Bunge lako sasa lipokee, lijadili na kuridhia mapendekezo kuhusu **Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani ,2012 (GGGI), yaani, (The Agreement on**

Establishment of The Global Green Growth Institute Of 2012), kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono Hoja.

Jackson Kiswaga, Mb.
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA
03 Septemba, 2026

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa tutachangia. Tunaanza na Mheshimiwa Pius Zebhe Yanda.

MHE. PIUS Z. YANDA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko Mezani. Ninaomba nianze kwa kusema kwamba, Tanzania kama nchi nyingine zinazoendelea inakabiliwa na athari za mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa ikifanya juhudi za kila aina kuhakikisha kwamba changamoto hizo zinafanyiwa kazi, lakini katika juhudi hizo, Serikali ina historia ya kufanya kazi na taasisi mbalimbali ambazo zinafanana na *GGGI,* kwa mfano *UNEC, UNDP* na taasisi nyingine zinazofanana na hizo. Taasisi hizo zimekuwa ni kiungo muhimu sana katika upatikanaji wa teknolojia, kujenga uwezo kwa Watanzania wenzetu, na pia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kitu kizuri ni kwamba, taasisi hizo zote zinategemea mapendekezo ya Watanzania au taasisi husika, wao wanakuja tu kuwezesha upatikanaj wa fedha kutoka kwenye mifuko ya fedha ya mabadiliko ya tabianchi, kwa mfano *GF, GCF.*

Mheshimiwa Spika, kulingana na Tanzania kuwa na Dira ya 2050 ambayo ina nguzo mahususi ya mazingira na mabadiliko ya

tabianchi, majukumu ya utekelezaji wa mikakati yote ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi na mazingira yamekuwa makubwa zaidi. Hiyo inamaanisha nini? Inamaanisha kwamba ni kwa kipindi ambacho sasa tunahitaji *resources*, tunahitaji kuwezeshwa upande wa teknolojia, na pia kujengewa uwezo ili tuweze kuhakikisha tunaenda na kasi ya jitihada za kukabiliana na uharibifu wa mazingira na pia mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo basi, tunaona kwamba *GGGI* itakuwa ni taasisi ya ziada pamoja na ambazo tayari tunafanyanazo kazi, kutuwezesha sisi kufikisha yale malengo ambayo tunayatarajia chini ya Dira ya 2050.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia kwa zile nchi ambazo tayari zimeshakuwa wanachama, zimeanza kufaidika na kufanya kazi pamoja na hiyo taasisi ikiwemo nchi za Afrika Mashariki. Tuna kila sababu sasa ya kuhakikisha kwamba na sisi tunakuwa wanachama ili tuweze kufaidika na taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunachotaka kusema tu ni kwamba, cha msingi tuwe na utayari wa kuanza kuandaa mawazo au mapendekezo ambayo sasa tunaweza tukaanza kushirikiana na taasisi hiyo, ili tuweze kupata fedha za kuwezesha utekelezaji wa miradi hiyo ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi na pia teknolojia, hasa kwa mfano upande wa tathmini ya hewa ya kaboni. Haya ni maeneo ambayo tunahitaji teknolojia ya ziada.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni *NEMC* itakuwa na mamlaka makubwa ya kusimamia mambo ya mazingira. Tufike mahali tuwe na teknolojia ambayo inaweza ikawa inafuatilia uharibifu wa mazingira katika nchi nzima. Hayo yote yanahitaji ushirikiano na taasisi kubwa kama hizo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Ramadhani Singano, wajiandae Mheshimiwa Ulenge na Mheshimiwa Mwinyi Jamal.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya. Pia nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye kinara namba moja katika suala zima la mazingira.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Biblia katika Kitabu cha Hosea inasema "*Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa",* lakini ukirudi katika Quran Mungu anasema "*Zaharal-fasādu fīl-barri wal-bahri bimā kasabat aydin-nāsi";* anasema, ufisadi umeongezeka bara na baharini kwa sababu ya mikono ya watu kutokutenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ni katika kutii maandiko haya ya kuendana na mabadiliko ya tabianchi, na mabadiliko ya Kimataifa. Sisi hatuwezi tukakaa kama kisiwa kwa sababu mabadiliko ya tabianchi hayana kizuizi, anga ni lile lile moja.

Mheshimiwa Spika, kama inavyokumbukwa, ulikuwepo mkataba wa Kimataifa ule wa *UNFCCC (United Nation Framework Convention on Climate Change),* ukaja *policy agreement* ikiwa chini ya Umoja huu wa Mataifa, baada ya hapo ikatengenezwa Mifuko ya fedha ya *GCF (Global Climate Fund)* na *GEF (Global Environmental Facility)*. Sasa, hii ndiyo zinatoa mitaji kwa ajili ya kuwezesha miradi hii ya mazingira ikiwepo *green growth,* ambapo baadaye ikaonekana sasa iwepo taasisi muhimu ambayo itakuwa ikishauri, ikijenga uwezo, tena mpaka wa kiteknolojia ambayo ndiyo *Global Green Growth Institute (GGGI)*.

Mheshimiwa Spika, taasisi hii ina kazi nyingi muhimu kwa Taifa letu. Mojawapo kama nilivyoongea hapo awali kwamba ni taasisi ya ushauri, tunataka ije itushauri. Ni taasisi ya kiteknolojia; tunapishana na wenzetu kwa sababu tunataka tukimbie, tunataka tufike mahali tuendane na dunia. Waswahili wanasema, ukitaka umsaidie mtu usimpe samaki, mfundishe kuvua aende baharini kwa sababu utakuwa umetengeneza milo ya muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuzipata hizi fedha imeonekana ufanisi wetu ni mdogo. Tunashukuru taasisi yetu ya *NEMC* ilishakuwa na ithibati kupitia *Adaptation Fund* na ikawa hadi sasa kuanzia 2017 imeshatupatia shilingi bilioni 26 za Kitanzania kupitia ufadhili huu.

Mheshimiwa Spika, ipo pia *CRDB* nayo ina ithibati kupitia Mfuko wa *GCF (Global Climate Fund),* na mpaka leo tumeshapata shilingi bilioni 260 kwenye miradi hii ya kijani kibichi. Sasa kwa sababu ya ufanisi mdogo, taasisi hii ikitujengea uwezo tutakimbia haraka. Yapo manufaa yamepatikana katika nchi jirani, ikiwemo nchi ya Uganda, ambayo miaka ya 2018 mpaka 2023 wao wameweza kupata shilingi bilioni 144 kupitia mifuko hii kwa kuwa wao wameanza kuchangamka mapema. Hata nchi ya Rwanda mwaka 2022 wamefaidika kwa kupata shilingi bilioni 85.8.

Mheshimiwa Spika, sasa hata kama ni kipofu, lakini ukisikia maelezo haya yenye udhibitisho, yanakutosha kushawishika...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante, mengine unaweza kumwandikia Mheshimiwa Waziri.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Ulenge, jiandae Mheshimiwa Mwinyi Ramadhani.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia katika Mkutano huu wa Nne wa Kikao cha Saba cha Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye Enzi na Utukufu, ambaye ametujalia kuweza kukutana asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, niseme kwamba ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, na ninaomba

kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuunga mkono hoja hii ya kuridhia Tanzania kujiunga na shirika au taasisi ya ukuzaji kijani duniani kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa mujibu wa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, inaonekana wazi uhalisia wa taasisi hii siyo wa kutiliwa mashaka, kwa maana *authenticity of GGGI is not questionable*. Nchi nyingi za Afrika zimeshajiunga, na nchi 15 ziko mbioni kujiunga, na hata Jumuiya ya Ulaya iko mbioni kujiunga.

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu walivyotangulia kuzungumza, nchi hizo za Afrika Mashariki zimenufaika, lakini siyo tu kunufaika kama mkopo, hizi fedha ni *grant*. Hizi fedha baadhi yake siyo mkopo, kama ile shilingi bilioni 260 aliyoipata *CRDB,* shilingi bilioni 52 ni *grant*, siyo mkopo. Kwa maana hiyo kuna fedha zimekaa tu mahali fulani, tunaweza kuzipata kwa sisi kujiunga na taasisi hii ya *GGGI*. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono jambo hili kwa manufaa endelevu ya mabadiliko ya tabianchi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niseme kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusimamia nishati safi ya kupikia siyo tu amejali afya za wanawake wa Tanzania, lakini vilevile ameonesha kujali mazingira. Kwa mantiki hiyo, kuunga mkono jambo hili ni kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha Taifa letu linakuwa imara katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, linakuwa imara katika kuwa himilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono hoja na turidhie nchi yetu ijiunge na *GGGI* ili tupate tu hizi fedha ambazo zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiuhalisia katika mazingira kuna fedha nyingi mno ambazo watu katika nchi mbalimbali wanazipata, lakini sisi kwa sababu ya kutokuwa na ithibati na uwezo mahiri wa kuandika maandiko ya miradi ili tuweze kupata ithibati na kuidhinishwa ili tuweze kupata fedha hizo, mara zote tumekuwa

hatuzipati. Tunatamani sisi kama Taifa tuweze kula keki hii ya dunia ambapo yapo mashirika yanayojitolea na kukusanya fedha hizi kwa ajili ya masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu linahitaji fedha ili kutekeleza mikakati, mipango na programu mbalimbali za uhifadhi wa mazingira. Kwa mfano, Tanzania inahitaji shilingi trilioni 97.8 kwa ajili ya mpango wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Tanzania inahitaji shilingi trilioni 128.5 kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, tunahitaji shilingi trilioni 7.2 kwa ajili ya programu ya mageuzi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu sasa ya kujiunga na taasisi hii ili kuwa miongoni mwa Mataifa yanayonufaika na mpango huu wa kupata fedha hizi ambazo zimekaa tu *somewhere*. Wenzetu wananufaika na kula fedha hizi, lakini sisi Tanzania tumechelewa kufaidika. Ni wakati sahihi sasa kama Taifa tuingie na kujiunga na *GGGI* ili tule keki ya dunia kama nchi nyingine wanavyokula.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhani, wajiandae Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Patali Patali.

MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN: Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia neema ya uhai na afya njema.

Mheshimiwa Spika, pili nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho lake zuri. Kwanza ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tumejiridhisha kuwa nchi yetu ina haki na wajibu kabisa kujiunga na taasisi hii ya *GGGI* kwa sababu tuna jukumu kubwa la kuilinda nchi yetu kwenye mazingira, na hasa tunapoelekea sasa hivi katika mwelekeo wa biashara ya kaboni au hewa ya ukaa, ili Taifa hili liweze kupiga hatua, tuwe na

mazingira sahihi, tuweze kuungana na kazi na heshima kubwa ambayo ameileta Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuridhiwa kwa mkataba huu kutaleta heshima sana kwa nchi yetu, kwa sababu nchi za wenzetu takribani 52 zimeshajiunga katika mkataba huu. Sisi Tanzania tukichelewa, na kwa sababu ya kasi yetu ya maendeleo, itakuwa tunairudisha nyuma nchi yetu. Bado takribani nchi 20 sasa zimeomba maombi ya kujiunga na taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi Tanzania kwa sababu tuna umuhimu wa kufanya kazi hiyo, na nchi yetu inaelekea katika kukuza mazingira na kuipa nguvu sana taasisi yetu ya *NEMC* na Wizara na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira ili iweze kufanya kazi yake na kwa sababu sisi wananchi tuna deni la kulinda mazingira ili kupata hewa safi na kupata mazingira bora na kutunza vyanzo vyetu vya maji na kuiheshimisha nchi yetu, ni lazima tupate.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa taasisi hii inaongeza nchi yetu kupata nguvu kwa sababu tutapata washauri kutoka kwenye taasisi hii, na kupata fedha katika kusaidia taasisi mbalimbali. Tukijiunga na Mkataba huu, tutapata mambo muhimu sana yatakayoweza kusaidia nchi yetu na taasisi zetu za ndani. Taasisi hii ina uwezo wa kutosha na ina wataalamu wa kutosha. Kwa hiyo, kwetu sisi Tanzania kujiunga, kuna manufaa makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninatumia nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako kuunga mkono hoja hii ili tuweze kuridhia mkataba huu, tuweze kupata mafanikio makubwa ya nchi yetu na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Pindi Chana, ajiandae Mheshimiwa Patali Patali.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. Nipongeze sana uwasilishaji wa Mheshimiwa Waziri pamoja na maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu, *Agreement on the Establishment of Global Green Growth Institute* ni muhimu. Mkataba huu unasema ni *Global Green Growth,* yaani Mkataba ambao unahusisha dunia nzima *(global)* katika uanzishaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi sana tuliotoka Mikoa ya Njombe, Iringa na Nyanda za Juu Kusini ni watu wa kilimo. Tunapoongelea uchumi wa kijani, huu mkataba ni moja ya vitendea kazi ambavyo vitatusaidia katika masuala ya tafiti, kuandika miradi mbalimbali na kupata fedha kwa Watanzania wengi waliojikita kwenye kilimo, takribani 65% ya Watanzania kutokana na idadi ya watu wapo kwenye masuala ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kule Njombe tumejikita katika kilimo, miti, parachichi, misitu na mbao. Kwa hiyo, mkataba huu kwa kweli ni mkataba muhimu, utatupa faida za kijamii, faida za kiuchumi na za ajira. Ikumbukwe kwamba, katika nchi yetu 55% ya Tanzania ni misitu. Pia, ikumbukwe kwamba, Tanzania ina takribani hekta milioni 48 za misitu. Misitu hii lazima tuilinde, lakini pia tufanye tafiti namna gani ya kuilinda na kuiendeleza ili ituletee mvua na ituletee biashara za kiuchumi kama mbao na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakapokuwa sehemu ya mkataba huu, baada ya kusaini tunakuwa *part of the treaty*. Pia, sisi Tanzania chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumeendelea kuwa sehemu ya mikataba mbalimbali nchini kwa ile sera ya kutofungamana na upande wowote. Kwa hiyo, mkataba huu utakuwa na faida nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kusema ili iingie kwenye *Hansard* vizuri. Baada ya kusaini, isiwe tu kwamba tunasaini, ni lazima tutege faida, lazima tuchote faida ambazo tutanufaika na na *treaty* hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano, tunapozungumza utafiti, tunavyo vyuo kama *Sokoine University,* wao ni *specialist* wa *agriculture*. Tunao vijana wasomi Olmotonyi, vyuo vyetu vya *FITI* na *FWITC*. Hawa wote wanaweza pia kuwa *volunteers, headquarters* za *Global Green Growth Institute*.

Mheshimiwa Spika, lazima tupeleke vijana wetu wakaone kweli Tanzania tuna uwezo wa kufanya hizi kazi. Tu-*volunteer* na idadi kubwa hii ya Watanzania isiyopungua watu takribani milioni 61, kila siku wana-*graduate* vizuri kabisa. Tupeleke *volunteers,* tupate hizo fedha kupitia benki zetu za masuala ya *carbon credit* na pia tuendelee kufanya ile miradi ya *carbon credit*. Kwa eneo hili kubwa la misitu lazima halmashauri ziendelee kunufaika na masuala ya *carbon credit*. Kwa hiyo, ninaendelea kutoa wito kwa Wizara kuhusu miradi ya *carbon credit*. Halmashauri nyingi zimekuwa zikiomba, zina maeneo ya misitu. Tunaomba tuingie mikataba ya *carbon credit* kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wataalamu wafike kwenye hizi halmashauri na vikao vya *ALAT* watoe elimu ili halmashauri zianze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, halmashauri hizi zinatunza sana hii misitu. Hifadhi zetu hizi zinatunzwa sana. Tunazo hifadhi zisizopungua 21 chini ya *Tanzania National Parks*. Maeneo ambayo watu hawaweki mifugo ya nyuki, hawaweki masuala mbalimbali, ule ni uhifadhi. Sasa tunapohifadhi bila kunufaika na miradi ya *carbon credit,* sisi wenyewe tunakuwa tunajipunja.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika tusaini mkataba huu, tuwe sehemu ya hii *treaty* na tupate huo utaalamu, wataalamu waje tuingie hiyo mikataba na tupate hizo fedha ambazo wamesema tutanufaika. Kwa hiyo, ninaunga mkono hoja lakini pamoja na kuwa sehemu, ni vizuri tuka-*make sure* tunanufaika na huu mkataba.

Mheshimiwa Spika, tunaridhia mikataba mingine kwa kuweka *reservation* kwamba kifungu hiki na hiki tunaridhia, kasoro hiki kutokana na *tradition* na *culture* zetu. Japo kutokana na

maoni ya Kamati ya *treaty* hii, Kamati inasema turidhie vifungu vyote bila *reservation*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, ahsante.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Patali, halafu Mtoa hoja, ajiandae.

MHE. PATALI S. PATALI: Mheshimiwa Spika, kwa heshima ninaomba nichukue fursa hii kwanza kabisa kuipongeza Serikali, kupitia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada kubwa sana hasa katika kupambana na kukabiliana na haya mabadiliko ya tabianchi. Vivyo hivyo, ninaipongeza Wizara kwa kuja na jambo hili. Mimi ni sehemu ya hii Kamati ya Maji na Mazingira ambaye nimepata fursa ya kupitia na kulichakata vizuri hili jambo. Kwa hiyo, ninaamini nitakachokishauri hapa kitakuwa na msingi mzuri kwa sababu nimekuwa sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tukubaliane kwamba *talk of the globe* kwa sasa ni mabadiliko ya tabianchi. Kuna *reference* mbalimbali, kuna kuongezeka kwa joto duniani. Mataifa kama *Syria, Norway, Spain* na nchi nyingine za Ulaya sasa hivi zina-*suffer* kwa sababu ya *global warming*.

Mheshimiwa Spika, hata hivi karibuni tumeona kwenye vyombo vya Habari, Taifa kama Nepal, wameingia kwenye janga kubwa la mafuriko makubwa kutokana na barafu kuyeyuka na ikaangamiza watu wengi sana. Haya yote ni mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, hata sisi kama nchi, hatujabaki salama. Kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini *TMA*, hivi karibuni tumetangaziwa kwamba tutakuwa na vipindi vya *El-Nino*, na ni vipindi tishio. Haya yote ni mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwa Wabunge wote na wananchi wanaotusikiliza, tulichukulie suala hili la kujiunga na hii taasisi ya *GGGI,* kwani ni jitihada za Serikali kuhakikisha inawaweka wananchi wake salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwa kujiunga na yale tuliyoyaona kwenye mkataba huu kuna mambo mengi sana. Lengo la Serikali ni kuwaweka salama wakulima wa viazi kule Mbeya Vijijini, Ilungu, Santilya, pamoja na Igoma; lengo la Serikali kupitia mkataba huu, ni kuwaweka salama wakulima wa pareto kulinda ardhi yao kule Mbeya Vijijini; lengo la Serikali ni kuwaweka salama wavuvi wa samaki katika Ziwa Rukwa kule kwa kaka yangu Mheshimiwa Mulugo, ukizingatia sasa hivi hakuna samaki kwa sababu tu ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumze kwa kifupi. Wenzangu wamezungumza mambo mengi sana ya umuhimu wa mkataba huu. Ila kuna jambo moja kubwa ambalo hatujalizungumzia, ni kuhusu kupata fursa ya ushawishi wa kidiplomasia kwenye masuala ya mazingira duniani. Tunafahamu na wenzangu wamesema, ili upate fursa mbalimbali, huu mkataba unatupa fursa ya ku-*mobilize funds* zile zinazokuja kama kichocheo cha kukabiliana na hali ya mazingira duniani, lakini lazima uwe na ushawishi.

Mheshimiwa Spika, kupitia mkataba huu, hayo ndiyo mambo tunayokwenda kunufaika nayo. Pia, tunaenda kupata uzoefu mkubwa wa namna ya kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, ambayo tayari yameshayapata Mataifa mengine. Vilevile, wataalamu wetu wanaenda kujipatia uzoefu kwa sababu pia wanaenda kukopa uzoefu kutoka kwenye Mataifa mengine, kujua wanatumia mbinu gani kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa yale yaliyomo kwenye Mkataba huu, lakini lipo jambo moja zuri zaidi. Mikataba yote hii ambayo sisi kama Wabunge tunawajibika kuishauri Serikali, kuna jambo moja ambalo lazima tuliangalie kwa jicho la tatu. Mkataba huu unatupa fursa, pale ambapo tutaona kama

Taifa hakuna sababu ya kuendelea nao, ndani ya miezi sita kumwandikia Mkurugenzi Mkuu na *automatically* tunakuwa tumejitoa. Hilo tumeliona, tumelitazama na hili linatutaarifu kwamba Mkataba huu ni salama kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusiache kushauri. Kuna mambo ya msingi ya kuyazingatia. Ushauri wangu wa kwanza, kuna haja ya Serikali kuendelea kufanya *monitoring* baada ya kujiunga kwenye huu mkataba.

Mheshimiwa Spika, tukishakuwa wanachama tayari wa huu Mkataba, kuna mabadiliko ambayo yataendelea kufanyika. Sasa yale mabadiliko lazima Serikali iyaone kila siku tayari tukiwa wanachama, kama mabadiliko hayo yatakuwa na tija kwa Taifa. Kama hayatakuwa na tija, tutumie Kifungu cha Ibara ya 20 ambacho kinaturuhusu sisi kujitoa baada ya miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie jambo lingine. Tunajiunga na Mkataba huu kwa sababu tuna matarajio makubwa. Ni jukumu la Serikali kuendelea kufuatilia endapo Serikali imepata yale tuliyokuwa tunayatarajia tukiwa kwenye Mkataba huu na kama hatujayapata au kutakuwa hakuna yale ambayo tunayatarajia, basi kuna sababu za msingi za sisi kujitathmini upya kuendelea kuwepo kwenye Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa mara nyingine tena, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mtoa hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. Kwanza, ninaomba nichukue nafasi hii kuishukuru na kuipongeza Kamati chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Gedion Kiswaga, kwa taarifa ambayo waliiwasilisha hapa, na maoni mazuri ambayo tumeyapokea, lakini kimsingi jinsi ambavyo wameweza kutuunga mkono katika kuliwasilisha azimio hili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuzungumza kwa niaba ya Wabunge wote, ambao ni dhahiri maoni ya Waheshimiwa Wabunge hawa yanaakisi mitazamo ya Waheshimiwa Wabunge wengine ambao hawakupata nafasi ya kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka ninaomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hapa leo. Nikianza na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kiswaga ambaye aliwasilisha taarifa kwa umahiri na umakini wa hali ya juu kabisa. Pia, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti Prof. Yanda, Mheshimiwa Singano, Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa Mwinyi, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana na Mheshimiwa Patali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi ambavyo maoni haya yalivyowasilishwa, ni dhahiri kwamba Waheshimiwa Wabunge wanaunga mkono Serikali juu ya umuhimu wa kuwasilisha Azimio hili hapa Bungeni na kwamba sasa huu ndiyo wakati mwafaka wa kuwasilisha na kulipitisha Azimio hili. Wameeleza faida nyingi sana, ambazo kama Taifa tutafaidika nazo, kupitia kuridhiwa kwa azimio hili.

Mheshimiwa Spika, mengi ya faida yamezungumzwa. Ninataka niungane na Waheshimiwa Wabunge kwamba, msingi wa maendeleo ya nchi yetu unakwenda sambamba na mwongozo ama Dira yetu ya Mwaka 2050. Katika nguzo kuu tatu za Dira ile, nguzo moja inahusu masuala ya uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba na Dira yetu ya Mwaka 2050, Ofisi ya Makamu wa Rais imeamua kuchukua hatua madhubuti. Miongoni mwa hatua kubwa na za msingi ambazo tumechukua, ni kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya mazingira nchini, hususan kwenye taasisi zetu mbili muhimu sana ambazo ndizo zimepewa majukumu ya moja kwa moja ya kutekeleza shughuli za mazingira ama zinagusa mazingira katika nchi yetu. Taasisi hizo kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mnafahamu, ni Taasisi ya

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, na Taasisi ya Kituo cha Kuratibu Biashara ya Hewa Ukaa.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba umuhimu wa kufanya mageuzi makubwa na mapana kwenye taasisi hizo, yanakwenda sambamba na hali halisi ya baadhi ya changamoto ambazo zipo kwenye sekta za mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kwa mfano, ninyi ni mashahidi, mmeshuhudia kwamba bado kuna changamoto mbalimbali za kimazingira katika nchi yetu ambazo zinahitaji chombo cha *NEMC* kuwa ni chombo imara zaidi na chenye meno ya kuweza kusaidia kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza, juu ya umuhimu wa kutumia fursa ya biashara ya hewa ukaa ambayo imeshamiri sasa hivi duniani kwa kuhakikisha kwamba tunakiimarisha kituo chetu cha *NCMC* cha kuratibu biashara hii ya hewa ukaa, ili kiweze kutimiza malengo ya Serikali ya kuhakikisha kwamba tunatumia fursa zote za kwenye biashara ya hewa ukaa kuweza kusaidia kupunguza athari ya hewa ukaa katika nchi yetu. Vilevile, kuhakikisha kwamba tunasaidia kuongeza kipato katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa hiyo inakwenda sambamba na mabadiliko mbalimbali ya kisheria na mabadiliko ya kitaasisi ambayo yanakwenda kuhakikisha kwamba sasa tunakuwa na vyombo vyetu hivi viwili ama taasisi hizi mbili zitakazokuwa na mifumo mizuri ya kisasa na miundo mizuri ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hivi karibuni utakumbuka, tumezindua mfumo wa kufuatilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira nchini unaoitwa *TOCEMS* kupitia Taasisi yetu ya *NEMC*, ambao utasaidia sana kuweza kubaini kwa haraka na kwa wakati huo huo uharibifu wa mazingira popote pale nchini na kuchukua hatua kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, hii inakwenda sambamba na kuimarisha uwezo, lakini kubwa zaidi ni eneo ambalo linahusu mikakati na mipango ambayo itasaidia kutuelekeza katika kukamilisha malengo hayo.

Mheshimiwa Spika, pia, ninataka nigusie, mikakati hiyo na malengo hayo ya kiserikali yanahitaji fedha nyingi. Nitoe mfano wa maeneo matatu; tuna mkakati ama Mpango wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi, ambao unagharimu zaidi ya shilingi trilioni 97.8. Huu ni mkakati wa kuanzia mwaka 2025 mpaka mwaka 2035 ambapo ni mkakati wa miaka 10.

Mheshimiwa Spika, tuna mkakati wa miaka mitano wa mageuzi ya usimamizi wa mazingira endelevu. Wenyewe unagharimu takribani shilingi trilioni 7.2. Vilevile, tuna mpango wa tatu ama *ND III* ambao ni Mpango wa Mchango wa Nchi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi. Wenyewe unagharimu karibu shilingi trilioni 128.5. Hizi ni fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, sisi hatutarajii fedha hizi zote zitoke kutokana na Bajeti ya Serikali. Ndiyo maana tunasema kwamba fursa yoyote inayoweza kutusaidia kupata fedha hatutaiacha. Kujiunga kwa Tanzania katika *GGGI,* ni moja kati ya fursa muhimu na adhimu ya kusaidia mipango ya Serikali niliyoitaja ili iweze kutekelezeka. Mipango hii ni muhimu sana katika kukabiliana na changamoto za mazingira ukilinganisha na mikakati mingine ya mageuzi niliyoizungumza hapo kabla.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachukua fursa hii, kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuliona hilo. Sisi tutatumia nafasi hii ya kupitisha Azimio hili kuhakikisha tunaiwezesha nchi yetu kunufaika ipasavyo na fursa mbalimbali kama ambavyo nchi nyingine nyingi zilizojiunga zimeweza kufaidika na fursa nyingi sana katika taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, labda nianze kutaja fursa ambazo tunadhani ni za muhimu sana sisi kuanza nazo pindi ambapo nchi yetu itakuwa imejiunga na taasisi hii. Moja katika changamoto ambayo inatukabili sasa hivi kama Taifa, ambayo imekuwa

ikitukosesha fursa za fedha nyingi sana katika mifuko ya Kimataifa, ni uwezo wa taasisi zetu za ndani kupata ithibati.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna taasisi nyingi sana ambazo nyingine zina zaidi ya hata miaka minane zimeomba kupata ithibati kutoka kwenye mifuko ya fedha ambayo iko zaidi ya 60 ili iweze kusimamia fedha. Kama ambavyo mnajua mifuko hii haitoi fedha bila kupitia kwenye taasisi zilizopata ithibati nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano leo hii, Benki ya *NMB,* Benki ya *TADB, NBC,* hata Wizara ya Fedha yenyewe na *COSTECH,* ni miongoni mwa taasisi ambazo zimekwama kupata ithibati kwa muda mrefu. Kuingia kwetu kwenye taasisi ya *GGGI* kutatusaidia kuimarisha uwezo wa taasisi zetu za ndani na kuongoza kuweza kupata ithibati.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa taasisi ambazo zimepata ithibati nchini ni mbili; *CRDB* ambayo imepata ithibati ya fedha kidogo, Dola milioni 110 tu kutoka Mfuko wa *GCF (Global Climate Finance)* na Taasisi ya *NEMC* ambayo yenyewe imepata Dola za Kimarekani milioni 10 tu kutoka Mfuko wa *AF (Adaptation Fund),* ambapo kati ya hizo shilingi milioni 30 ni *grants*.

Mheshimiwa Spika, mtaona tuna ombwe kubwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, malizia...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, tuna upungufu na changamoto kubwa katika hili. Hivyo tunahitaji kujiunga katika taasisi hii ili tuweze kujenga uwezo wa taasisi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninataka nimalizie kwa jambo moja, kwamba ni muhimu Waheshimiwa Wabunge na wananchi wakafahamu kwamba kuna nchi ambazo zimefaidika vya kutosha na fedha nyingi sana. Nitoe mfano wa nchi mbili. Kwa mfano, India imefanikiwa kupata karibu Dola bilioni 1.38 za

Kimarekani baada ya kujiunga na taasisi hii. Pia, imesaidia taasisi za nchi hiyo kuweza kujengewa uwezo na kupata ithibati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nchi nyingine ambazo zimepata fedha nyingi kwa Afrika, kuna Nchi ya Ethiopia, ambayo imepata fedha zaidi ya dola milioni 77.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, fursa za kujiunga na taasisi hii ni pana sana kwa maeneo mengi; kujengewa uwezo, kusaidia ajira katika nchi yetu, kusaidia kupata ithibati na kusaidia kupata fedha zitakazotusaidia katika kutatua changamoto za mazingira katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa sasa nitawahoji, kuhusu Azimio la Bunge kuhusu kuridhia Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani *(Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute)*.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Bunge la Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani (Agreement on the Establishment of the Global Green Growth Institute) liliridhiwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda, na sasa hili ni Azimio la Bunge. Kwa hiyo, Serikali itaendelea na hatua zinazofuata. *(Makofi)*

Ninawapongeza Kamati na Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri mlizofanya. Endeleeni kusimamia mazingira na mhakikishe kuwa nchi iko salama kwenye masuala ya mazingira.

Katibu.

Hapa Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu wa Bunge

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. CECILIA D. PARESSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na afya njema aliyotujalia siku ya leo. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, ninaomba nichukue fursa hii kuanza na maneno ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii kwa dhati kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuaminiwa na Watanzania na kuchaguliwa kwa kura za ushindi, kishindo, na heshima kubwa katika Uchaguzi Mkuu uliopita. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia katika historia ya nchi yetu na kuwa Rais wa kwanza Mwanamke kwa kuchaguliwa kupitia sanduku la kura, na anakuwa Rais wa kwanza Mwanamke katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika, mtakubaliana nami kuwa historia imemtambua, itamkumbuka, na jina lake litaandikwa kwa wino wa dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tumeshuhudia kupitia uongozi wake, amani, utulivu, na mshikamano vimeendelea kuimarishwa, na pia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo

inaendelea kufanyika. Tunamshukuru na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na huu ni uthibitisho kuwa wanawake wakipewa nafasi ya uongozi wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu azidi kumpa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan maarifa, busara, uvumilivu, hekima na nguvu ya kuendelea kutuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi hii pia nimpongeze Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uteuzi wake ni uthibitisho kuwa Mheshimiwa Rais ameendelea kuamini vijana katika uongozi wake na kuweka historia nyingine ya kuwa na Makamu wa Rais kijana toka tumepata uhuru wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza mchumi mbobezi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa msaidizi wake kwa nafasi ya Waziri Mkuu. Huu ni uthibitisho mwingine kuwa Mheshimiwa Rais anaendelea kuamini vijana katika Serikali anayoiongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa namna ya kipekee nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake imara na thabiti katika kuliongoza Bunge hili. Pia nikupongeze wewe, Mheshimiwa Naibu Spika, Daniel Baran Sillo, kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Spika kuliongoza Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii ndiyo zana kuu inayoliwezesha Bunge kutekeleza jukumu lake katika udhibiti wa sheria ndogo nchini na kuliweka katika nafasi stahiki ya kusimamia

madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu wa Bunge, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, iliweka Mezani nakala za matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake kwa mujibu wa Kanuni ya 46, Kanuni Ndogo ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2025. Hatua hiyo ni sehemu ya utaratibu wa Bunge unaohusu kuingiza nyaraka katika mchakato wa Kibunge kwa madhumuni ya kumbukumbu rasmi, taarifa, uchambuzi, na pale inapohitajika, hatua zaidi za Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kanuni ya 46(8) ya Kanuni za Bunge, imeweka sharti kwamba taarifa ambazo sheria inaelekeza ziwasilishwe Bungeni, ikiwemo matoleo ya Gazeti la Serikali na nyongeza zake, zikijumuisha sheria ndogo, zitajadiliwa na Kamati inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo na muundo wa taarifa. Taarifa hii inahusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu. Lengo ni kuliwezesha Bunge kutekeleza kwa ufanisi jukumu lake la udhibiti wa mamlaka ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza imeweka msingi wa taarifa kwa kueleza madhumuni, mawanda, majukumu ya Kamati, na mbinu zilizotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili inaeleza misingi ya kisheria na ya kiuchambuzi iliyotumika na kuwasilisha matokeo yaliyobainika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu inabainisha maoni ya Kamati kuhusu matokeo ya uchambuzi na mapendekezo kwa

muundo wa Maazimio ili Bunge likiyapitisha yawe Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni na mawanda ya uchambuzi. Kwa madhumuni ya uchambuzi uliofanywa na Kamati ni kuliwezesha Bunge kutekeleza kwa ufanisi jukumu lake la udhibiti wa kibunge wa sheria ndogo kwa kujiridhisha iwapo madaraka yaliyokasimiwa na Bunge kwa mamlaka mbalimbali yametumika ndani ya mipaka iliyowekwa, hayakinzani na Katiba, sheria mama, na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni hayo, mawanda ya uchambuzi yalihusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu. Uchambuzi wake ulijumuisha ulinganisho na Katiba ya nchi, sheria mama, na sheria nyingine za nchi. Aidha, misingi ya uandishi bora wa sheria na uhalisia katika utekelezaji wake ulizingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbinu na mchakato wa uchambuzi. Taarifa imebainisha mbinu na mchakato kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, kama vile:-

(i) Kufanya ziara pale ilipohitajika ili kupata ushahidi wa ziada, kujionea mazingira ya utekelezaji, na kujiridhisha kuhusu hoja zilizobainika kulingana na muktadha halisi;

(ii) Kupokea na kusikiliza maoni ya wadau wa Sheria Ndogo ilipobidi ili kupata mtazamo wa kiutendaji, uzoefu wa utekelezaji wa masharti yanayohusika, pamoja na kubaini athari zake kwa wadau na wananchi kwa ujumla;

(iii) Uchambuzi wa kina ambao ni uchunguzi wa kimsingi uliolenga kuchunguza kwa undani uhalali, uhalisia, madhumuni na athari za masharti yaliyobainika; na

(iv) Mashauriano na mamlaka zilizohusika na Sheria Ndogo ili kupata maelezo yao kuhusu hoja za kiuchambuzi

zilizobainika kwa madhumuni ya kuiwezesha Kamati kujiridhisha kuhusu masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii ya taarifa inaeleza misingi ya uchambuzi wa sheria ndogo, maana na nafasi ya sheria ndogo katika mfumo wa sheria za nchi, na madaraka ya Bunge ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muhtasari, ninaomba nieleze yafuatayo:-

(i) Kamati ilichambua Sheria Ndogo kwa kuzingatia misingi ya kisheria, mipaka ya mamlaka, ulinganifu na sheria mama na athari zake katika utekelezaji wa sheria. Uchambuzi huu unatambua kuwa Sheria Ndogo ni nyenzo muhimu za kuwezesha utekelezaji wa sheria mama na zina athari za moja kwa moja kwa wananchi. Kwa msingi huo, Bunge linapaswa kuzichambua ili kulinda uhalali wa kisheria, maslahi ya umma, na uwajibikaji wa Serikali;

(ii) Kifungu cha Nne cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinafafanua Sheria Ndogo kuwa ni pamoja na Kanuni, Amri, Notisi na Hati zinazotokana na mamlaka ya kisheria. Aidha, Kifungu cha 41(1) kinaonyesha kuwa Sheria Ndogo ni sehemu ya mfumo wa sheria mama. Kadhalika, Kifungu cha 42 kinasisitiza kwamba kitendo kinachofanyika chini ya Sheria Ndogo kinachukuliwa kuwa kimefanyika chini ya sheria mama;

(iii) Sheria Ndogo huathiri moja kwa moja utekelezaji wa Sheria za Bunge na maisha ya wananchi. Aidha, zinapaswa kuwezesha utekelezaji wa sheria mama lakini hazipaswi kubadilisha au kupanua sheria mama;

(iv) Ibara ya 64(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria. Wakati Ibara ya 97(5) inaliruhusu Bunge kukasimu kwa mtu au mamlaka nyingine uwezo wa kutunga Sheria

Ndogo ndani ya mipaka iliyowekwa na Bunge. Hata hivyo, kukasimu mamlaka hakumaanishi kukabidhi mamlaka bila mipaka;

(v) Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinataka Sheria Ndogo kuwasilishwa Bungeni, sharti hili linawezesha Bunge kudhibiti mamlaka iliyokasimiwa;

(vi) Mamlaka iliyokasimiwa haipaswi kujiongezea madaraka kupitia Sheria Ndogo wala kuweka masharti yanayokinzana na Katiba au sheria mama. Kwa msingi huo, uchambuzi wa Sheria Ndogo ni kinga ya mamlaka ya Bunge;

(vii) Kukasimu mamlaka hakufuti wajibu wa Bunge wa kusimamia utekelezaji wake. Bali Bunge linapaswa kufuatilia na kusimamia matumizi ya mamlaka hayo ili yatumike kwa uhalali, ndani ya mipaka na kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu. Jumla ya Sheria Ndogo 33 zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu, zilichambuliwa kama inavyoonekana katika majedwali, kiambatanisho namba moja na kiambatanisho namba mbili, ambayo ni sehemu ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia vigezo sita ambavyo ni mamlaka, uhalali, ulinganifu, utekelezaji, uandishi, na usahihi. Vigezo hivyo vilihusika kujibu maswali muhimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Sheria Ndogo imetungwa kwa mamlaka gani? Ina msingi gani wa kisheria? Inaendana na Katiba na sheria mama au sheria nyingine za nchi? Inatekelezeka? Je, imeandikwa kwa usahihi? Vigezo na maswali hayo viliwezesha Kamati kutenganisha kasoro za kisheria, kiutaratibu na kiutendaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi. Uchambuzi umebaini maeneo yaliyohitajika kufanyiwa marekebisho na kuyaweka katika makundi makuu matatu. Makundi hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Baadhi ya Sheria Ndogo zimeweka masharti yanayokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi;

(ii) Baadhi ya Sheria Ndogo hazijazingatia misingi ya uandishi wa sheria; na

(iii) Baadhi zimeweka masharti ambayo hayaendani na uhalisia wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufafanuzi wa maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Ndogo kukiuka masharti ya sheria mama au sheria nyingine. Dosari ya kukiuka sheria mama hutokea Sheria Ndogo inapoweka masharti yanayozidi, kubadilisha au kupingana na mamlaka yaliyotolewa na sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinakataza Sheria Ndogo kuwa na masharti yanayokinzana na sheria iliyotoa mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni Kanuni zinazoitwa *The Civil Aviation Regulation, 2026*. Kanuni ya 61 inaweka faini isiyozidi shilingi 1,000,000 au kifungo kisichozidi miezi sita, lakini sheria mama, kwa maana ya Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80, imeweka faini isiyopungua Dola 1,000 au kifungo kisichopungua miezi 12. Kwa maelezo haya, Sheria Ndogo imepunguza adhabu iliyowekwa na Bunge, ambayo ni kinyume na mamlaka yaliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria. Dosari ya kiuandishi hutokea masharti ya Sheria Ndogo yanapoandikwa bila uwazi, usahihi, mantiki na kuleta utata unaoweza kuathiri maana, tafsiri au utekelezaji wake. Kwa mfano, katika Kanuni ziitwazo *The Banking and Financial Institution Regulation, 2025*, Kanuni ya 10(3) ina sentensi isiyokamilika inayoweza kuleta tafsiri nyingine na kuathiri uhakika wa sheria. Aidha, katika *The Transport Licensing Regulation, 2025,* Jedwali la Tatu lina fomu inayorejea Kanuni ya 22(2) ambayo haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Ndogo kuweka masharti yasiyo na uhalisia. Dosari ya kutokuwa na uhalisia hutokea Sheria Ndogo inapoweka masharti yasiyotekelezeka katika mazingira halisi au yasiyo na uwiano na uwezo wa rasilimali zilizopo. Mfano katika Kanuni ziitwazo *The Fertilizer Regulation, 2026*, Jedwali la Pili linaweka ada ya Dola 10,000 kwa kila msimu kwa majaribio ya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango hicho kinaweza kuwa mzigo mkubwa kwa wazalishaji wadogo na kikwazo katika uendelezaji wa sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2025. Kifungu cha 10 kinaweka tozo ya asilimia tano ya thamani ya chombo kwa kila siku ambayo mzigo uliokamatwa unashikiliwa. Hali hiyo inazalisha kero kwa wananchi kutokana na kusababisha tozo kubwa kuliko thamani halisi ya mzigo wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano hiyo inaonyesha kuwa uhalali wa kisheria pekee hautoshi, sharti lazima liwe kutekeleza kwa uhalisia, kwa uwiano, na bila kuwa kikwazo kwa madhumuni ya sheria mama. Mamlaka zinazotunga Sheria Ndogo zinapaswa kuzipima kwa mazingira halisi ya utekelezaji, uwezo wa wahusika, na athari zinazoweza kujitokeza ili masharti yatekelezwe kwa ufanisi na kuendeleza madhumuni ya sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, kubainika kwa Sheria Ndogo zenye masharti yanayokinzana na sheria mama, kasoro za kiuandishi, na zenye masharti yasiyo na uhalisia, ni miongoni mwa mambo yanayosisitiza umuhimu wa uchambuzi wa Sheria Ndogo. Dosari hizo zikiendelea kuwepo, bila Bunge kuzibaini, zinaweza kusababisha kero kwa wananchi na kuathiri shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Mapendekezo. Kutokana na uchambuzi wa Sheria Ndogo, sehemu hii inatoa mtazamo wa jumla kuhusu masuala yaliyobainika. Mtazamo huo una sura ya maoni ambayo yanajenga msingi wa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Sheria Ndogo inapovuka mipaka iliyowekwa na Bunge, ni jukumu la Bunge kuhakikisha kwamba mamlaka inayohusika inarekebisha dosari hiyo.

(ii) Mgongano wa kisheria kati ya Sheria Ndogo na Sheria Mama au sheria nyingine za nchi, unadhoofisha madhumuni ya Bunge kukasimu mamlaka yake na kuathiri mfumo wa sheria nchini.

(iii) Sheria Ndogo zenye makosa ya kiuandishi zinakosa uwezo wa kueleweka, kutabirika, na kutekelezeka kwa ufanisi. Ni wajibu wa Bunge kuzifuatilia ili ziweze kutekelezeka.

(iv) Sheria Ndogo zinapokuwa na masharti yasiyotekelezeka, zinageuka kuwa mzigo kwa wananchi na kushindwa kufikia madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge.

(v) Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu marekebisho ya Sheria Ndogo, zinapowasilishwa Bungeni, Bunge litakosa fursa ya kujiridhisha iwapo mamlaka yaliyokasimiwa yanatumika kwa madhumuni, mipaka na masharti stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo. Kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa, sasa ninaomba kuwasilisha mapendekezo ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka ya mamlaka yaliyokasimiwa.

Kwa Kuwa, mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo, yanapokasimiwa na Bunge yanapaswa kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na ndani ya mipaka iliyowekwa na sheria mama au sheria nyingine inayotoa mamlaka hayo;

Na Kwa Kuwa Sheria Ndogo yenye masharti yanayovuka mipaka ya mamlaka yaliyokasimiwa, inaweza kuathiri uhalali wa kisheria, kudhoofisha dhamira ya Bunge kukasimu madaraka ya kutunga sheria kwa mamlaka zinazohusika, na kusababisha mamlaka zinazohusika kutumia madaraka ambayo hayakukusudiwa na Bunge;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zote zinazohusika na Sheria Ndogo zilizobainika kutoka nje ya mamlaka yaliyokusudiwa, kama zinavyoonekana kwenye majedwali ya uchambuzi, zifanyiwe marekebisho stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinganifu wa mfumo wa kisheria.

Kwa Kuwa, Sheria Ndogo zinapaswa kuendana na Sheria Mama pamoja na sheria nyingine za nchi zinazohusika ili kudumisha uhakiki na uelekeo unaofanana katika mfumo wa sheria;

Na Kwa Kuwa Sheria Ndogo yenye masharti yanayokinzana na Sheria Mama au sheria nyingine za nchi inaweza kusababisha mgongano wa kisheria, kuleta tafsiri zinazokinzana, kudhoofisha utekelezaji wa madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge na kuvuruga uthabiti wa mfumo wa sheria nchini;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na masharti

yanayokinzana na Sheria Mama au sheria nyingine za nchi, zifanye marekebisho stahiki ili kuhakikisha kuwa Sheria Ndogo hizo zinaendana na mfumo wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzingatiaji wa misingi ya uandishi wa sheria.

Kwa Kuwa, Sheria Ndogo zinapaswa kuandikwa kwa kuzingatia misingi ya usahihi, uthabiti na ufasaha wa kisheria ili masharti yake yawe yanaeleweka, yanayotabirika na yanayotekelezeka;

Na Kwa Kuwa, Sheria Ndogo zilizo na masharti yenye utata au yasiyoandikwa kwa kuzingatia misingi hiyo inaweza, moja, kusababisha ugumu wa kueleweka na kutafsiriwa; pili, kuleta uelewa na utekelezaji usiofanana miongoni mwa wahusika; na tatu, kudhoofisha utekelezaji wa madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari za kiuandishi zifanye marekebisho stahiki ili kuhakikisha kuwa masharti yake yanaeleweka, yanatafsirika kwa uelekeo unaofanana, na yanatekelezeka kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhalisia na utekelezaji wa masharti.

Kwa Kuwa, Sheria Ndogo zinapaswa kuzingatia mazingira halisi ambayo yanalenga kuyasimamia, pamoja na uwezo wa wahusika na taasisi zinazowajibika kuzitekeleza ili masharti yake yawe yanatekelezeka kwa ufanisi;

Na Kwa Kuwa, Sheria Ndogo zenye masharti yasiyoendana na mazingira halisi ya utekelezaji zinaweza kusababisha ugumu wa utekelezaji na tafsiri, kuweka uelewa usiofanana miongoni mwa wahusika, na kukwamisha madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyoendana na uhalisia wa utekelezaji zifanye marekebisho ili kuhakikisha kuwa masharti hayo yanaendana na mazingira halisi, uwezo wa utekelezaji na madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwajibikaji wa mamlaka zilizokasimiwa.

Kwa Kuwa, ukasimiaji wa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo unaambatana na wajibu wa mamlaka zilizokasimiwa kutumia madaraka hayo kwa mujibu wa sheria mama na kuwajibika kuhusu namna inavyotumika;

Na Kwa Kuwa, Bunge linapobaini dosari katika Sheria Ndogo, mamlaka zinazohusika zinapaswa kuchukua hatua stahiki kuhusu dosari hizo na kutoa mrejesho kwa Bunge ili kuliwezesha kufuatilia na kujiridhisha na mapendekezo yaliyoazimiwa na ili Bunge kutimiza wajibu wake wa udhibiti wa Sheria Ndogo;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zinazohusika na Sheria Ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari kama zilivyoainishwa katika majedwali ambayo ni kiambatanisho kwa taarifa hii, zifanye marekebisho na kuziwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Katibu wa Bunge kabla au ifikapo tarehe 2 Novemba, 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Taarifa hii inaliwezesha Bunge kuhakikisha kuwa Sheria Ndogo zinazotungwa kwa uhalali zinaendana na mfumo wa sheria na zinazingatia uhalisia wa utekelezaji. Ni imani ya Kamati kwamba utekelezaji wa maazimio ya Bunge yanayotokana na mapendekezo ya Kamati utaongeza ubora wa Sheria Ndogo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii kwa mara nyingine kutoa shukrani zangu za dhati kwako, Mheshimiwa Spika wa Bunge, Wenyeviti wenzangu wa Bunge kwa kuweka utaratibu wa Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilisha taarifa hapa Bungeni. Kwa namna ya kipekee ninamshukuru pia Mheshimiwa

Profesa Palamagamba John Aidan Kabudi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kwa kuendelea kuweka uratibu mzuri ambao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, ninawashukuru Mawaziri wote, Manaibu Mawaziri wote na watendaji wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi na kujibu hoja zilizoibuliwa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru wadau wote walioshiriki na kufika mbele ya Kamati kutoa maoni yao kuhusu kanuni za mbolea za mwaka 2026. Ushiriki wao umewezesha Kamati kupata uelewa mpana kuhusu masuala ya mbolea na kuisaidia Kamati kuboresha kanuni hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu wa Bunge na hatimaye kufanikisha kazi hii. Kwa heshima kubwa, ninaomba majina yao yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda kumshukuru kwa dhati Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge, kwa ushirikiano wake wa dhati kwa Kamati hii katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi mkubwa hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali taarifa hii kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu na kupitisha mapendekezo ya Kamati kuwa maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

3 SEPTEMBA, 2026

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KATIKA MKUTANO WA PILI NA MKUTANO WA TATU – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu. Taarifa hii ndiyo zana kuu inayoliwezesha Bunge kutekeleza jukumu lake katika udhibiti wa sheria ndogo nchini na kuliweka katika nafasi stahiki ya kusimamia madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwenye Mkutano wa Pili na Mkutano Tatu wa Bunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge Uratibu na Wenye Ulemavu aliweka Mezani Nakala za Matoleo ya *Gazeti la Serikali* pamoja na Nyongeza zake kwa mujibu wa Kanuni ya 46 (2) ya Kanuni za Bunge za Mwaka 2025. Nyongeza za matoleo hayo ni sheria ndogo zilizopaswa kuwekwa Mezani kwa mujibu wa Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo ni sehemu ya utaratibu wa Bunge inayohusu kuingiza nyaraka katika mchakato wa kibunge kwa madhumuni ya kumbukumbu rasmi, taarifa, uchambuzi na pale inapohitajika, hatua zaidi za kibunge.

Kwa msingi huo, Kanuni ya 46 (8) ya Kanuni za Bunge imeweka sharti kwamba, Taarifa ambazo sheria inaelekeza ziwasilishwe Bungeni ikiwemo matoleo ya *Gazeti la Serikali* na Nyongeza zake zikijumuisha sheria ndogo, zitajadiliwa na Kamati inayohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa fasili ya 10 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati inayohusika na Nyongeza za Matoleo ya Gazeti la Serikali ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Sheria Ndogo. Hivyo, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 46 (9) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanyia kazi ipasavyo sheria ndogo zilizowasilishwa. Katika kazi yake, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni za Bunge ili kuhakikisha kwamba, kazi yake inafanyika kwa utaratibu, uhalali, uwazi, ushirikishwaji na uadilifu wa kibunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha kazi ya uchambuzi wa sheria ndogo, tarehe 21 Agosti, 2026 nilikujulisha kwa maandishi kwa mujibu wa fasili ya 10 fasili ndogo ya 2 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Nakushukuru sana kwa kuelekeza Taarifa hii ipangwe kwenye Orodha ya Shughuli za leo kwa mamlaka uliyonayo chini ya fasili ya 10 fasili ndogo ya 3 ya Nyongeza ya Nane.

Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge. Kwa mgawanyo huo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inayohusu utangulizi inaonesha maelezo ya jumla kuhusu taarifa yenyewe, lengo la Kamati kuripoti Bungeni, mantiki ya Bunge kufuatilia sheria ndogo na mambo mengine ya jumla kuhusu Taarifa ya Kamati;

(b) Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi inafafanua shughuli za uchambuzi na misingi yake pamoja na matokeo ya uchambuzi. Aidha, inaeleza sheria ndogo ambazo zilichambuliwa kwa vigezo vya uchambuzi vinavyobainishwa;

(c) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni ya Kamati kuhusu Matokeo ya Uchambuzi pamoja na Mapendekezo kwa muundo wa maazimio ili Bunge likiyapitisha yawe maazimio ya Bunge. Kadhalika, Sehemu hii inahitimisha Taarifa na kutoa hoja.

Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, fasili ya 10 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimeipa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo, jukumu la msingi la kuchambua sheria ndogo. Uchambuzi huo unalenga

kujiridhisha iwapo sheria ndogo zimezingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria mama inayotoa mamlaka ya kutungwa kwake na sheria nyingine za nchi. Jukumu hili ni sehemu ya utekelezaji wa wajibu wa Bunge wa kudhibiti matumizi ya madaraka ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine.

Madhumuni na Mawanda ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya uchambuzi uliofanywa na Kamati ni kuliwezesha Bunge kutekeleza kwa ufanisi jukumu lake la Udhibiti wa Kibunge wa sheria ndogo, kwa kujiridhisha iwapo madaraka yaliyokasimiwa na Bunge kwa mamlaka mbalimbali yametumika ndani ya mipaka iliyowekwa, hayakinzani na Katiba, sheria mama na sheria nyingine za nchi. Hivyo, lengo la uchambuzi haliishii kutathmini uhalali wa masharti yaliyowekwa, bali pia kuangalia kama masharti hayo yana mantiki ya kisheria, yanaweza kutekelezeka na yanazingatia misingi ya uandishi bora wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni hayo, mawanda ya uchambuzi yalihusisha sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu. Uchambuzi wake ulihusisha ulinganisho na Katiba ya nchi, sheria mama na sheria nyingine za nchi. Aidha, misingi ya uandishi bora wa sheria na uhalisia katika utekelezaji wake ilizingatiwa. Kufanya hivyo ni kuendana na mantiki ya masharti ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria kuhusu sheria ndogo kuwekwa mezani Bungeni.

Mbinu na Mchakato wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, kubainisha njia au mbinu na mchakato wa uchambuzi katika taarifa ya Kamati ni jambo muhimu na msingi wake ni masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge. Njia na mchakato huo unajumuisha:

(a) Uchambuzi wa Awali wa sheria ndogo (*Preliminary Scrutiny*) ambao ulilenga kubaini kwa haraka kama sheria ndogo ina hoja au maeneo yanayohitaji uchunguzi zaidi;

(b) Kufanya ziara pale ilipohitajika ili kupata ushahidi wa ziada, kujionea mazingira ya utekelezaji na kujiridhisha kuhusu hoja zilizobainika kulingana na muktadha halisi;

(c) Kupokea na kusikiliza maoni ya wadau wa sheria ndogo, ilipobidi, ili kupata mtazamo wa kiutendaji, uzoefu wa utekelezaji wa masharti yanayohusika, pamoja na kubaini athari zake kwa wadau na wananchi kwa ujumla;

(d) Uchambuzi wa kina (*Substantive Scrutiny*) ambao ni uchunguzi wa kimsingi uliolenga kuchunguza kwa undani uhalali, uhalisia, madhumuni na athari za masharti yaliyobainika;

(e) Mashauriano na Mamlaka zilizohusika na sheria ndogo ili kupata maelezo yao kuhusu hoja za kiuchambuzi zilizobainika, kwa madhumuni ya kuiwezesha Kamati kujiridhisha kuhusu masuala hayo; na

(f) Kufanya hitimisho la uchambuzi na kuweka msimamo wa Kamati kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi, maoni ya wadau na ufafanuzi uliotolewa na Mamlaka zinazohusika. Hatua hii ndiyo iliyoifikisha Kamati kwenye maandalizi ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, mchakato huu uliiwezesha Kamati kutekeleza jukumu lake kwa hatua madhubuti, kwa umakini na kwa kuzingatia ushahidi. Aidha, mchakato wa shughuli za Kamati, umeifanya Kamati kutoishia kwenye kusoma na kutafsiri masharti ya sheria ndogo bali kuangalia mazingira ya utekelezaji wake na athari zake kadiri ilivyowezekana. Vilevile, uliisaidia Kamati kukusanya ushahidi wa ziada na kusikiliza maoni ya wadau. Hatua hizo, ziliiweka Kamati katika nafasi nzuri ya kupima ufafanuzi uliotolewa na Mamlaka zinazohusika wakati wa mashauriano.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, msimamo wa Kamati ulijengwa kwa kuzingatia sheria, ushahidi, mazingira ya utekelezaji na madhumuni ya sheria ndogo. Hivyo, naomba kulithibitishia Bunge lako tukufu kuwa mapendekezo yanayotolewa katika Taarifa hii ni matokeo ya mchakato madhubuti wa uchambuzi uliolenga kuhakikisha kuwa kila hoja inapata uzito unaostahili

kabla ya Kamati kuweka msimamo wake na kutoa mapendekezo ambayo yakiridhiwa yatakuwa Maazimio ya Bunge.

SEHEMU YA PILI

UCHAMBUZI NA MATOKEO

Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo zilizochambuliwa ni sehemu ya mfumo wa utekelezaji wa sheria na utawala wa nchi. Ingawa zinatokana na mamlaka yaliyokasimiwa kupitia sheria mama, masharti yake yana athari za moja kwa moja kwa Serikali, taasisi na wananchi. Kwa mantiki hiyo, sheria ndogo hizo si jambo la kiutawala pekee, bali ni jambo linalostahili udhibiti na uangalizi wa kibunge ili kuhakikisha kuwa mamlaka yaliyokasimiwa yanatumika ndani ya mipaka na madhumuni yaliyowekwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati ilizichambua sheria ndogo kwa kuzingatia mamlaka ya kisheria yanayozipa uhalali, mipaka ya mamlaka hayo, ulinganifu wake na sheria mama na athari za masharti yake katika utekelezaji wa sheria. Hivyo, sehemu hii inaeleza msingi wa kisheria na vigezo vilivyotumika katika uchambuzi, kabla ya kuwasilisha kwa kina matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu.

Msingi wa Uchambuzi wa Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, msingi wa uchambuzi wa sheria ndogo unaendana na kuzingatia kuwa, sheria hizo haziitwi sheria ndogo kwa sababu ya umuhimu mdogo bali ni kutokana na chimbuko lake. Sheria hizi zinalenga kuwezesha utekelezaji wa sheria iliyotungwa na Bunge. Sheria ndogo ndizo zinazoweka kwa undani taratibu, masharti na mambo mbalimbali yanayohitajika ili sheria mama iweze kutekelezwa ipasavyo. Kwa ujumla, sheria ndogo ni sheria muhimu zinazowaathiri wananchi moja kwa moja na kugusa ustawi wa maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, iwapo Bunge litaishia kutunga Sheria na kusahau dhima yake ya ufuatiliaji na uchambuzi wa sheria ndogo, halitajitoa kwenye mchango wake kwa athari za sheria ndogo kwa Serikali, umma, ustawi wa jamii na wananchi kwa ujumla. Hivyo, kila mchango wa Mbunge katika Taarifa hii ni fursa ya kuongeza mtazamo, kubaini maeneo ambayo yanahitaji msisitizo wa sauti za wananchi kupitia wawakilishi wao na kuifanya Taarifa hii kuwa msingi imara zaidi wa uamuzi na hatua za Bunge.

Maana na Nafasi ya Sheria Ndogo katika Mfumo wa Sheria

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa uchambuzi wa sheria ndogo, unadhihirika kwa kuelewa nafasi yake katika mfumo wa sheria. Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, kinafafanua "sheria ndogo (subsidiary legislation)" kuwa ni pamoja na Amri (Orders), Matamko (Proclamations), Kanuni (Rules), Kanuni za Mahakama (Rules of Court), Kanuni za Wizara (Regulations), Notisi (Notices), Sheria Ndogo za Halmashauri (By-laws) na Hati (Instruments) zilizotokana na Sheria au mamlaka nyingine halali. Kwa hiyo, tofauti ya majina haiondoi ukweli kwamba zote ni aina za sheria zinazotungwa chini ya mamlaka iliyotolewa kupitia sheria ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 41(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinaweka msingi kwamba sheria inaporejea sheria nyingine, kwa ujumla inachukuliwa kuwa inarejea pia sheria ndogo zilizotungwa chini ya sheria inayorejewa. Kifungu hiki kinaonesha kuwa, sheria ndogo ni sehemu ya mfumo mpana kisheria wa kutekeleza sheria mama. Masharti na utekelezaji wake vinaweza kuwa na athari ya moja kwa moja ya kisheria hata kama si sheria iliyotungwa moja kwa moja na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 42 kinaelekeza kuwa kitendo kinachofanyika chini ya sheria ndogo kinachukuliwa kuwa kimefanyika chini ya sheria mama ambayo sheria ndogo hizo zimetungwa chini yake. Hivyo, utekelezaji wa sheria ndogo unaweza kuleta athari za moja kwa moja kwa utekelezaji wa Sheria za Bunge na kwa wananchi, jambo linalozipa sheria ndogo umuhimu wa pekee katika udhibiti na uangalizi wa kibunge.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, sheria ndogo zinapaswa kuwezesha utekelezaji wa madhumuni ya sheria mama na si kubadilisha, kufanya upanuzi wa masharti ya kisheria au kuyapunguza kinyume na mamlaka iliyotolewa. Kwa hiyo, uchambuzi wake huzingatia uhalali wa mamlaka iliyotumika, mipaka ya mamlaka hayo na uhusiano kati ya masharti ya sheria ndogo na sheria mama.

Madaraka ya Bunge Kutunga Sheria na Kukasimu

Mheshimiwa Spika, madaraka ya kutunga sheria za nchi ni mamlaka ya msingi ya Bunge, yaliyotolewa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara ya 97(5) imelipa Bunge uwezo wa kumkabidhi mtu au mamlaka nyingine jukumu la kuweka sheria ndogo kwa mipaka inayoainishwa na Bunge lenyewe. Kwa hiyo, madaraka ya kuweka sheria ndogo yanayotumiwa na mamlaka hizo ni madaraka yaliyokasimiwa na Bunge. Kukasimu kwa mamlaka hizo hakumaanishi kwamba Bunge limeacha wajibu wake wa kuhakikisha mamlaka hizo zinatumia madaraka yake ndani ya mipaka iliyowekwa na madhumuni ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, jukumu hilo la usimamizi linaonekana pia katika kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinachoweka sharti la Kanuni na sheria ndogo nyingine kuwasilishwa Bungeni ndani ya muda uliowekwa. Utaratibu huu unalipa Bunge fursa ya kuendelea kutekeleza jukumu lake la udhibiti wa mamlaka yake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bunge, Kanuni za Bunge zimeweka mfumo wa Kamati na utaratibu wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Utaratibu huo unaliwezesha Bunge kutekeleza jukumu lake la udhibiti wa sheria ndogo kwa njia ya uchambuzi. Kwa hiyo, uchambuzi unaofanywa na Kamati si hatua ya kiutaratibu pekee, bali ni utekelezaji wa wajibu wa kikatiba wa Bunge.

Mipaka ya Mamlaka ya Kutunga Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya kutunga sheria ndogo si mamlaka ya kujitegemea, bali ni mamlaka yaliyokasimiwa na

Bunge kupitia sheria mama. Kwa hiyo, mamlaka hayo lazima yatumiwe kwa madhumuni yaliyokusudiwa na ndani ya mipaka iliyowekwa na sheria iliyoyatoa. Sheria ndogo haiwezi kutoa mamlaka ambayo hayajatolewa na sheria mama, wala kuweka masharti yanayokwenda kinyume na Katiba, sheria mama au sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, mipaka hiyo, inaifanya Kamati kujiuliza sheria ndogo imetungwa kwa mamlaka gani, kwa madhumuni gani na ndani ya mipaka ipi? Kwa msingi huo, Kamati inapochambua sheria ndogo, huangalia kwa makini uhusiano kati ya mamlaka yaliyotolewa na masharti yaliyowekwa. Lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba mamlaka zilizokasimiwa hazitumii vibaya madaraka yake na kuvuka mipaka iliyowekwa na Bunge.

Udhibiti wa Kibunge wa Mamlaka Yaliyokasimiwa

Mheshimiwa Spika, kukabidhi kwa mamlaka nyingine jukumu la kuweka sheria ndogo haiwi sababu inayoliruhusu Bunge kutotekeleza jukumu lake la kusimamia matumizi ya sheria hizo. Kinyume chake, udhibiti wa kibunge unahakikisha kwamba, mamlaka yaliyokasimiwa yanatumika kwa uhalali, kwa madhumuni yaliyokusudiwa na kwa kuzingatia mipaka iliyowekwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huu, uchambuzi unaofanywa na Kamati ni sehemu ya mfumo wa uwajibikaji wa matumizi ya mamlaka yaliyokasimiwa. Kupitia uchambuzi huo, Kamati kwa niaba ya Bunge inahakikisha kuwa mamlaka hayo yametumika kwa mujibu wa sheria na kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Hali hiyo inasaidia kuzuia matumizi ya mamlaka yanayoweza kuathiri haki za wananchi, kuongeza wajibu usio na msingi wa kisheria au kuleta matokeo ambayo hayakukusudiwa na sheria mama.

Vigezo Vilivyotumika katika Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuishia kuangalia kama sheria ndogo imetungwa na mamlaka iliyotajwa katika sheria mama. Ili kuipima kwa ukamilifu, Kamati ilitumia vigezo sita vya msingi:

Mamlaka, Uhalali, Ulinganifu, Utekelezekaji, Uandishi na Usahihi. Vigezo hivi ndivyo vilivyokuwa kipimo cha Kamati katika kubaini kama sheria ndogo imetungwa kwa mamlaka sahihi, kwa madhumuni yaliyokusudiwa na ndani ya mipaka ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha kwanza ni Mamlaka ambacho kilileta swali: Je, sheria ndogo imetungwa kwa mamlaka gani na ndani ya mipaka ipi? Kigezo cha pili ni Uhalali kilicholeta swali: Je, masharti yake yana msingi halali wa kisheria? Cha tatu ni Ulinganifu kilicholeta swali: Je, yanaendana na Katiba, sheria mama na sheria nyingine za nchi? Cha nne ni Utekelezekaji kikiwa na swali: Je, masharti hayo yanaweza kutekelezeka katika mazingira halisi? Cha tano ni Uandishi kilicholeta swali: Je, vifungu vimeandikwa kwa uwazi na kwa kuzingatia misingi ya uandishi wa sheria? na cha sita ni Usahihi kikiuliza: Je, kuna makosa au kasoro za kiufundi zinazoweza kuathiri maana au utekelezaji?

Mheshimiwa Spika, kwa pamoja, vigezo hivi viliiwezesha Kamati kuangalia sheria ndogo kwa mfululizo kamili wa uhalali wake. Yaani, imetokana na mamlaka gani, imeweka masharti gani, inaendana na sheria zipi, inatekelezekaje na imeandikwaje. Kwa msingi huo, Kamati iliweza kutofautisha kasoro za kisheria, kiutaratibu na masuala yanayohitaji maboresho ya kisera au kiutendaji.

Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Pili wa Bunge, Serikali iliwasilisha Mezani Magazeti ya Serikali na nyongeza zake. Kati ya nyongeza hizo zilikuwepo sheria ndogo ishirini na tano (25) zilizobainika kuwa na dosari mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo zilizowasilishwa na kuchambuliwa na Kamati zilitoka Wizara zifuatazo: -

(a) Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji – sheria ndogo moja (01);

(b) Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) - sheria ndogo kumi na nane (18);

(c) Wizara ya Madini - sheria ndogo moja – (01);

(d) Wizara ya Fedha – sheria ndogo moja (01);

(e) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi - sheria ndogo moja (01);

(f) Wizara ya Ujenzi – sheria ndogo moja (01);

(g) Wizara ya Uchukuzi – sheria ndogo moja (01); na

(h) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo – sheria ndogo moja (01).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina ulioiwezesha kubaini dosari mbalimbali. Maelezo ya kina kuhusu dosari zilizobainika, maoni na ushauri wa Kamati yameainishwa katika Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili, lililoambatishwa katika Taarifa hii kama **KIAMBATISHO Na. 1**

Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge, Serikali iliweka mezani matoleo ya Magazeti ya Serikali na nyongeza zake. Uchambuzi wake ulionesha kuwa jumla ya sheria ndogo nane (08) zilihitaji kufanyiwa uchambuzi wa kina. Wizara zilizohusika na sheria ndogo hizo ni:

(a) Wizara ya Uchukuzi – sheria ndogo sita (06); na

(b) Wizara ya Kilimo – sheria ndogo mbili (02).

Mheshimiwa Spika, katika mchanganuo wa sheria ndogo uliowasilishwa, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina katika sheria ndogo hizo nane (08), ambapo ilibaini dosari na kutoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha na kuimarisha maudhui ya sheria

hizo, kama inavyoainishwa katika Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Tatu lililoambatishwa kwenye Taarifa hii kama **KIAMBATISHO Na. 2.**

Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia vigezo vya uchambuzi vilivyobainishwa awali, Kamati ilichambua sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu wa Bunge na kubaini maeneo mbalimbali yanayohitaji marekebisho au hatua za kuboresha. Miongoni mwa matokeo hayo ni sheria ndogo kuweka masharti yanayokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi, kutokuzingatia misingi ya uandishi wa sheria na kuweka masharti yasiyotekelezeka kwa uhalisia.

Mheshimiwa Spika, matokeo haya yanaonesha umuhimu wa uchambuzi wa sheria ndogo katika kuhakikisha kuwa mamlaka yaliyokasimiwa na Bunge yanatumika kwa uhalali, ndani ya mipaka iliyowekwa na sheria mama na kwa namna inayoweza kutekelezeka kwa ufanisi. Kwa mantiki hiyo, uchambuzi huu haukuishia kubaini kasoro, bali umeiwezesha Kamati kuainisha maeneo yanayohitaji kuimarishwa katika matumizi ya mamlaka yaliyokasimiwa na utekelezaji wa sheria kwa ujumla. Katika sehemu hii, Taarifa inaainisha dosari hizo na kuonesha namna zilivyobainika, athari zake na hatua zinazopendekezwa.

Sheria Ndogo Kukiuka Sheria Mama au Sheria Nyingine

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo kukiuka sheria mama au Sheria nyingine za nchi ni dosari ya kisheria inayojitokeza pale ambapo masharti yake yanazidi, kubadilisha au kwenda kinyume na mamlaka yaliyotolewa na sheria mama. Kwa mantiki hiyo, sheria ndogo haiwezi kuweka sharti linalopingana na matakwa ya sheria mama au sheria nyingine ya nchi, isipokuwa pale ambapo mamlaka ya kufanya hivyo imetolewa wazi na sheria inayohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kigezo cha ulinganifu, Kamati ilijiuliza: Je, masharti ya sheria ndogo yanaendana na masharti ya sheria mama yaliyotoa mamlaka ya kutungwa kwake? Kwa kujibu

swali hilo, Kamati ililinganisha masharti ya sheria ndogo na vifungu vya sheria mama vinavyotoa mamlaka hayo na kubaini maeneo ambayo masharti ya sheria ndogo yanatofautiana au kukiuka sheria mama. Hali hiyo ni kinyume na msingi uliowekwa na Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kwamba sheria ndogo iliyotungwa chini ya mamlaka ya sheria ya Bunge haipaswi kuwa na masharti yanayokinzana na sheria iliyotoa mamlaka ya kutungwa kwake au na sheria nyingine yoyote ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia msingi huo, sheria ndogo inapaswa kuwezesha utekelezaji wa sheria mama bila kubadili au kukinzana na masharti yake. Miongoni mwa maeneo ambayo Kamati ilibaini mgongano huo ni katika masharti ya adhabu, ambapo baadhi ya sheria ndogo ziliweka viwango au muda wa adhabu tofauti na vilivyowekwa katika sheria mama.

Mheshimiwa Spika, mfano wa kwanza unahusu The Civil Aviation (Aeronautical Information Services) Regulations, 2026 (TS. Na. 38 la tarehe 30 Januari 2026), zilizotungwa chini ya Kifungu cha 5 cha Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80. Kamati ilibaini kuwa Kanuni ya 61 inaweka adhabu ya faini isiyozidi Shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi miezi sita, au adhabu zote mbili kwa pamoja. Hata hivyo, Kifungu cha 73 cha Sheria ya Usafiri wa Anga Sura 80, kinaweka adhabu ya faini isiyopungua kiasi kinacholingana na Dola za Marekani 1,000 au kifungo kisichopungua miezi 12, au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, tofauti hii si tofauti ya uandishi wala ya namna ya kueleza adhabu, ni tofauti ya kiwango cha adhabu kilichowekwa na sheria ndogo dhidi ya kiwango kilichowekwa na sheria mama.

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili unahusu kanuni ziitwazo: The Tanzania Shipping Agencies (Dry Port) Regulations, 2025 (TS. Na. 606 la tarehe 17 Oktoba 2025), zilizotungwa chini ya Kifungu cha 61(2)(g)(ii) cha The Tanzania Shipping Agencies Act, Sura ya 415. Kamati ilibaini kuwa Kanuni ya 35(k) inaweka adhabu ya kifungo kisichopungua miaka miwili lakini kisichozidi miaka mitano, au faini ya Shilingi milioni 20 hadi milioni 40, au asilimia 10 ya thamani ya

mzigo unaohusika. Kwa upande mwingine, Kifungu cha 57 cha sheria mama kinaweka faini ya Dola za Marekani 20,000 hadi 40,000, au kifungo cha miaka mitatu hadi mitano, au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, hapa pia tofauti ina uzito kisheria, ambapo sheria ndogo imeweka kiwango cha chini cha kifungo kuwa miaka miwili, wakati sheria mama imeweka miaka mitatu. Aidha, sheria ndogo imeweka pia mfumo wa faini tofauti na ule uliowekwa na sheria mama. Kwa hiyo, masharti hayo hayaakisi kiwango cha adhabu kilichowekwa na Bunge katika sheria mama. Kwa kiwango hicho, yanazua suala la matumizi ya mamlaka yaliyokasimiwa nje ya mipaka iliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, mifano hii inatokana na kanuni moja ya msingi kwamba, mamlaka yaliyokasimiwa hayawezi kuwa makubwa kuliko mamlaka yaliyotolewa na Bunge. Pale ambapo sheria ndogo inabadili kiwango cha adhabu kilichowekwa na sheria mama, suala linalojitokeza si la uandishi, bali ni kuvuka mpaka wa mamlaka yaliyokasimiwa. Bunge linatarajia mamlaka inayohusika itarekebisha masharti hayo ili yaendane na sheria mama na kurejesha sheria ndogo ndani ya mipaka ya mamlaka iliyotolewa.

Sheria Ndogo Kutozingatia Misingi ya Uandishi wa Sheria (Drafting Principles)

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo huwa na dosari ya kiuandishi pale ambapo masharti yake hayajaandikwa kwa namna iliyo wazi, sahihi, yenye mantiki na isiyoleta utata, kiasi cha kuweza kuathiri maana, tafsiri au utekelezaji wake. Kwa hiyo, uandishi wa sheria si suala la lugha pekee, bali ni sehemu ya kuhakikisha kuwa dhamira na madhumuni ya sheria yanaelezwa kwa usahihi na yanaweza kutekelezwa kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kigezo hicho, Kamati ilichambua The Banking and Financial Institutions (Non-Interest Banking Business) Regulations, 2025 (TS. Na. 688 la tarehe 19/12/2025) iliyotungwa chini ya Kifungu cha 71 cha The Banking and Financial Institutions Act, (Cap 342). Kamati ilibaini kuwa Kanuni ya 10(3), inayoitaka Bodi kuhakikisha kuwa uhuru wa

Kamati unakuwepo, ina kosa la kiuandishi la kutokamilika kwa sentensi. Dosari hiyo inaweza kuleta tafsiri zaidi ya moja au kufanya sharti linalohusika lisieleweke kwa namna moja, na hivyo kuathiri uhakika na utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilibaini kutokuzingatiwa kwa misingi ya uandishi wa sheria, hususan katika Kanuni ya The Transport Licensing (Exclusive Licence) Regulations, 2025 (TS. Na. 9 la tarehe 23/1/2026) ambazo zimetengenezwa chini ya Kifungu cha 46 cha The Transport Licensing Act, Sura ya 317. Jedwali la 3 la Kanuni hii linaweka fomu ya "Notisi ya Uboreshaji" ambayo ina makosa ya kiuandishi kwa kurejea kanuni ya 22 (2) ambayo kimsingi haipo. Kosa hili linaweza kuleta mkanganyiko juu ya kanuni inayokusudiwa na fomu hii. Kwa mtazamo wa Kamati, kasoro ya kiuandishi inapoweza kubadili maana, kuleta utata au kuathiri utekelezaji wa sharti la kisheria, haiwezi kuchukuliwa kuwa ni suala la uhariri pekee, bali ni dosari inayostahili kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, uzingatiaji wa misingi ya uandishi wa sheria ni muhimu katika kuhakikisha sheria zinaandikwa kwa lugha iliyo wazi, sahihi, yenye mantiki na isiyoleta utata. Uandishi bora huwezesha sheria kueleweka kwa usahihi, kutafsiriwa na kutekelezwa kwa ufanisi. Aidha, huimarisha uwazi na uthabiti wa sheria na hivyo kuhakikisha dhamira na madhumuni yaliyokusudiwa yanafikiwa ipasavyo.

Sheria Ndogo Kuweka Masharti Yasiyo na Uhalisia

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo huwa na dosari ya kutokuwa na uhalisia pale ambapo sharti lililowekwa, ingawa linaweza kuwa na msingi wa kisheria, haliwezi kutekelezeka kwa ufanisi katika mazingira halisi au linaweka matakwa yasiyo na uwiano na mazingira, uwezo na rasilimali zilizopo. Kwa hiyo, zaidi ya kuwa halali sharti la kisheria linapaswa liweze kufanya kazi kwa uhalisia na kufikia madhumuni yaliyokusudiwa bila kuwa kikwazo kisichokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kigezo hicho, Kamati ilibaini hali hii katika Kanuni ziitwazo The Fertilizers Regulations, 2026 (TS. Na. 68 la tarehe 20 Februari 2026), zilizotungwa chini ya Kifungu

cha 53 cha Sheria ya Mbolea, Sura ya 378. Jedwali la Pili la Kanuni hizo linaweka ada ya Dola za Marekani 10,000 kwa kila msimu na kwa kila aina mpya ya mbolea au kirutubisho cha mbolea kwa ajili ya majaribio ya mbolea shambani.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wa Kamati, kiwango hicho kinaweza kuwa mzigo mkubwa, hususan kwa wazalishaji wadogo. Athari yake ni kuwa kikwazo katika uzalishaji na uendelezaji wa sekta ya mbolea badala ya kuwezesha utekelezaji wa madhumuni yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilibaini hali hiyo katika Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2025 (TS. Na. 301). Kifungu cha 10 kinaweka tozo ya asilimia tano ya thamani ya chombo kilichobeba mzigo, kwa kila siku ambayo mzigo uliokamatwa kwa kutolipiwa ada au ushuru unashikiliwa. Kamati iliona kuwa, msingi huo wa ukokotoaji unaweza kutengeneza mzigo mzito wa ulipaji usiowiana na thamani ya mzigo wenyewe. Kwa mfano, mzigo wa thamani ndogo unapobebwa na chombo chenye thamani kubwa, tozo yake inaweza kuwa kubwa kuliko thamani halisi ya mzigo.

Mheshimiwa Spika, mifano hii inaonesha kuwa sharti linaweza kuwa halali kisheria lakini likawa gumu au lisilofaa katika utekelezaji. Kwa kuwa, uhalali pekee hautoshi, Kamati hujiuliza: Je, sharti hili linaweza kutekelezwa kwa uhalisia, kwa uwiano na bila kuwa kikwazo kwa madhumuni ya sheria mama? Hiki ndicho kipimo kinachosaidia kuhakikisha kuwa sheria ndogo si sahihi kisheria kwa maandishi tu, bali pia zinafanya kazi kwa ufanisi katika mazingira halisi.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati inaona kuwa mamlaka zinazotunga sheria ndogo zinapaswa pia kuzipima kwa mazingira halisi ya utekelezaji, uwezo wa wahusika na athari zinazoweza kujitokeza. Kufanya hivyo kunawezesha masharti yaliyowekwa kutekelezwa kwa ufanisi, kwa uwiano na kwa mujibu wa madhumuni ya sheria mama.

SEHEMU YA TATU

MAONI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa sheria ndogo, sehemu hii inatoa mtazamo wa jumla kuhusu masuala yaliyobainika. Mtazamo huo una sura ya maoni ambayo yanajenga msingi wa mapendekezo ya Kamati ambayo yataliwezesha Bunge kufikia uamuzi sahihi kuhusu masuala yaliyobainika kwenye sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu.

Maoni

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia nafasi ya sheria ndogo katika kuwezesha utekelezaji wa sheria na katika kusimamia masuala yanayogusa moja kwa moja maisha na maslahi ya wananchi, Kamati imeona umuhimu wa kutathmini ubora na uhalali wa sheria hizo kwa kuzingatia mipaka ya mamlaka yaliyokasimiwa, ulinganifu wa mfumo wa sheria, misingi ya uandishi wa sheria, uhalisia na utekelezekaji wa masharti pamoja na uwajibikaji wa mamlaka zilizokasimiwa. Kwa msingi wa uchambuzi huo, Kamati inawasilisha maoni yake kama ifuatavyo: -

Mipaka ya mamlaka yaliyokasimiwa

Mamlaka yanapokasimiwa kwa ajili ya kutunga sheria ndogo, yanapaswa kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na ndani ya mipaka iliyowekwa na sheria mama au sheria nyingine inayotoa mamlaka hayo. Sheria ndogo yenye masharti yanayovuka mipaka hiyo au yanayokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi inaweza kudhoofisha utekelezaji wa madhumuni yaliyokusudiwa, kuathiri uhalali wa utekelezaji wa mamlaka yaliyokasimiwa na kuvuruga uthabiti wa mfumo wa sheria nchini.

Ulinganifu wa Mfumo wa Sheria

Sheria ndogo zinapotungwa, zinapaswa kuendana na sheria mama pamoja na sheria nyingine za nchi zinazohusika ili kudumisha mshikamano, uhakika na uelekeo unaofanana katika mfumo wa sheria. Sheria ndogo yenye masharti yanayokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi inaweza kusababisha mgongano wa kisheria, kuleta tafsiri zinazokinzana, kudhoofisha utekelezaji wa madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge na kuvuruga uthabiti wa mfumo wa sheria nchini.

Uzingatiaji wa Misingi ya Uandishi wa Sheria

Sheria ndogo zinapaswa kuzingatia misingi ya uandishi wa sheria, ikiwemo usahihi, uwazi, uthabiti na ufasaha, ili masharti yake yawe yanayoeleweka, yanayotabirika na yanayotekelezeka kwa ufanisi. Sheria ndogo yenye masharti yenye utata au yasiyoandikwa kwa kuzingatia misingi hiyo inaweza kusababisha ugumu wa kueleweka na kutafsiriwa, kuleta uelewa na utekelezaji usiofanana miongoni mwa wahusika na hatimaye kudhoofisha utekelezaji wa madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge.

Uhalisia na Utekelezekaji wa Masharti

Sheria ndogo zinapaswa kuzingatia mazingira halisi ambayo zinalenga kuyasimamia, pamoja na uwezo wa wahusika na taasisi zinazowajibika kuzitekeleza, ili masharti yaliyowekwa yawe yanatekelezeka kwa ufanisi na kwa uelekeo unaoeleweka. Sheria ndogo yenye masharti yasiyoendana na uhalisia wa utekelezaji inaweza kusababisha ugumu wa utekelezaji na tafsiri, kuweka uelewa usiofanana miongoni mwa wahusika na hatimaye kufanya sheria ishindwe kufikia madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge, hivyo kupunguza tija na thamani ya ukasimishaji wa madaraka ya kutunga sheria ndogo.

Uwajibikaji wa Mamlaka Zilizokasimiwa

Madaraka yaliyokasimiwa na Bunge ya kutengeneza sheria ndogo, yanapaswa kuendana na wajibu wa mamlaka zinazohusika kutoa mrejesho na kuchukua hatua stahiki pale

dosari zinapobainika, ili kuwezesha Bunge kufuatilia. Mamlaka zinazohusika zinaposhindwa kutoa mrejesho au kuchukua hatua kuhusu dosari zilizobainishwa, zinalikosesha Bunge fursa ya kujiridhisha iwapo mamlaka yaliyokasimiwa yanatumika kwa mujibu wa madhumuni, mipaka na masharti yaliyowekwa na sheria mama.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati ina maoni kwamba, uchambuzi wa sheria ndogo unaolisaidia Bunge, Serikali, wananchi na kuwezesha ustawi wa maisha yao, unapaswa kubaini, iwapo mamlaka yaliyokasimiwa yametumika kwa uhalali, kwa madhumuni yaliyokusudiwa, kwa namna inayotekelezeka na kwa kuzingatia maslahi ya wananchi kama ilivyobainishwa katika Taarifa hii.

Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na Kamati kuhusu uhalali, ulinganifu, ubora, utekelezekaji na uwajibikaji katika utungaji na utekelezaji wa sheria ndogo, Kamati inapendekeza hatua stahiki za kibunge ili kurekebisha dosari zilizobainika na kuimarisha matumizi ya mamlaka yaliyokasimiwa. Kwa msingi huo, Kamati inawasilisha mapendekezo yake na kuliomba Bunge liridhie kama ifuatavyo: -

Mipaka ya Mamlaka Yaliyokasimiwa

KWA KUWA, mamlaka ya kutunga sheria ndogo yanapokasimiwa na Bunge yanapaswa kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na ndani ya mipaka iliyowekwa na sheria mama au sheria nyingine inayotoa mamlaka hayo;

NA KWA KUWA, sheria ndogo yenye masharti yanayovuka mipaka ya mamlaka yaliyokasimiwa inaweza:

(a) kuathiri uhalali wa sheria hiyo;

(b) kudhoofisha dhamira ya Bunge kukasimu madaraka ya kutunga sheria kwa mamlaka zinazohusika; na

(c) kusababisha mamlaka zinazohusika kutumia madaraka ambayo hayakukusudiwa na Bunge.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zote zinazohusika na sheria ndogo zilizobainika kutoka nje ya mamlaka yaliyokusudiwa kama inavyoonekana kwenye Majedwali ya Uchambuzi, zifanye marekebisho stahiki.

Ulinganifu wa Mfumo wa Sheria

KWA KUWA, sheria ndogo zinapaswa kuendana na sheria mama pamoja na sheria nyingine za nchi zinazohusika ili kudumisha uhakika na uelekeo unaofanana katika mfumo wa sheria;

NA KWA KUWA, sheria ndogo yenye masharti yanayokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi inaweza –

(a) kusababisha mgongano wa kisheria;

(b) kuleta tafsiri zinazokinzana;

(c) kudhoofisha utekelezaji wa madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge; na

(d) kuvuruga uthabiti wa mfumo wa sheria nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na sheria ndogo zilizobainika kuwa na masharti yanayokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi zifanye marekebisho stahiki ili kuhakikisha kuwa sheria hizo zinaendana na mfumo wa sheria wa nchi.

Uzingatiaji wa Misingi ya Uandishi wa Sheria

KWA KUWA, sheria ndogo zinapaswa kuandikwa kwa kuzingatia misingi ya usahihi, uthabiti na ufasaha wa kisheria ili masharti yake yawe yanayoeleweka, yanayotabirika na yanayotekelezeka;

NA KWA KUWA, sheria ndogo zilizo na masharti yenye utata au yasiyoandikwa kwa kuzingatia misingi hiyo inaweza –

(a) kusababisha ugumu wa kueleweka na kutafsiriwa,

(b) kuleta uelewa na utekelezaji usiofanana miongoni mwa wanaohusika; na

(c) kudhoofisha utekelezaji wa madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari za kiuandishi zifanye marekebisho stahiki ili kuhakikisha kuwa masharti yake yanaeleweka, yanatafsirika kwa uelekeo unaofanana na yanatekelezeka kwa ufanisi.

Uhalisia na Utekelezekaji wa Masharti

KWA KUWA, sheria ndogo zinapaswa kuzingatia mazingira halisi ambayo zinalenga kuyasimamia pamoja na uwezo wa wahusika na taasisi zinazowajibika kuzitekeleza ili masharti yake yawe yanatekelezeka kwa ufanisi;

NA KWA KUWA, sheria ndogo zenye masharti yasiyoendana na mazingira halisi ya utekelezaji zinaweza –

(a) kusababisha ugumu wa utekelezaji na tafsiri,

(b) kuweka uelewa usiofanana miongoni mwa wahusika; na

(c) kukwamisha madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na sheria ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyoendana na uhalisia wa utekelezaji, zifanye marekebisho ili kuhakikisha kuwa masharti hayo yanaendana na mazingira halisi, uwezo wa utekelezaji na madhumuni yaliyokusudiwa na Bunge.

Uwajibikaji wa Mamlaka Zilizokasimiwa

KWA KUWA, ukasimishaji wa madaraka ya kutunga sheria ndogo unaambatana na wajibu wa mamlaka zilizokasimiwa kutumia

madaraka hayo kwa mujibu wa sheria mama na kuwajibika kuhusu namna yanavyotumika;

NA KWA KUWA, Bunge linapobaini dosari katika sheria ndogo, mamlaka zilizohusika zinapaswa kuchukua hatua stahiki kuhusu dosari hizo na kutoa mrejesho kwa Bunge ili-

(a) Kuliwezesha kufuatilia na kujiridhisha na marekebisho yaliyoazimiwa; na

(b) Kutimiza wajibu wake wa kiudhibiti wa sheria ndogo

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na sheria ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari kama ilivyobainishwa katika Majedwali ambayo ni kiambatisho cha Taarifa hii, zifanye marekebisho na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Katibu wa Bunge kabla au ifikapo tarehe 2 Novemba, 2026.

Hitimisho

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu wa sheria ndogo umekuwa nyenzo muhimu ya kuliwezesha Bunge kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kusimamia matumizi ya mamlaka yaliyokasimiwa. Aidha, Taarifa hii inaliwezesha Bunge kuhakikisha kuwa sheria ndogo zinatungwa kwa uhalali, zinaendana na mfumo wa sheria na zinazingatia uhalisia wa utekelezaji. Ni imani ya Kamati kwamba, Utekelezaji wa maazimio ya Bunge yanayotokana na mapendekezo ya Kamati utaimarisha uwajibikaji wa mamlaka zilizokasimiwa na kuongeza ubora wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa Bungeni. Ni matumaini yangu kwamba utaratibu huu utakuwa endelevu na hivyo kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa kwa kiasi kikubwa masuala mengi yanayoibuliwa kutokana na uchambuzi wa sheria ndogo yanagusa maisha ya kila siku ya wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nimshukuru Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Kabudi, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) kwa kuendelea kuweka uratibu mzuri ambao uliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati kwa ajili ya kutoa ufafanuzi na kujibu hoja zilizoibuliwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa wadau wote walioshiriki na kufika mbele ya Kamati kutoa maoni yao kuhusu Kanuni za Mbolea za mwaka 2026. Ushiriki wao umeiwezesha Kamati kupata uelewa mpana kuhusu masuala ya mbolea, jambo ambalo limeisaidia Kamati kuboresha Kanuni hizo kwa manufaa ya sekta ya mbolea na Taifa kwa ujumla. Naomba niwatambue wadau hao kama ifuatavyo: -

1. Minjingu Mines & Fertiliser Limited;
2. Tanzania National Chamber of Commerce (TNCC);
3. Triachem Tanzania Limited;
4. Itracom Fertilizers Limited;
5. Pangani Production Field (Paprof) Group Tanzania;
6. Anti Corruption Voices Foundation;
7. Tanzania Biotech Products Limited;
8. Tanganyika Law Society – TLS;
9. Lavan Investment Limited; na
10. Tanzania Crop Care Limited.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu wa Bunge na hatimaye kufanikisha kazi hii.

Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge (*Hansard*): -

1. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, (Mb) – **Mwenyekiti;**
2. Mhe. Zuberi Yahya Mfaume, (Mb) – **Makamu Mwenyekiti;**
3. Mhe. Sigrada Wilhelm Mligo, (Mb);

4. Mhe. Agnes Mathew Marwa, (Mb);
5. Mhe. Mwanaenzi Hassan Suluhu, (Mb);
6. Mhe. Salehe Mbwana Mhando, (Mb);
7. Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe, (Mb);
8. Mhe. Jesca Yuda Mbogo, (Mb);
9. Mhe. Imamu Mtumwa Vuai, (Mb);
10. Mhe. Mussa Omar Salim, (Mb);
11. Mhe. Rashid Habib Ali, (Mb);
12. Mhe. Juma Khamis Sadifa, (Mb);
13. Mhe. Suleiman Premji Arif, (Mb);
14. Mhe. Clayton Revocatus Chipando, (Mb);
15. Mhe. Haji Kombo Mdowe, (Mb); na
16. Mhe. George Boniface Simbachawene, (Mb).

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kumshukuru kwa dhati Ndg. Baraka I. Leonard, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wake wa dhati na Kamati hii katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Hoja

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako, liipokee na kuikubali Taarifa hii kuhusu Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu na kupitisha Mapendekezo ya Kamati kuwa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Cecilia Daniel Paresso, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO
03 Septemba, 2026

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mwenyekiti wetu

wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa uwasilishaji makini wa taarifa ya Kamati yako.

Waheshimiwa Wabunge kabla ya kuendelea na hatua inayofuata, ninalo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuwa, Maafisa Uhamiaji wamewasilisha Hati za Kusafiria za Wabunge zilizokuwa tayari. Hivyo Waheshimiwa Wabunge ambao hawajachukua hati zao za kusafiria, wanaombwa kufika katika jengo la Utawala *ground floor* ukumbi namba tisa, leo tarehe 3 Septemba, 2026 kuanzia saa nne asubuhi ili kupata hati hizo za kusafiria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea taarifa ya Kamati, tunaanza mjadala au uchangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Imamu Mtumwa Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, Mheshimiwa Mdowe Haji Kombo ajiandae.

MHE. IMAMU MTUMWA VUAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwanza kabisa, ninaomba nirekebishe, jina hili liingie kwenye *Hansard* vizuri. Ninaitwa Imamu Mtumwa Vuai, siyo Imamu Mtumwa Nahodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwa wazima wa afya na kukutana katika hafla ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapenda kwa dhati ya moyo wangu kumshukuru Mwenyekiti kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa hii ya Kamati. Kwa upande wangu, katika mchango wangu, nitajaribu kujielekeza kwenye maeneo matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni uhalisia. Tumeona Mwenyekiti alipojaribu kulizungumzia eneo hili la uhalisia, amegusa mifano miwili. Mfano wa kwanza ilikuwa ni ile Sheria ya Ushuru ya Jiji la Dar es Salaam, na alijaribu kugusia kama mnakumbuka vizuri, kile kifungu ambacho kilikuwa kinatoza chombo cha usafiri badala ya mzigo kwa asilimia tano kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa asilimia tano kwa siku kama ni adhabu ya chombo kinachosafirisha mzigo, ni kubwa sana. Kwa sababu, kama tutaangalia vizuri wanaosafirisha mizigo, baadhi ya wakati inawezekana ikawa sio wafanyabiashara wakubwa, ni wafanyabiashara wadogo ambao amekodi lori lenye thamani ya shilingi milioni 200, lakini mzigo wake una thamani ya shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema kwamba kwa sababu amekiuka masharti hajalipa ushuru, tumchaji asilimia tano kwa siku, tafsiri yake Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, kwa siku tunaenda kumchaji shilingi milioni 10. Kwa hiyo, tunaposema kama Kamati kwamba hili jambo halina uhalisia, tuna maana kwamba halina uhalisia kweli kweli, kwa sababu hatuwezi kumchaji mwananchi shilingi milioni 10 kwa siku kwa sababu tu eti thamani ya kile chombo ndiyo kiweze kuchajiwa ile kodi. Hili jambo halina uhalisia kabisa. Lazima tuwe wakweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Sheria Ndogo ni ndogo kwa jina lake, lakini ni kubwa kwa athari zake. Kwa hiyo, wakati tunapotunga hizi sheria ni lazima tuzingatie hilo pia. Athari za tozo ambazo tunaziweka katika sheria zetu, zinaenda kuwaathiri moja kwa moja wananchi wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hii ikiongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Daktari wa Maendeleo, anatamani sana wananchi wa chini hawa tusiwaadhibu kwa kodi hizi au kwa tozo hizi na Sheria Ndogo ambazo zitakuwa hazina maslahi kwa maisha yao wala kwa kutekeleza ile dhana nzima ya Dira yetu ya Taifa ya 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningeweza kuligusia kwa ufupi ni matumizi ya lugha ya Kiingereza kwenye Sheria Ndogo. Wakati tunajadili, zipo baadhi ya sheria ambazo zinaletwa kwa lugha ya Kiingereza. Ninataka tukumbuke kwamba lugha yetu ya Taifa ni lugha ya Kiswahili. Vilevile, Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza, Ibara ya 85 imeeleza kwa uwazi kwamba, lugha ambayo itatumika kutunga Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hiyo imeenda mbali zaidi kwa kusema kwamba endapo itatokea tumetumia lugha ya Kiingereza, basi itafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili, lakini bado kuna baadhi ya Sheria Ndogo mpaka leo zinaletwa kwa lugha ya Kiingereza. Watanzania walio wengi, hatufahamu lugha ya Kiingereza kwa ufasaha.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Hitimisha Mheshimiwa.

MHE. IMAMU MTUMWA VUAI: Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ninaomba nihitimishe kwenye matumizi ya fedha za kigeni. Zipo baadhi ya sheria bado zinafanya *quotation* kwa dola za Kimarekani, jambo ambalo tunaenda kinyume hata na zile *regulations* ambazo zimewekwa na *BoT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, atafuatiwa na Mheshimiwa Mdowe Haji Kombo, na Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, ajiandae. Mheshimiwa Mdoe Haji Kombo.

MHE. MDOWE HAJI KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi leo niweze kuchangia katika taarifa ya Kamati ambayo imewasilishwa mbele yetu. Kwanza kipekee ninaomba nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya ya kutuletea maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Sheria Ndogo ameeleza hapa katika uchambuzi wetu wa Sheria Ndogo ambazo zimeletwa mbele yetu, kuna dosari na changamoto nyingi ambazo zimejitokeza. Kwa upande wangu ninaomba nizungumzie katika dosari za kimaandishi, lakini pia nizungumzie katika dosari za sheria kukinzana na sheria nyingine

za nchi ikiwemo Sheria Mama na hata Katiba wakati mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Ndogo hizi ambazo zimeletwa mbele yetu, nitatolea mfano katika Sheria Namba 311 ya tarehe 6/6/2026, ambayo Sheria ilikuwa inazungumzia Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe Mwaka 2015 ambayo imetungwa chini ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 12(3) kinarejea kimakosa Kifungu cha 8 kuwa ndicho kinaweka utaratibu wa kuuza mali iliyokamatwa, ilhali ukirudi katika Kifungu hicho kwenda kukisoma, unaenda kukutana na kitu kingine tofauti na hicho ambacho kimeelezwa hapa. Hii ni dosari ya kiuandishi lakini siyo dosari tu ya kiuandishi lakini hii ni kwa sababu inakwenda kuathiri moja kwa moja utendaji na ufanyaji kazi wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiachilia mbali sheria hiyo, kuna sheria nyingine ambayo ni *GN* Na. 358 ambayo inahusu Sheria Ndogo za Ada Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni za Mwaka 2025. Sheria hizi zimetungwa chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali ya Mitaa, Sura ya 290 chini ya Kifungu cha 16(1).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 10 (3) kimerejea kimakosa Kifungu cha 8 kuwa ndicho kimeweka utaratibu wa kuuza mali iliyokamatwa ilhali unaporudi katika sheria yenyewe kwenda kuisoma unakutana na kitu kingine tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linapotunga sheria, linakasimu madaraka kwa mamlaka nyingine kutunga Sheria Ndogo. Hatuishii tu kuwakasimisha madaraka wao, isipokuwa tunatakiwa tuwe kifua mbele kuhakikisha kwamba kile ambacho sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumekikusudia ndicho kimeenda kufanyika huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaporudi, tunazikuta sheria hizi zimekuwa zinaenda tofauti na vile ambavyo sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumekusudia. Maana yake ni nini? Maana yake wananchi wetu wanaelewa kwamba mamlaka ya kutunga sheria ni mamlaka ya Bunge. Kwa hiyo, sheria zinapokwenda kule zikawavuruga na zikawaumiza, lawama zote zinarudi kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili linakwenda kuchukuliwa kwamba ni Bunge dhaifu ilhali sisi siyo Bunge dhaifu, ni Bunge ambalo tunasimama na tunasimamia masilahi ya wananchi. Ukiachana na makosa hayo ya kiuandishi kuna makosa mengine ambayo unakwenda kukuta sheria zinakinzana na sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa sheria hiyo tunarudi katika sheria ile ile ya *GN* Na. 311 ya tarehe 6 Juni kwa Wilaya ile ya Wanging'ombe ambayo katika Kifungu cha 14 kinatoa adhabu kwa mtu aliyekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo unakuja kulikuta kwamba adhabu iliyowekwa na kifungu hiki, inakiuka adhabu iliyowekwa na Kifungu cha 66 Sura ya 290 ya Sheria ya Mama. Pia, adhabu hii inakiuka masharti ya sheria ya tafsiri ya sheria. Kwa hiyo, ukiukwaji huu wa sheria moja kwa moja unaweza kusababisha adhabu iliyowekwa kukosa uhalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara yake ni nini? Ninarudi kule, madhara yake ni kwamba sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunakwenda kudharaulika kupitia hizi mamlaka ambazo tumezikasimia madaraka ya kwenda kutunga Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu kwa mamlaka ambazo tunazikasimia madaraka zielewe kwamba wanapaswa kuelewa kuwa utungaji wa kanuni siyo nafasi ya wao kutengeneza mamlaka mpya au kwenda kufanya ambavyo wao wanajisikia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, ahsante sana, ninaomba uhitimishe hoja.

MHE. MDOWE HAJI KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninahitimisha, bali waelewe utungaji wa kanuni ni njia ya kuwezesha mamlaka iliyotolewa na sheria mama inaenda kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanaenzi Hassan Suluhu, Mheshimiwa Zuberi Yahaya Mfaume ajiandae.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye mjadala huu unaohusisha Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti wetu, mama yetu kwa namna ambavyo amewasilisha vyema. Sisi kama wadau wa Sheria Ndogo katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yapo mambo ambayo tumeyaona na tunaona yanaenda kutupigisha shoti kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wabunge, tukienda mbele ya wananchi wanatuambia kwamba hizi sheria siyo mmezipitisha ninyi wenyewe Wabunge. Ninaomba niwaambieni ukweli, Kamati ya Sheria Ndogo hatutakubali kupitisha sheria yoyote ambayo inaenda kuwakandamiza wananchi kwa namna nyingine yoyote, hatutaipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutawaomba Waheshimiwa Wabunge muwe mnatuunga mkono pale tunapoleta marekebisho ya sheria kwa sababu hizi sheria nyingine zinaenda kuwakandamiza wananchi ambao wametupigia kura ili tuweze kufika humu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi nimesafiri kwenda Tokyo (Japan). Tokyo (Japan) wanafanya sawasawa na sisi tunavyofanya katika majiji yetu kwa mfano Dar es Salaam kukamata magari ambayo yanapaki ovyo ovyo barabarani, lakini wao wana sababu ya kufanya hivyo kwa sababu wametengeneza sehemu nyingi za *parking* za kulipia katika hayo maeneo. Kwa hiyo, wewe ukipaki gari barabarani tafsiri yake umeacha zile sehemu ambazo wametengeneza, umeenda kufanya vitu ambavyo ni tofauti na wao ambavyo wamepangilia, wanakuwa na sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam wanakamata magari yanayopaki ovyo barabarani lakini hawatengenezi sehemu za kupaki hayo magari. Kwa mfano, ukienda Jiji la Dar es Salaam hata ukisikiliza mijadala yao, unasikia halmashauri inapanga kutengeneza hoteli, *apartments* badala ya kutengeneza majengo marefu hata ya ghorofa 30 kwa ajili ya kupaki magari ili ukimkamata mtu unamwambia *parking* ile pale, kwa nini umepaki hapa? Hawana sababu ya kuendelea kufanya hicho wanachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tutaendelea kudhibiti hizi sheria ambazo zinaletwa na sisi kama Wabunge tuzipitishe ili ziende zikawashambulie wananchi, hatutapitisha. Ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, zipo sheria ambazo tunazipitisha kwa sababu zinaenda kutengeneza mapato kwenye halmashauri, lakini zinaenda kugeuka kuwa ndiyo chimbo la watu kupata rushwa, kutengeneza fedha. Tunapitisha Sheria ya Usafi, kutoza tozo kwa ajili ya usafi, lakini Mheshimiwa Rais amekuwa shahidi wetu, juzi kasema bado miji ni michafu na watu wanatoa hela kwa ajili ya kusafisha miji yetu huko mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunawaomba sana hasa Waheshimiwa Madiwani ambao wapo kwenye halmashauri zetu, waziangalie hizi sheria kabla hazijatufikia huku ili zisituchonganishe. Watakuwa wanatengeneza, wanapitisha sheria, zikifika huku

kwetu juu tunazipiga chini kwa sababu tunaona zinaenda kuwakandamiza wananchi, hatutazipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana tuwe makini hasa wataalamu, sababu hizi sheria ili zifike Bungeni zinakuwa zimepita hatua tofauti tofauti, lakini wataalamu wetu wapo. Unaiona kabisa hii sheria ikifika kule itakuta kwenye Kamati kuna watu kama wakina Baba Levo, hawataipitisha, unaileta kama mtego. Sisi tunasoma, tukigundua huu ni mtego, tunairudisha huko chini unaonekana umefanya kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana wataalamu wetu watusaidie kazi sisi Wabunge pale wanapoiona hii sheria inaenda kuwakandamiza watu, inaenda kinyume na sheria mama wairudishe huko huko kabla haijafika kwenye Kamati ya Sheria Ndogo, kwa sababu ikifika kwetu tutaipiga chini wala hatutakuwa na huruma na hilo, kwa sababu wananchi wameshajua kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo lenye kazi ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sheria yote inayowakandamiza hawawalaumu Madiwani, hawawalaumu wataalamu, wanawalaumu Waheshimiwa Wabunge na sisi Wabunge hatutakubali kulaumiwa kwa sheria za ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie Bunge hili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwaambia wananchi sheria yoyote mnayoiona inakandamiza kipato chenu, inakandamiza mazingira yenu ya kufanya biashara, inakandamiza mazingira yenu ya kupata kipato tuleteeni, toeni maoni na sisi tutaiangalia na kama tunaona ina sababu za msingi za kupigwa chini tutaiondoa ili iende ikafanyiwe marekebisho ili iendane na hali halisi ambayo tunaenda nayo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa sababu sheria zinaweza zikawa zilitungwa miaka mitatu iliyopita, kila mwaka maisha yanabadilika, mazingira yanabadilika, maisha ya watu yanabadilika, kwa hiyo, ni lazima tuwe tunaendelea hivi hivi kupitia zile sheria hata ambazo zilipitishwa na Bunge. Kama

mazingira mwaka jana yalikuwa yapo sawasawa mwaka huu mazingira yamebadilika, imekuwa haifai tutaipiga chini...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo machache, ninaunga mkono hoja ya Kamati ya Sheria Ndogo na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tupitishe haya mabadiliko ambayo tumeyaleta hapa kwenu ili yaende yakafanyiwe marekebisho kuendana na hali halisi ya nchi yetu ya Tanzania, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Mwanaenzi Hassan Suluhu, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Yahaya Mfaume, Mheshimiwa Arif Premji ajiandae.

MHE. MWANAENZI HASSAN SULUHU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia taarifa iliyowasilishwa na Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji mzuri alioutoa, na pia niipongeze Kamati kwa maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika kuchambua sheria hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kada ya sheria ni kada muhimu sana katika Taifa letu, kada hii ndiyo inaenda kuamua maendeleo na lile tabasamu alilolikusudia Mheshimiwa Rais kuliwasilisha kwa wananchi. Sheria Ndogo ni miongoni mwa sheria ambazo zinapaswa kuzingatia misingi ya uandishi wa kisheria ikiwemo usahihi, uwazi, ufanisi na uthabiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti haya yasipozingatiwa, basi sheria ndogo hizi zitashindwa kutekelezeka. Katika uchambuzi, Kamati ya Sheria Ndogo wakati sheria hizi zilivyowasilishwa Mezani, tumekuta changamoto mbalimbali

ikiwemo ya kukinzana kwa sheria, yaani kanuni inaenda kukinzana na sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linazorotesha kutekelezeka kwa kanuni zile kwa sababu masharti hayajazingatiwa kwenye sheria mama. Kwa mfano, *GN* namba tisa Kanuni ya 24 imekuja kutoa adhabu ambayo tayari katika sheria ya mama imeshawekwa. Kwa mfano, ndani ya Sheria ya Leseni ya Usafirishaji Kifungu cha 36 kimekuja kuweka masharti ya kuzingatia wakati mwombaji wa leseni akienda kinyume na masharti hayo adhabu yake ni nini? Sasa Kanuni ikaja ikaweka tena masharti yale, jambo ambalo linaenda kukinzana na sheria mama na hivyo kupelekea sasa sheria ile kutokutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kada hii iweze kufikia malengo, nitoe rai kwa wale wote wanaopewa mamlaka ya kutunga sheria hizi, basi wazingatie miongozo na masharti ya utungaji wa sheria ili ziendane na sheria mama na ziweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, ninaunga mkono hoja na niwaombe Waheshimiwa Wabunge waweze kuipitisha taarifa hii ili iende kutekelezeka, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanaenzi Hassan Suluhu, ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Yahaya Mfaume, atafuatiwa na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji; Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Naibu Waziri ajiandae.

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa na mimi kuchangia mjadala huu wa Kamati ya Sheria Ndogo. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti wetu kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa ya Kamati. Mheshimiwa Mwenyekiti hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraka ya Bunge katika kutunga sheria yanapatikana katika Ibara ile ya 64 na 97. Pia, Bunge linakasimu madaraka yake katika idara mbalimbali kama inavyoonekana katika Ibara ya 97(5). Ibara ya 96 pia inaipa

mamlaka Bunge ya kuunda Kamati, na miongoni mwa Kamati hizo ni pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ni kudhibiti madaraka ambayo Bunge imekasimu kwa idara zile za Serikali katika kila sheria inayotunga ambayo inawapa nguvu ya kutunga Sheria Ndogo kwa ajili ya ufanisi wa sheria mama. Kwa kufanya hivyo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, matangazo yale ya Serikali yanapoletwa kwa ajili ya uchambuzi, huwa yanafanya uchambuzi zaidi kwa kuangalia je, kanuni zile zimezingatia Katiba ya Nchi, sheria mama na sheria nyinginezo? Kwa sababu maeneo hayo ndiyo msingi mkuu wa uhalali wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya udhibiti Sheria Ndogo zinaweza zikasababisha sintofahamu kubwa katika jamii kwa sababu ufanisi wa sheria mama kimsingi unategemea sana Sheria Ndogo. Kwa hiyo, Kamati ya Sheria Ndogo ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha inadhibiti mamlaka iliyotoa ya utungaji wa hizi kanuni ili ziendane na mawanda ambayo yanapaswa kupitiwa katika utungaji wa hizi Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika Tangazo la Serikali Na. 327 linalohusu Uundaji wa Bodi ya Mfuko wa Elimu katika Halmashauri ya Tandahimba katika Kifungu cha 25 na ukiangalia Tangazo la Serikali Na. 606 kuhusiana na masuala ya *Shipping Agencies Regulation* Kifungu kile cha 35, na pia ukienda katika Tangazo la Serikali Na. 9 linalohusiana na *Transport Licensing Regulation 2026* pamoja na Tangazo la Serikali Na. 38 linalohusiana na *Civic Aviation Regulation* katika Kifungu kile cha 61, unaona hapa taasisi mbalimbali za Serikali ambazo zimepewa mamlaka ya kutunga sheria ndogo zote zimefanya makosa makubwa ya kutoa adhabu zinazokinzana na sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pasipokuwa na udhibiti wa Bunge kupitia Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo, maana yake sheria ndogo zitajichukulia mamlaka ambayo hayapo kisheria, itakuwa nje ya mawanda. Kwa hiyo, ni muhimu kwa Kamati ya Sheria Ndogo kuendelea kufanya uchambuzi na baadaye kuleta

matokeo ya uchambuzi ule katika Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kutoa maazimio ya kurekebisha makosa yanayotokana na sheria hizo ndogo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Arif Suleiman Premji atafuatiwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Nderiananga, na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajiandae.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninashukuru kwa kupewa fursa hii. Kuna Mwanasheria mmoja alisema; "*Law touch mind, regulation touch pocket and kitchen.*" Maana yake, sheria mama inagusa akili na fikra, lakini Sheria Ndogo na kanuni hizi, zinagusa mifuko na jikoni kwa mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunapoongesa tuna sheria mama zaidi ya 450 katika nchi hii na tuna Sheria Ndogo zaidi ya 90,000 ambazo ndiyo zinahusika kwenye kuendesha maisha ya mwananchi *day to day* na zinawagusa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni muumini sana wa ukweli. Sheria hizi zinazotungwa, Sheria Ndogo je, zinaleta ufanisi wa sheria mama au zinakwenda kugeuka kuwa kipato kwa baadhi ya taasisi na baadhi ya halmashauri zetu? Inabidi tujiulize sana kwani nachelea kusema, ipo siku wapo wananchi watawatuma wawakilishi na watasema sasa ile halmashauri isiitwe halmashauri ya mji fulani, iitwe halmashauri ya tozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa nini? Tuongee kwa uhalisia na hapa ninaomba nitoe *fact* moja ambayo ni *reality*. Bajeti yetu ya 2026/2027 ndani yake ukiangalia kuna kitu wanaita *non tax revenue* ambayo ni shilingi trilioni 1.97 ambayo

wamepewa maelekezo watu wa halmashauri *(local government authority)* ndiyo inabidi ikusanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wanakusanya vipi? *By introducing by laws*. Kwa kuweka Sheria Ndogo ambazo zinakwenda kuwaumiza wananchi kwa namna moja au namna nyingine. Mfano wa uhalisi, Gazeti la Mwananchi la tarehe 9 Julai, kama sikosei, taasisi fulani inaitwa *LATRA* wakasema wanapunguza faini kutoka shilingi 250,000 ije shilingi 150,000 baada ya malalamiko mengi sana ya madereva. Huu ni mfano wa uhalisia kabisa kwamba faini hizi zinakuwa ni chanzo pia cha mapato kwa ajili ya taasisi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba sana tuondokane na ule mtazamo, ile *mindset,* tuje kwenye *compliance*. Kwa kuwa kazi ya Sheria Ndogo ni kumfanya mwananchi awe *compliant* na siyo kugeuza iwe kipato *(one of the sources of the revenue)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaishauri sana Serikali kwa kuzingatia hilo, sheria mama ipo, Sheria Ndogo ifuate taratibu, iangalie Katiba, iangalie uhalisia wa mwananchi aliyeko vijijini na mjini, *then we introduce*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii pia kuipongeza sana Serikali, kwani nilikuwa napitia baadhi ya *document* nikakutana na kitu wanaita *BTI (Bertelsmann Transformation Index),* ni taasisi au ripoti ambayo inatengenezwa Ujerumani. Ripoti hiyo ilitoka mwezi wa Juni, 2026 na ikawa inaonesha *good governance* kwa baadhi ya nchi, hasa *developing countries*. Kwa nchi yetu sisi tumekuwa *ranked* wa 45 kati ya 137. Kwa hiyo, ninaipongeza sana Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ninasisitiza sana tuzingatie uhalisia wa wananchi. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge pia mtuunge mkono sana kwenye taarifa yetu ambayo imewasilishwa na Mwenyekiti wetu wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Ummy Nderiananga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na mtoa hoja ajiandae.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uzima na afya njema hadi kufikia siku hii ya leo. Kipekee ninatumia fursa hii kutoa shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Spika, na kwako Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa pia shukrani zetu za Serikali kwa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, kwanza kwa Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii na *Secretariate* kwa ushirikiano na utendaji wao makini ambao wameendelea kuonyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, *Chief Whip*, Mheshimiwa Prof. John Aidan Mwaluko Kabudi, ninaomba kuchangia kwa kuanza kwa kuunga mkono hoja iliyowasilishwa na Kamati kutokana na uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu niungane na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati kuendelea kumpongeza na kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maono yake ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kutekeleza vyema Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, pia tunaanza kutekeleza vizuri Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 kwa kuangalia sheria zetu tulizonazo, kufanya maboresho na mabadiliko ili iende kuleta tabasamu kwa Watanzania. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza na Kanuni ya 46(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Agosti, 2025, Serikali huwa inawasilisha Bungeni katika kila Mkutano wa Bunge nakala za matoleo ya Magazeti ya Serikali pamoja na nyongeza zake. Baada ya hapo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo hufanya uchambuzi wa sheria ndogo zilizoainishwa ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, sheria mama na sheria nyingine za nchi kwa mujibu wa Kifungu cha 10 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Agosti, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu hii ni Kamati muhimu sana na imekuwa ikifanya kazi ya uchambuzi wa sheria hizo kwa weledi, uzalendo na uaminifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wamekuwa wakifanya kazi hii bila kuchoka na yote haya ni kwa sababu Kamati hii inatenda hayo yote kwa manufaa ya wananchi wetu. Nimewasikiliza Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wakichangia kwamba wananchi wa Tanzania wanapoona kuna sheria zinakinzana au zinawaumiza, wasisite kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge ambao ni wawakilishi wa Watanzania ili waweze kutuletea na sisi tuweze kufanya maboresho. Kwa hiyo, ninawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ya Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Serikali imeanza kufanyia kazi Mapendekezo na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, ambapo baadhi ya Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari, zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ili kuzirekebisha kasoro hizo ikiwemo kuwasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa mapitio na uhakiki kabla ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Aidha, kama ilivyoshauriwa na Kamati, Sheria Ndogo hizo baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali zitawasilishwa Bungeni kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, maagizo ya Kamati, tumeyapokea kwa unyenyekevu mkubwa na tunaenda kuyafanyia kazi. Ninawahakikishia, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tutasisitiza, tutasimamia na tutaratibu Wizara zote zinazohusika kama ambavyo tumekuwa tukiendelea kufanya na huwa tunawakumbusha na maelekezo ya Serikali yametolewa kwa mamlaka zote kwamba katika uandishi wao wahakikishe wanamshirikisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuepuka kasoro kama hizi. Tutaendelea kuwakumbusha wahusika ili kupunguza changamoto zinazojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru, kupongeza na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwani amekuwa akifanya kazi kubwa na nzuri na imani yetu ni kwamba kwa kushirikiana na ofisi yake, changamoto hizi zitakwenda kwisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti alipozungumza amezitaja sheria hizi ambazo zimekinzana, sheria kama mbili hivi na mimi nimeshasema, Serikali tumeanza kuzifanyia kazi. Kwa kuwa tuko pia na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndani ya Bunge hili, Mheshimiwa Hamza Johari, naye amesikia na ofisi yake inaendelea kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sioni haja pia ya kuendelea kurudia mifano hii, lakini ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mwenyekiti na Kamati kwamba tutaendelea kuwasimamia Wizara, taasisi, idara na Serikali kuzingatia maagizo yanayotolewa na Kamati yetu hii ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ili kupunguza changamoto mbalimbali zinazojitokeza mara kwa mara wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo, kwani sote tunafahamu kwamba kutozingatiwa kwa misingi ya uandishi bora wa sheria ni ishara ya uwezekano wa utekelezaji wa sheria mama usio na tija wala ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, ninaomba niendelee kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe, kwa niaba ya Serikali, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Johari Hamza, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nimesimama kwa ajili ya kujibu hoja moja ya kisheria, lakini kabla sijajibu hoja hiyo, ninamshukuru Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru pia Wajumbe mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja mbalimbali. Sasa ninajielekeza katika kujibu moja ya hoja ambayo ilikuwa inataka kupata ufafanuzi na majibu kwa nini baadhi ya Sheria Ndogo zinaendelea kuletwa Bungeni kwa lugha ya Kiingereza?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Sheria ya Tafsiri ya Sheria imeelekeza kuwa lugha ya sheria itakuwa ni Kiswahili na ni kweli kwamba baadhi ya ya Sheria Ndogo zinaendelea kuja kwa lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu ni kwamba msingi mkuu wa uandishi wa Sheria Ndogo inafuata lugha ya sheria mama. Kwa hiyo, kwa kuwa zoezi la kuendelea kutafsiri sheria zetu linaendelea, na kwa kuwa baadhi ya Sheria Ndogo ziliandaliwa kabla sheria mama hizo bado hazijaenda kwenye lugha ya Kiswahili, basi msingi wa kisheria ni kuiandika sheria hiyo ndogo kwa lugha ya sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, inapokuja kwenye Bunge hili kwa lugha ya Kiingereza, ikishapitishwa haituzuii sasa kufanya zoezi la kuitafsiri Sheria Ndogo hiyo kwenda kwenye lugha la Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii ni *guiding principle* tu ya uandishi wa sheria kwamba Sheria Ndogo zinafuata lugha ya

sheria mama. Ofisi yangu inaendelea na zoezi la ufasiri wa sheria ili kuhakikisha kwamba sheria zote zinakuwa kwenye lugha ya Kiswahili. Hadi sasa jumla ya sheria 446 tumeshazitafsiri kwenda kwenye lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, kukamilika kwa zoezi hili kutawezesha Sheria Ndogo zitakazokuja baadaye ziikute sheria mama ikiwa ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya muda fulani, karibu zote sasa zitakazokuwa zinakuja zitakuwa kwenye lugha ya Kiswahili. Aidha, kama mmebaini vizuri, ukiangalia taarifa ya Kamati ya Bunge lililopita na Bunge hili, utaona mapungufu zimepungua kwa kiasi kikubwa sana. Kwa pendekezo hili sasa la kuhakikisha kwamba wakati wa kutunga Sheria Ndogo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inashirikishwa ipasavyo, itaendelea kusaidia kupunguza changamoto tulizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tumeweka mkakati wa kuhakikisha kwamba wanasheria katika halmashauri, Wizara na taasisi wanajengewa uwezo zaidi na mafunzo zaidi katika uandaaji wa hizi Sheria Ndogo. Pia, tumeandaa sheria kifani ya Sheria Ndogo mbalimbali ambazo zitakuwa ndiyo nyenzo za kuwasaidia wanasheria katika halmashauri, wizara na taasisi wakati wa kutengeneza hizi Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunawashukuru Kamati kwa maoni yao, lakini tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge pia kwa maoni yao. Tutayachukua kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kwamba changamoto hizi zinapungua kabisa kama siyo kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, ninaongeza muda kwa mujibu wa kanuni zetu tumalize shughuli iliyoko mbele yetu. Sasa ninamwita mtoe hoja, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, ahitimishe hoja yake.

MHE. CECILIA D. PARESSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru tena kwa fursa hii uliyonipatia kwanza, ya kuwasilisha taarifa ya Kamati hapa Bungeni na sasa kuhitimisha taarifa hii kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo. Ninapenda pia kukushukuru kwa kuongoza vyema mjadala huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa pia shukrani zangu kwa wananchi wenzangu na wanachama wenzangu wa Chama cha Mapinduzi katika Mkoa wa Arusha kwa ushirikiano wanaonipatia na kwa kipekee katika Wilaya ninayotoka, Wilaya ya Karatu. Baadhi ya wanachama wenzangu na viongozi wamejumuika nami hapa leo Bungeni kwa ajili ya kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala wetu huu ulipata jumla ya Wabunge sita waliochangia hoja hii, na pia Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy Nderiananga pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari. Tunawashukuru sana kwa michango yao, maoni na maboresho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Serikali, tunawashukuru pia kwa kukubali na kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wameziwasilisha hapa Bungeni, nasi Kamati kupitia taarifa yetu, tuliziainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Ndogo ni nini au ni zipi? Kwa ajili ya ufafanuzi na kuweka uelewa wa pamoja, tunaweza kuitafsiri Sheria Ndogo kwa maana ya ndogo (udogo) au kuiona ni kitu fulani ambacho hakina uzito, lakini Sheria Ndogo hizi ni sheria muhimu sana. Ni kanuni mbalimbali zinazotungwa na mamlaka mbalimbali, amri zinazotolewa, notisi mbalimbali zinazotolewa, lakini kubwa zaidi ni sheria za halmashauri zetu nchini. Kwa mfano, sheria mbalimbali za ada na ushuru pamoja na hati mbalimbali zinazotolewa na mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukielewa umuhimu au maana ya hizi Sheria Ndogo, tunahusisha moja kwa moja matumizi ya Sheria Ndogo na wananchi wetu katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kutunga hizi Sheria Ndogo kwa mujibu wa Ibara ya 97(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge limekasimu madaraka haya kwa mamlaka kutunga Sheria Ndogo hizi. Mamlaka hayo ambayo sisi kama Bunge tunapokasimu, ni lazima tuwe makini na tuwe na wivu wa mamlaka yetu tuliyoyatoa kwa mamlaka husika kukasimu madaraka hayo. Hivyo basi, tunapaswa kuzitazama na kuzichambua hizo sheria zinazotungwa na mamlaka tuliyoikasimu na kutazama misingi mikubwa mitatu ifuatayo: isikinzane na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; isikinzane na sheria mama; na isikinzane na sheria nyingine za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, hizo sheria zinawagusa wananchi moja kwa moja wakiwemo wafanyabiashara wadogo wadogo katika halmashauri zetu, boda boda, wakulima, wafugaji, mama lishe na baba lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunatambua inawagusa wananchi moja kwa moja, ni lazima Bunge liendelee kuwa na jicho la karibu la kuzipitia na kuzichambua sheria ndogo zote ili zisilete mkanganyiko au madhara ya moja kwa moja kwa wananchi wetu ambao sisi tunawawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana utaona hapa michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge imejikita kuendelea kusisitiza kwamba mamlaka iliyopewa dhamana ya kutunga sheria hizi ni lazima ziakisi yale yaliyoainishwa ya kutokinzana na sheria mama na kuleta raha na furaha kwa wananchi wetu bila kuleta bugudha yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, msingi wa mjadala wa Kamati yetu na maazimio tunayoyaleta hapa umewekwa na sheria ya nchi kupitia Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kwamba Sheria Ndogo zinatungwa kwa utaratibu bila kuleta ukinzani wala kuleta tafsiri iliyokuwa ya utatanishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuziruhusu mamlaka hizi kutunga Sheria Ndogo, ingewezekana Bunge sisi kutunga hizi

Sheria Ndogo, lakini ili kuleta ufanisi na kuakisi mazingira na kufanya urahisi katika utekelezaji, ndiyo maana Bunge tumezipa mamlaka hayo mamlaka mbalimbali kutunga hizo Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi huo ndiyo unasababisha leo Bunge kupitia kanuni zetu tulizoziweka kupata fursa ya kupokea taarifa hii, kuichambua, kutoa maoni na hatimaye kuweka Maazimio ya Bunge ambayo sasa mamlaka husika itaenda kuyatekeleza kwa ajili ya kuleta ufanisi na kuakisi kile kinachoonekana kwenye Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango iliyotolewa katika mjadala huu inaonyesha uwakilishi sahihi wa wananchi wa kutambua nafasi halisi ya Sheria Ndogo katika maisha ya kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema haya machache, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu pamoja na kuzingatia michango ya Wabunge waliochangia, ipokee taarifa hii na kupitisha mapendekezo yaliyotolewa ili yawe Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. KHAMIS ALI VUAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Wote tumeafiki, kwa hiyo, tunatangaza rasmi kwamba taarifa ya Kamati, maoni na mapendekezo yote yamekubaliwa na Bunge Zima.

Ninachukua nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Cecilia Paresso; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Yahya Mfaume, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi nzuri na kubwa mliyofanya. Ni matarajio ya Bunge kwamba maoni na mapendekezo ya Kamati yatatekelezwa na kusimamiwa na Serikali kwa ajili ya ustawi wa wananchi wetu wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema maneno haya tumefika mwisho wa shughuli ambazo zipo kwenye orodha ya leo. Kuna matangazo machache kabla hatujafika mwisho kabisa.

Wageni waliopo Bungeni muda huu ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni 12 wa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, ambao ni marafiki zake kutoka Kibakwe mkoani Dodoma. Karibuni sana *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi, Mbunge, hiki ni kikundi cha mtandao wa vijana wajasiri-kilimo Tanzania kutoka Morogoro, Mbeya na Zanzibar. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia, tunao wageni 25 wa Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, ambao ni wafanyabiashara wa *Unique Mamas* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 50 wa Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, Mbunge, ambayo ni timu ya washindi wa Kafiti *Cup* kutoka Wilaya ya Ilemela Jijini Mwanza. Ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Katika ligi hiyo washindi ni *Kawekamo FC*, hongereni sana. Mnaye Mbunge makini hapa Bungeni, Mheshimiwa Kafiti, Mbunge wa Ilemela anawawakilisha vizuri sana. Hongera sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao viongozi na vijana sita wanufaika wa *Fountain Gate Foundation*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 86 na walimu 15 wa Shule ya Sekondari Ng'ong'ona kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 16 wa Chuo cha *Nangwa Vocational Training Center* kutoka Mkoani Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 7.04 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 4 Septemba, 2026 Saa Tatu Asubuhi)

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA